Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADIILANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Tisa – Tarehe 17 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

### MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba Sera ya Ubinafsishaji madhumuni yake makubwa ilikuwa ni kuongeza pato, ajira na ufanisi. Shamba la Kapunga Mbarali lenye hekta 5,500 lilibinafsishwa na aliyepewa analima hekta 100 tu kati ya 5,500. Je, huu ni utekelezaji sahihi wa sera ya ubinafsishaji?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba tunaye mwekezaji pale Mbarali kwenye shamba la Kapunga na anaendelea kupanua lile shamba kadri ya uwezo alivyokuwa ameupanga. Kwa hiyo, mimi nadhani kubwa pale ambalo wote tunatakiwa kulijua na kulifuatilia kama Watanzania ni kuona ni kwa kiwango gani ameweza kutimiza yale ambayo tulikuwa tumekubaliana kwenye mkataba wetu.

Sasa nadhani katika hali kama hiyo utakuta pengine ndiyo hali iliyopo kwenye maeneo mengi. Hajaondoka, hajahama kwa hiyo, mimi nadhani ni vizuri tukakubali kwamba jitihada zipo anaweza kuwa na mapungufu ya hapa na pale. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alikwenda Mbarali na akapata kuonana na wananchi wakilalamika kwamba mwekezaji huyu mbali tu na kwamba alikuwa amewazuia hata mifereji ya kumwagilia maji katika mashamba yao, lakini vile vile anawakodisha kwa shilingi milioni moja kwa hekta moja na wakamwomba Rais kwamba shamba hili lichukuliwe lirudishwe kwa wananchi.

Je, kitendo cha kumwachia Mwekezaji afanye hivyo na huku tuna sera ya MKURUBITA ambayo inataka kuwarasimisha wananchi. Je, hatuoni kwamba Serikali inakwenda kinyume na sera hiyo ya MKURUBITA? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, of course ni jambo kidogo gumu kwa sababu ni mambo yetu ya kisheria kwa namna tulivyoingia mikataba. Unachokiona pale kwamba baada ya ubinafsishaji ule, shamba lile ni mali yake na ni jukumu lake kuliendeleza. Sasa kama wako Watanzania ambao kwa mpango ulivyo wanaona wanachelewa na wanakubali kukodishwa ili shamba lile liweze kutumika kwa ufanisi zaidi, hilo ni jambo jingine. Lakini tungependa tunachoweza kufanya ni kufuatilia kuona mpango wenyewe hasa umefikia hatua gani kulingana na makubaliana tuliyokuwa tumewekeana.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Takribani miaka 2 iliyopita Serikali ilitueleza juu ya dhamira yake ya kuanzisha Mtandao wa Serikali *(E-Government)* na hii ilikuwa ni dhamira nzuri kwa nia ya kuiunganisha Serikali na kuboresha utendaji wake.

Je, ni kwa kiwango gani baada ya mfumo huo kuanzishwa umefanyakazi na umeweza kuinufaisha Serikali katika kipindi hiki cha miaka miwili?

Kama mfumo huu umeunganisha Serikali na imefanya kazi vizuri ni kwa nini baadhi ya watendaji wa Serikali bado kuna migongano katika maelezo ambayo yanatokana na utendaji wake?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Killimbah, swali lake kama ifuatavyo:-

Kwanza nikuombe tu radhi kwa sababu ni jambo ambalo kidogo lina utalaam ndani na sina undani sana wa wapi jambo hili limefikia ili tuweze kukupa jibu ambalo ni sahihi zaidi. Lakini, ninachoweza kusema tu ni kwamba ni kweli kwamba Serikali tulianzisha mradi huo na Idara Kuu ya Utumishi chini ya Ofisi ya Rais, ndio wanaosimamia eneo hilo. Utaratibu umekwishaanza na unaendelea, sasa sidhani kama baada ya kuanzishwa basi mara moja migongano yote ya upatikanaji wa taarifa itapatikana kwa sababu inategemea watumiaji wanavyotumia *facility* hiyo ni kwa kiasi gani. Lakini inawezekana lisiwe kamilifu sana pengine nitamwomba Dada yangu Hawa Ghasia akipata muda aweze kuzungumza na wewe ili akupe hasa mambo yalivyo kwa hivi sasa ili uweze kuridhika. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunijibu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini nilikuwa nataka Serikali itupe maelezo labda katika moja ya waathirika wakubwa na masuala haya ya kuweza kutendewa kazi haraka ni wastaafu na hasa wanapodai mafao yao.

Je, hawa wastaafu hawa waliopo vijijini, ambao wanadai mafao wanaweza wakaunganishwa katika mtandao huu ili wasiwe na usumbufu huu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama suluhu inapatikana chini ya mfumo wa *E- Government* inawezekana ndiyo, lakini inawezekana vile vile isiwezekane. Lakini ninachojua ni kwamba pale Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ambayo inashughulika na masuala ya pensheni walipewa hilo jukumu la kujaribu kurahisisha mfumo ili watu hawa wa pensheni waweze kuwa wanapata huduma hiyo kwa haraka zaidi.

Kwa hiyo, katika hatua ya awali kwanza ilikuwa ni kuingiza majina ya wale wote wastaafu ambao wako chini ya pensheni kwenye mfumo ambao utawezesha rekodi zao ziweze kupatikana kwa urahisi, jambo ambalo nafurahi tu kusema kwamba kwa sehemu kubwa kazi ile imeshafanyika na ndio maana hata sasa unaona kuna unafuu kidogo katika uwezeshwaji na upatikanaji wa pensheni za wafanyakazi. Lakini ni kweli kwamba changamoto bado ni kubwa, tunahitaji kuendelea kuboresha. Kwa hiyo, naamini kabisa eneo hili litakapokuwa limekamilika tutaweza kufanyakazi hiyo kuwa nyepesi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupewa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka jana Serikali iliunda vikosi kazi zaidi ya vitatu kuchunguza zoezi zima la hamisha mifugo lililofanyika kinyume na taratibu maeneo mbalimbali hapa nchini. Leo ni mwaka wa pili, hakuna taarifa yoyote iliyotolewa juu ya uchunguzi huo uliofanyika. Leo Serikali inawaambia nini Watanzania?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilifanya hilo zoezi, iliunda hiyo timu, timu ilifanya kazi ikamaliza hiyo kazi, ikatukabidhi na sisi tumeishalishughulikia kwa kiasi kikubwa. Tumekwishatoa maelekezo kwa wale wote ambao walibainika kwamba walifanya zoezi hilo vibaya wachukuliwe hatua za kisheria na baadhi yao wako mahakamani hivi sasa tunavyozungumza. Kwa hiyo, taarifa ile ilikuwa ni kuisaidia Serikali kuwezesha kuelewa kina cha tatizo lilivyokuwa na kama kuna wahusika waweze kuchukuliwa hatua zinazostahili.

Sasa bado tunangoja tuone mwisho wa zoezi hilo la wale waliofikishwa mahakamani nini ili tuweze kusaidiwa kuweza kujua tunakwendaje sasa kwa maana ya upana wa zoezi lenyewe. Kwa hiyo, kazi tulifanya na imekamilika.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali ilitamka hapa Bungeni kwamba wafugaji walionyang'anywa mifugo yao watalipwa. Nini hatma ya wafugaji hao mpaka sasa ukizingatia wengi wao walifilisiwa na wana hali ngumu ya maisha na hata watoto wao wameshindwa kwenda masomoni? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema ndio tulisema hivyo au hapana. Lakini la msingi hapa ni kwamba lengo la kutaka wale wote waliohusika wapelekwe mahakamani ni kutaka kujua kwa uhakika hali ya kisheria ilivyo katika masuala yote ambayo yamehusiana na zoezi lile. Kwa hiyo, yale mapungufu ndiyo yatakayotusaidia kufanya uamuzi baada ya pale tunachukua hatua gani kwa wale wote

ambao itabainika kwamba kama mtu alishtakiwa ametiwa hatiani maana yake ndiyo kusema kwa mifugo ambayo alikuwa amehusika nayo ni dhahiri Serikali lazima tutazame tuseme tunafanyaje katika mazingira hayo kwa sababu aliyehusika ni mtumishi ambaye tulikuwa tumemweka kufanya hiyo kazi ndiyo hasa ilikuwa lengo letu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika zoezi la uandikishaji wapiga kura kwenye Daftari la Kudumu, baada ya wananchi kupata elimu ya kutosha wengi walijitokeza na kujiandikisha katika Daftari la Kudumu ili waweze kupata haki ya kupiga kura. Endapo wapiga kura hawa siku ya kupiga kura kitambulisho chake kikawa kimepotea au kikapotea siku mbili kabla ya kupiga kura; Je, ni jinsi gani Serikali itawasaidia wapiga kura hawa waweze kupiga kwa sababu ni haki yao ya kimsingi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu alikuwa amejiandikisha na anayo kadi ya mpiga kura halafu kwa bahati mbaya imepotea au pengine imeungua au imeibiwa, mimi nadhani kubwa tunachoweza kusema pale ni kwamba kama akiweza kujieleza na kujitambulisha mapema katika vyombo vinavyohusika napenda niamini kwamba huyu hawezi kupoteza nafasi ya kupiga kura kwa sababu hiyo. Kunaweza kufanyika utaratibu mwingine haraka wa kumwezesha kwa sababu majina yake na rekodi zake zote zitakuwepo.

Kwa aina hii ya Mtanzania sidhani kama tunaweza kuwa na tatizo kubwa pengine nitaiomba tu Tume ya Uchaguzi Taifa watakapokuwa wanatoa maelezo juu ya wale wanaotaka kuhamisha data pengine na hili walieleze vizuri ili Watanzania waweze kujua hali itakuwaje endapo itatokea hivyo. (*Makofi*)

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Nne, kwa nia na dhamira njema ikipeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri, Serikali za Mitaa na madhalani sekta ya barabara za vijijini imeongezeka kutoka shilingi bilioni 23.4 kwenda shilingi bilioni 83.5 ongezeko ambalo ni mara tatu au zaidi. Kwa maana hiyo, ukiangalia kwa sekta zote ziko Halmashauri ambazo zinapata zaidi ya shilingi bilioni 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji ambao ndiyo wenye Halmashauri, wasimamizi wa shughuli za maendeleo na walinzi wa fedha hizi Madiwani kwa mfano wanalipwa kutoka shilingi 60,000 mpaka 120,000 wakati Wenyeviti wa Vijiji wanaolazimika kuwasimamia watendaji hawapewi posho yoyote na mimi nalinganisha kama mtu mwenye duka kubwa lenye mamilioni anamkabidhi mlinzi alinde kwa kirungu kitu ambacho kinaekelea hizo mali zitapotea na kuibiwa wakati wowote.

Ni lini Serikali yako itafanya maamuzi bila kigugumizi kwa kuangalia uwiano wa fedha zinazopotea kwenye Halmashauri  na  malipo ya Madiwani na posho kwenda kwa Wenyeviti wa Vijiji ili kuweka motisha ya Madiwani kufanya kazi vizuri na pengine

kuweka ile sehemu ya kivutio iweze kupata watu wenye sifa nzuri zaidi na hivyo kuboresha utendaji wa kazi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Naamini umeeleweka kabisa.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni watu ambao tunaelewa tatizo hili kwa kina tunatamani sana Wenyeviti wetu wapate posho au hata mishahara.

Hali kadhalika hata Madiwani tungetamani sana wapate posho zaidi kuliko pengine hicho wanachokipata, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba bado uwezo wa Serikali si mkubwa na wote hapa mnafahamu.

Kwa hiyo, tunachoweza kusema tu ni kwamba kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unaongezeka juhudi zitafanyika kuendelea kuongeza posho, hata hapo walipofika Madiwani posho hiyo haikuwa hivyo tulijitahidi tukaongeza kidogo na ndio maana imefikia mpaka 120,000. Kwa hiyo, ni suala la uwezo tunaamini tunaweza tutaweza kufikia huko siku zinazokuja tukiwa na uchumi mkubwa.

Lakini kwa upande wa Wenyeviti, tulichokwisha kuagiza Halmashauri zote wafanye ni kuhakikisha kwamba wanalipwa posho kutokana na fedha ambayo tunarejesha kwao kama sehemu ya fidia kwa sababu tuliondoa vyanzo fulani vya kodi na tulisema formula itakuwa ni ile ile ambayo ilikuwa inatumika wakati walipokuwa wanakusanya mapato. Sasa pengine tuendelee kutoa maelekezo kwa Halmashauri hizo kama zipo, ziko ambazo mimi najua zinafanya lakini, inawezekana wako wachache ambao hawatekelezi hilo agizo kwamba waendelee kutekeleza hilo jambo tena bila kusita kwa sababu wanalijua na lilikwishaagizwa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa vile suala la Madiwani ni suala muhimu Mheshimiwa Lubeleje, swali la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Kwa kuwa baada ya Mabaraza ya Madiwani kuvunjwa, Waheshimiwa Madiwani watatakiwa kulipwa mafao. Je, Serikali imeweka utaratibu gani ili kuwalipa mafao yao Madiwani na je, Serikali imetenga fedha hizo kwa ajili ya kuwalipa mafao Madiwani baada ya kumaliza muda wao? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niamini kwamba jambo hilo litatekelezwa kwa sababu tulitoa kauli, tuliahidi kwamba jambo hilo tutalifanyia kazi, tutawalipa watakapokuwa wametimiza muda wa kipindi chao cha miaka mitano. Kwa hiyo, siamini kwamba ni jambo ambalo liko nje ya uwezo wetu, nafikiri fedha ipo sijawasiliana na Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, lakini tutahakikisha wanalipwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana! Huo ndio mwisho wa maswali yaliyokuwa mezani yakielekezwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunamshukuru sana kwa majibu mazuri na ya uhakika kwa maswali yote aliyoulizwa.

Sasa tunaendelea na maswali ya kawaida na naomba tuanze na swali kwa Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, swali namba 64 ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Ndesamburo, namwona Mheshimiwa Suzan Lyimo.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 64

### Kuzuia Uharibifu wa Mazingira Katika Mlima Kilimanjaro

**MHE. SUSAN A. LYIMO: (K.n.y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, inaaminika kuwa baada ya miaka kumi (10) kutoka sasa barafu iliyopo juu ya Mlima Kilimanjaro itayeyuka na kupotea kabisa kwa sababu ya uharibifu wa mazingira unaofanywa na binadamu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuokoa Mlima huo ambao ni kivutio kikubwa cha watalii?

(b) Je, kunaweza kukatokea ukosefu wa maji ikiwa barafu yote itayeyuka na kupotea?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kufuatia kupungua kwa theluji katika Mlima Kilimanjaro na kama wanavyosema watafiti kuwa theluji hiyo imepungua kwa asilimia 80, jitihada mbalimbali zinafanyika Kimataifa na Kitaifa. Jitihada hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuzibana nchi zinazozalisha kwa wingi gesijoto kuliko kiwango kinachokubalika kisayansi, kupunguza uzalishaji gesijoto kwa kupitia majadiliano yanayoendelea chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi *(UNFCC).*

(ii) Kuanzishwa kwa Mfuko wa Fedha ili kusaidia nchi zinazoendelea kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, pamoja na kutokufikiwa kwa makubaliano ya kisheria muhimu huko Copenhagen; makubaliano yaliyofikiwa hasa katika miradi mikubwa ya Mpango wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ya Ukaa inayotokana na Ukataji wa Miti na Uharibifu wa Misitu (MKUHUMU) unaolenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta ya misitu.

(iii) Kuendelea kutoa elimu ya kutosha kuhusu uhifadhi na utunzanji wa mazingira kwa wananchi wanaozunguka Mlima Kilimanjaro.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya *(EU)* imeanza mchakato wa kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Kitaifa cha Kitaaluma cha Mabadiliko ya Tabianchi *(The Kilimanjaro International Climate Change Centre of Excellence)* mkoani Kilimanjaro ambacho pamoja na mambo mengine kitatoa elimu na kitakuwa kituo cha utalii kwa maonesho ya kiikolojia kwa kukusanya aina mbalimbali za mimea. Aidha, upembuzi yakinifu wa kuanzishwa kituo hiki umeanza.

(iv) Kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Shirika la Hifadhi ya Taifa ya Mlima wa Kilimanjaro *(KINAPA)* juhudi mbalimbali zinaendelea kufanywa za kudhibiti uchomaji moto na upandaji miti. Aidha, shughuli za doria kukabiliana na ujangili unaosababishwa na uchomaji moto unafanywa na *KINAPA* kwa kushirikiana na Kikosi cha Operesheni Maalum cha Jeshi la Polisi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuyeyuka kwa barafu au theluji katika Mlima wa Kilimanjaro ni dalili za ongezeko la joto duniani. Theluji ikiyeyuka na maji yakivukizwa *(evaporate*) kwenda angani na kama mvua ikaathirika kimtawanyiko kutakuwa na uhaba wa maji. Aidha, ukipima chemchem katika ukanda wa chini wa Mlima Kilimanjaro takwimu za kiekolojia zinaonyesha kwamba chemchemu ya maji inaongezeka wakati wa kiangazi.

Hii inaonyesha kwamba kiasi fulani cha theluji kinayoyeyuka kwenye Mlima Kilimanjaro ndiyo inaongeza maji chini ya ardhi katika ukanda huo. Kuna uwezekano wa kupungua kwa upatikanaji wa maji katika vyanzo vya maji kutoka Mlima Kilimanjaro kwa miaka ijayo iwapo theluji itapotea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuhimiza uongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro na wananchi wote kwa ujumla kuongeza jitihada za kutunza mazingira ya Mlima huu, hasa kwa kuthibiti uchomaji moto ovyo wa maeneo ya mlima huu na kuongeza juhudi za kupanda miti kwa wingi. Mlima huu ni urithi wetu lakini vile vile ni hazina siyo tu kwa nchi yetu ni kwa Afrika na dunia kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mlima Kilimanjaro ni fahari na urithi wa Tanzania na kwa kuwa mlima huu umekuwa kivutio kikubwa sana kwa watalii ambao wanaingiza pato kubwa

nchi yetu. Lakini pamoja na fahari hiyo na uharibifu unaotokana na kuchomwa au na gesijoto bado uharibifu unaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Killimbah *microphone* zenu zina shida kidogo zinaingiliana na utaratibu. Mheshimiwa Susan anza tena swali lako.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mlima Kilimanjaro ni fahari na urithi wa Tanzania na kwa kuwa Mlima Kilimanjaro unaingizia pato kubwa sana nchi yetu lakini kutokana na uharibifu wa mazingira na kupotea kwa theluji pale bado inaonekana katika bajeti ya mwaka huu hakuna fungu maalum lililotengwa kwa ajili ya kurudisha hadhi ya Mlima huu. Je, Waziri anaweza kutuambia kama kuna fungu maalum?

Pili, kwa kuwa sababu kubwa ya kupungua kwa theluji hiyo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni uzalishaji mkubwa wa gesi joto katika nchi nyingi. Na kwa kuwa bado kuna baadhi ya nchi ambazo zinazalisha gesi joto hizo kwa wingi hazijasaini mkataba wa Kyoto ikiwemo Marekani. Je, Serikali ya Tanzania inadhani ina ushawishi gani katika kusaidia nchi hizo ziweze kusaini mkataba kwani hiyo ndiyo sababu muhimu inayopelekea Mlima wetu kupungua kwa barafu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Kilimanjaro ni jambo ambalo kama nchi, tunalichukulia na tunalipa kipaumbele kikubwa na katika Bajeti yetu nadhani katika Wizara ya Maliasili na Utalii katika maeneo ya *TANAPA* utaona eneo na fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Lakini vile vile sisi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira katika moja ya maeneo na kama nilivyosema tuko katika majadiliano na Umoja wa Ulaya kwa ajili ya kuanzisha kile kituo cha Kimataifa cha Mabadiliko ya Tabianchi ambacho kitakuwa pale Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari fedha zimeshatengwa kwa ajili ya mtaalamu mwelekezi wa kufanya uchambuzi na kuandika mchoro kwa ajili ya kituo hicho. Baada ya hapo fedha tutazipata kupitia *initiative* hiyo hiyo ya Umoja wa Ulaya.

Lakini vile vile kuna miradi mbalimbali ambayo tunafanya, kuna mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kama nilivyoeleza Mradi wa MKUHUMI ambao tuna jumla ya dola milioni 100 kupitia Mfuko wa Norway na katika moja ya vitu tutakavyofanya ni kurudisha uoto wa asili katika maeneo ya Tanzania lakini hususan katika eneo hilo la Kilimanjaro.

Aidha, kuhusu Serikali jitihada gani zinafanywa kuweza kuzibanana kuzishawishi nchi ambazo zinaongeza gesi duniani kuweza kupunguza gesi hizo, kama nilivyozieleza katika makubaliano tuliyoyafikia kupitia *Copenhagen Accord* tulikubaliana kwamba majadiliano yaendelee kufanyika. Kufikia mkataba wa kisheria ni hatua moja ngumu

sana lakini ni hatua muhimu. Kilichofanyika pale Copenhagen ni kuziwezesha zile nchi ambazo zilikuwa haziko mezani kuanza kuingia katika meza na kujadiliana na ndio nchi kama Marekani zikaanza kuingia ambako kule Kyoto zilikuwa hazipo katika mchakato huo.

Sasa hivi tuko katika majadiliano ya kuelekea Cancun Mexico ili kuona nchi ziko tayari kiasi gani kufikia makubaliano ya kisheria. Lakini pamoja na kutokufikia makubaliano ya kisheria jitihada zinafanyika kuweza kupunguza gesi joto hizo na kuendeleza hatua za kuweza kupanda misitu kutumia utaalamu ule wa kuweza kuzishawishi nchi hizi zinazoweza kupanda misitu katika nchi za Afrika na nchi zingine ili kupunguza gesi joto kule. Lakini vile vile na wenyewe kuingia katika teknolojia ambayo itatumia nishati ambayo haitachafua mazingira.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mlima wa Kilimanjaro una msitu mnene haina haja ya kupanda miti. Tatizo ni watu kuchoma moto kila wakati. Je, Serikali inachukua hatua gani kwa hawa watu wanaochoma msitu huo kila wakati na sijawahi kusikia mtu aliyekamatwa na pande zote moto unawaka kila wakati wa kiangazi. Je, Serikali haisimamii msitu ule vizuri?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS , MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mlima wa Kilimanjaro eneo kubwa ni eneo ambalo lina uoto wa asili ambapo huhitaji kupanda miti. Lakini tunapozungumzia Mlima wa Kilimanjaro tunazungumzia *attachment* nzima ya maeneo mpaka ya chini yanayozunguka eneo kubwa tu ambalo linazunguka mlima ule. Kwa hivyo ni muhimu kabisa kwamba pamoja na maeneo yale yote yanayozunguka Mlima Kilimanjaro ni budi tuhifadhi na tukaendelea kupanda miti.

Ama kuhusu uchomaji moto ni kweli suala hilo limekuwa gumu na shughuli hizi zinavyofanyika, zinafanyika katika mazingira ambayo ngumu kuweza kumkamata mtu. Sasa hivi tulichokifanya ni sisi Ofisi yetu ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Jeshi la Polisi kuingia makubaliano ya kiutendaji ili sisi tugharamie fedha za mafuta na kikosi kile cha doria kikaweza kupita na kuweza kufanya *surveillance* kuweza kuwakamata hao majangili. Kwa hivyo tumelichukulia suala hili kwa umuhimu na tuna hakika kabisa safari hii tutawakamata na kupitia sheria yetu wale watu watachukulia hatua na wataweza kufungwa na faini ni kubwa kama mnavyoelewa. *(Makofi)*

Na. 65

**Leseni Kwa Wachimbaji Wadogo Wadogo wa Madini Misungwi**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI (K.n.y. ESTHER K. NYAWAZWA)** aliuliza:-

Kata ya Ilujamate, Wilaya ya Misungwi kijiji cha Buhanda, kitongoji cha Ishokelahela kuna wachimbaji wadogo wadogo wa Madini ya Dhahabu ambao Serikali

imewasimamisha kuchimba Dhahabu na Kampuni ya *"I AM Gold"* ifanye utafiti ambao umeanza tangu mwaka 1998:-

(a) Je, ni lini Serikali itatoa leseni kwa wachimbaji hao?

(b) Je, ni lini Kampuni hiyo itamaliza utafiti?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ya Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijawasimamisha wachimbaji wadogo kwenye eneo lote la Kijiji cha Buhunda, Kitongoji cha Ishokelahela Wilayani Misungwi. Wachimbaji walisimamishwa kuchimba kwenye eneo lenye leseni ya utafutaji wa madini *PL 1563/2000* lenye ukubwa wa kilometa za mraba 24.29 lililokuwa linafanyiwa kazi za utafutaji madini na Kampuni ya *IAM Gold.* Kampuni hiyo baada ya kufanya kazi kwenye eneo hilo ililipunguza ambapo sasa imebakiza kilometa za mraba 12.1 tu.

Eneo lililopunguzwa na Kampuni ya *IAM Gold* limegawiwa kwa wachimbaji wadogo kupitia leseni ndogo tano za uchimbaji mdogo wa madini zenye Namba *PML 0010097* na *PML 0010098* zinazomilikiwa na kikundi cha Vijana Wachimbaji wadogo wa Madini Buhunda *(Kiviwamabu Group), PML 0010909, 0010078* na *0010079* zinazomilikiwa na wachimbaji wadogo wengine.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *IAM Gold* inaendelea kulifanyia kazi eneo ililolibakisha na imeomba *Retention Lincence* ili kuchukua fursa hiyo kuendelea kubaini kiasi cha mashapo yaliyopo na kama yanaweza kuchimbwa kwa faida. Pale Kampuni itakapobaini usahihi wa mashapo hayo ndipo itakapoamua kuanzisha au kutokuanzisha mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la kuwapatia wachimbaji wadogo maeneo ya kufanyia kazi ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ambazo Wizara yangu ilitoa hapa Bungeni. Ushiriki wa *STAMICO* ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati huu.

Napenda kurudia tena kwamba nia ni kuwapatia wachimbaji wadogo na lengo ni kuwawezesha kufanya kazi zao kwa usalama, lakini pia kuongeza tija katika uzalishaji. Ili hili lifikiwe ni lazima wachimbaji wajenge tamaduni ya kufanya kazi kwenye vikundi vya ushirika. Hivyo, kama ilivyokuwa kwa kikundi cha wachimbaji wadogo cha KIVIWAMABU, napenda kutumia nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na wadau wenzangu katika uchimbaji mdogo, kuhamasisha vikundi na kuzingatia sheria na taratibu ili tupate mafanikio na tija iliyo kubwa zaidi. *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na

majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza nimpongeze yeye kwa jinsi Wizara yake ambavyo imeweza kuendelea kuwajali wachimbaji wadogo wadogo. Nampongeza sana.

Swali la kwanza kwa kuwa ahadi ya Serikali imekuwepo ya kuendelea kuwajali wachimbaji wadogo wadogo ambao wamejiunga katika vikundi na tayari yeye mwenyewe ameshuhudia kabisa kwamba vikundi vitano tayari viko kule Buhunda hali kadhalika pale Mwabuki kuna vikundi tayari vimejiunga na mliahidi kwamba kuna mfuko wa Serikali kwa ajili ya kuwasaidia hao mfuko huo umefikia wapi? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri ulipotembelea Wilaya ya Misungwi katika kijiji Seki, wananchi wengi sana walijitokeza kukusikiliza na wengine walikuuliza maswali hususan katika eneo la Ishokela, Seke, Nyamainza pamoja na Buhingo. Uliwahamasisha wewe mwenyewe wawekeze kwa maana ya kwamba wajenge nyumba nzuri kwa sababu umeme utakuja. Unawaahidi nini wananchi wa Seke, Nyamainza na Buhingo jinsi ulivyozungumza nao wewe mwenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Serikali iko palepale kwa sababu ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Hili suala la vikundi halikuishia kwenye jimbo la Misungwi tu, isipokuwa tumejaribu kufanya hivyo kwa wachimbaji wadogo wadogo popote watakapokuwa kwa kadri uhamasishaji ambao unategemea sana nguvu na jitihada za wenzetu pale ambao wako pale pale viongozi wa maeneo husika. Kwa mfano naomba niseme kule Busanda kwenye maeneo ya Rwamgwasa na Nyarugusu na maeneo kule ya Bukombe, Kapente kule kwa Mheshimiwa Jumanne Luhahula, kule Ulanga kwa Mheshimiwa Cellina Kombani ni maeneo ambayo yote tunahamasisha wachimbaji wadogo wadogo kwa kujua kwamba uwezeshaji wa mchimbaji mmoja mmoja hauwezi kuwa na tija. Lazima tuwawezeshe tukipeleka vifaa uwe ni kwa ajili ya wachimbaji wote kwa pamoja na wao wenyewe watafanya utaratibu wa kusimamia uwezeshaji ule uliopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuzingatia hayo Serikali ilitenga mfuko wa shilingi bilioni moja. Bilioni moja ni kianzio, mfuko huo ni mdogo lakini pia kuna *Sustain Management Programme for Mining* ambayo inasimamiwa pale Wizarani ambayo inapata fedha kutoka kwa wafadhili na tunategemea mfuko huo utaendelea kuchangiwa na vyanzo vingine vya fedha. Kwa hiyo, naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mfuko huo upo isipokuwa unaendelea na taratibu ili tujue namna tutakavyowasilisha ili mgao huo uwe na tija kwa wachimbaji wadogo.

Kama ulivyosema mwenyewe hili la pili Mheshimiwa Mbunge amenichomekea kidogo. Lakini labda niseme tu hili la umeme wa Seke tulikuwa tumelizungumzia kama jambo la muhimu kwa sababu wachimbaji wa pale na shughuli zote za kiuchumi za maeneo yale kusema kweli zikipata umeme zitaboreka sana. Kwa hiyo naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba utekelezaji huu uko chini ya utekelezaji wa mradi wa *MCC* ambao tumeutolea maelezo, nadhani Jumanne au Jumatatu wiki hii.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKIMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kero za wachimbaji wadogo katika Wilaya ya Misungwi ni sawa kabisa na kero za wachimbaji wadogo wadogo katika jimbo la Busanda. Ningependa kujua hasa katika maeneo ya Nyarugusu, Sabora kule Kaseme ambao walifungiwa machimbo kwa sababu ya baadhi ya watu kufa katika machimbo hayo.

Pia katika maeneo ya Rwamgwasa ningependa kujua Serikali ni lini itatoa leseni kwa wachimbaji hawa ili waweze kuendelea kuchimba madini kama kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipotaja maeneo ya jimbo la Busanda nilitegemea kwamba Mheshimiwa Lolencia hatosimama.

Lakini kwenye ziara hiyo tuliyofanya ya Wizara tuliokwenda Misungwi pia tulikwenda Jimbo la Busanda na pia tulikwenda kuangalia shughuli za wachimbaji wadogo Bukombe na ndiyo maana nikasema kwenye haya maeneo yote aliyoyataja ya Nyarugusu, Sabora, Kaseme Rwamgwasa tayari Serikali imeshatenga maeneo ambayo tumewapatia. Suala la hapa ni kwamba wachimbaji wadogo wanasema kwa maeneo yaliyotolewa maeneo yale yamekuwa hayakidhi kwa maana yamekuwa ni madogo.

Utaratibu na nadhani Mheshimiwa Mbunge tayari ameshawaleta wachimbaji wadogo mimi binafsi nimekutana nao. Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amekutana nao, tumekubaliana kwamba tunafanya tathmini ya yale maeneo ambayo yametolewa *I AM Gold* ambayo yanaweza kufanyiwa kazi kwa ufanisi kwa sababu ule uchimbaji mdogo mwenyewe lazima ufanye kwa ufanisi, ukiwapa maeneo ambayo uwezo hawana ya kuwapatia tija hatuwatendei haki.

Kwa hiyo, kwa sasa hivi eneo lile linafanyiwa uchunguzi, *STAMICO* wako wanaohusika, GST wanahusika, Wizara inahusika na tukipata tathmini iliyokuwa sahihi kwa vyanzo vyote hivi basi Serikali itatoa leseni kwa maeneo ya nyongeza ili kukidhi mahitaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo haya ya Sabora, Kaseme, Rwamgwasa na Nyarugusu.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Tatizo la Serikali kuwasimamisha wachimbaji wadogo wadogo mbali na huko Rwamgwasa na Buhanda pia limetokea Geita katika kijiji cha Mgusu.

Baada ya kutokea maporomoko na watu wakauawa na Waziri Mkuu akayafunga mashimo hayo kwa muda wa miezi mitatu. Lakini imekaa muda mrefu mno mpaka sasa hivi unakaribia mwaka machimbo hayo hayajafunguliwa. Katika taratibu za kuhamasisha wanachi hao ili wapewe maeneo waliambiwa waunde asasi ambayo itasaidiwa.

Lakini matokeo yake asasi iliyoundwa iliwashirikisha wakubwa tu wale wachimbaji wadogo wadogo wakaachwa. Matokeo yake ikatokezea hata wachimbaji wadogo kufanya maandamano na kufanya risasi zikafumuka wengine wakaumizwa.

Je, Serikali sasa itafanya mpango gani wachimbaji wadogo wadogo wale ambao walikwepa kuwekwa katika kundi la asasi ya kusaidiwa, asasi yao ikafikiriwa na aweze kufunguliwa machimbo hayo kwa faida ya kizazi chao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mgusu sio suala nadhani umeliweka kidogo sio sawa. Umesema watu baada ya kutokea ajali watu wakauawa, watu hawakuuawa, walikufa, ni tofauti kidogo.

Sasa ni jambo la kawaida tu kwamba si jambo kawaida lakini ni ajali. Imetokea ajali kwa sababu ya jambo ambalo Serikali tunalisema kila siku kwa uchimbaji mdogo mdogo. Hata kwenye majibu yangu ya msingi nimesema lengo la Serikali ni kuwatengenezea utaratibu wachimbaji wadogo ili ule uchimbaji uwe salama na uwe na tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefika Mugusu na nimeongea na wananchi na katika kuwasihi pale kwenye eneo lile la Mlima uliopatikana ajali tulilizungumza hili kama kabla hata ya ajali. Tukasema mazingira yanayofanywa pale ya uchimbaji ni hatarishi.

Kw hiyo, tukasema Serikali tukae pamoja na wachimbaji wadogo wadogo wa Mgusu ili tuangalie namna ya kujenga mazingira mazuri zaidi ili uchimbaji uwe na salama zaidi. Sasa katika hili pia pale pana suala la Mwekezaji ambaye anaitwa *Shanta Mining*. Lile suala la mwekezaji limeingia mgogoro pale kwa sababu kuna mambo ambayo yalitokea awali ya kihistoria ambayo yameleta mgogoro.

Sasa hivi tunalifanyia kazi ili lile suala la mwekezaji tutaangalia kama anaweza kufanya kazi kwa kushirikiana. Ametoa pendekezo la namna ya kufanya kazi ya kushirikiana pamoja na wachimbaji wadogo. Tutaliwasilisha, kama wako radhi kufanya kazi kwa njia hiyo ya ushirika na mchimbaji mkubwa inawezekana, kama haiwezekani inabidi tutafute njia nyingine.

Lakini lazima niseme pale Mugusu kuna watu ambao wako pale, kihistoria wale lazima tuzingatie kwamba ni Wanamugusu, halafu kuna wahamiaji waliotoka Mkuranga, waliotoka Pemba, waliotoka Mkanyageni, wako pale. Wanazamia machimbo yale yakitoa dhahabu. Sasa wale nao wanaleta mazingira kidogo ambayo usimamizi unakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimsihi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hili jambo linafanyiwa kazi na hata wiki mbili zilizopita tulikuwa tunazungumza na Mkuu wa Wilaya pale ili kumpa pendekezo akaliwasilishe kwa wananchi na

Mheshimiwa Mbunge wa pale ili waangalie namna watakavyoridhia kwa sababu hili ni jambo shirikishi, lazima tushirikiane nao ili kufikia maamuzi na hatima ya Mugusu.

Na. 66

**Mgodi wa Nyamongo Tarime Kuwa na Madini Mengi**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA (K.n.y. MHE. CHARLES N. MWERA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mgodi wa Nyamongo uliopo Wilayani Tarime unaomilikiwa na Kampuni ya Barrick unasemekana kuwa na Madini mengi ya dhahabu:-

(a) Je, ni kiasi gani cha dhahabu kimepatikana tangu mgodi huo uanze uchimbaji hadi sasa, na ni kiasi gani cha fedha kimepatikana?

(b) Je, Serikali imepata shilingi ngapi kutokana na dhahabu iliyochimbwa katika mgodi huo na wananchi wa Nyamongo na vijiji jirani wamepata kiasi gani cha fedha katika gawio hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2002 hadi 2008 mgodi wa *North Mara* umeshazalisha dhahabu yenye uzito wa wakia 1,638,091 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 843,212. Thamani ya dhahabu inayozalishwa kwa kila mwaka inatofautiana kwa kuwa bei ya dhahabu kwenye masoko ya dunia hubadilika mara kwa mara na uzalishaji pia umekuwa ukiongezeka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kujua mapato ya Serikali kutoka kwenye mgodi kama ule wa *North Mara,* inabidi kuangalia mapato kwa ujumla wake *(direct and indirect benefits).*

Kwa mujibu wa mfumo wa kodi unaotumika hivi sasa katika sekta ya madini, Serikali inaweza kupata mapato yake moja kwa moja *(direct benefits)* kupitia maeneo makuu yafuatayo (kwa mgodi wa dhahabu) *Royalty 3% of Net Back Value, Corporate Income Tax 30%, Dividend Withholding Tax 10%, witholding Tax on Technical Services and Management Fees 5% for local and 15% for foreign Contractors, Import Duty for equipment and machinery 0% during exploration and 5% after commencement of mining, VAT special relief, PAYE, skills, development levy, fuel levy, Local Government levy, licence fees and annual rents and expatriate payroll taxes.*

Pia Serikali inanufaika na shughuli za uchimbaji (*indirectly*) katika maeneo yafuatayo:-

*Foreign Direct Earnings* kutoka kwenye mauzo ya madini. Hivi sasa mauzo ya madini yanachangia zaidi ya asilimia 52 ya thamani ya mauzo ya bidhaa zote nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hicho miongoni mwa mapato ya moja kwa moja yaliyopatikana ni kiasi cha mrabaha kilichokusanywa na Serikali, Dola za Marekani milioni 24.789. Mbali na mrabaha, Serikali pia iliweza kupata kiasi cha Dola za Marekani milioni 26.492 kutokana na kodi na tozo mbali mbali kama vile *PAYE, Fuel levy* na *Excise Duty.*

Aidha hadi kufikia mwaka 2008 mgodi huo umekwishatumia kiasi cha Dola za Marekani zisizopungua milioni 2.00 katika kuchangia uendelezaji zisizopungua milioni 2.00 katika kuchangia uendelezaji wa huduma mbalimbali za kijamii kama vile kwenye miradi ya elimu, afya, maji na kilimo kwa jamii inayozunguka mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapokea mapato tofauti kwa njia mbalimbali. Yapo mapato ambayo yanapitia Halmashauri husika moja kwa moja na yapo mapato ambayo yanapitia mfuko Mkuu wa Serikali. Yale yanayopitia Halmashauri ni kama haya ambao yameainishwa hapo awali.

Aidha yapo mapato ya Serikali ambayo yanaingia kwenye Mfuko wa Serikali (*Basket Fund*). Hivyo haiwezekani kujua ni kiasi gani cha fedha iliyokusanywa na Serikali kutoka mgodi wa *North Mara* iliyotumika kuhudumia vijiji jirani na mgodi huo.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali kwamba michango inayochangiwa na migodi mbalimbali hasa inayofusiana na majengo, majengo hayo baadhi yao hayajengwi katika ubora unaostahiki. Je, ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa kuwajibisha mgodi unahusika na kadhia hii ya kutapeli wananchi katika migodi hiyo?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Jecha lirudie kwa taratibu zaidi.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeuliza kwamba kuna baadhi ya wananchi wanalalamika kwamba baadhi ya michango inayochangwa na migodi hasa ya majengo, majengo haya yanajengwa kwa kiwango kisichostahiki. Je, ni hatua gani zinazostahili kuchukuliwa kuuwajibisha mgodi utakaobainika unawatapeli wananchi ambao wanaozunguka maeneo haya ya mgodi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa anachosema Mheshimiwa Mwadini kuna kile kipengele cha *Social Responsibility* ambacho hii migodi inatakiwa iwe inatoa huduma fulani na misaada fulani kwa zile jamii zanazowazunguka. Kwa kawaida matarajio au utaratibu huu unatakiwa ushirikishe viongozi wa zile jamii zinazohusika. Sasa wanafanya mambo mawili ama wanaweza wakatoa pesa ule ujenzi ukafanywa na zile jamii zenyewe ama hawa

wanaweza kujenga kama madarasa au kituo cha Afya na kadhalika wakawakabidhi jamii husika.

Sasa kwa kusema ukweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kama wao wanajenga jengo halafu wanalikabidhi jengo lile linakuwa dhaifu, kusema kweli lazima wananchi wayafikishe malalamiko hayo kwa Serikali ili sisi tukabiliane nao kwa sababu huu unakuwa ni ujanja ambao haukidhi haja na haukubaliki.

Lakini ikiwa kama ile hela ilitolewa pesa ikaenda kwenye uongozi wa jamii, wakajenga jengo baya, basi hilo sasa linakuwa jambo la upande wa pili. Kwa hiyo, hapo ambapo pana tatizo kama hili labda tufikishiwe sisi Wizarani tutakabiliana nalo kwa bidii kabisa.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa maeneo ambayo imeanzishwa miradi hii mikubwa ya madini huwa wananchi wenyewe wanaelewa matatizo na mahitaji yao. Ni kwa nini Serikali kabla haijaingia mkataba na Makampuni haya isiwe Serikali yenyewe imefanya utafiti kujua maeneo haya yanashida gani kwa mfano kama ni barabara, shule nakadhalika ili ikaingizwa ndani ya mkataba ule toka mapema ili makampuni haya yasiwe na hiari kufanya yale mamb ya kijamii katika migodi inayohusika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye makubaliano yale ya awali ambayo yanapelekea kuanzisha mkataba huu wa *MDA* pana kitu ambacho Mheshimiwa Mbunge analifahamu ambayo inaitwa *Environmental and Social Impact Assessment* ambayo lazima ifanywe kabla haifikia hatua yoyote ya kuingiza kwenye Mkataba.

Sasa kwenye ile *Environmental and Social Impact Assessment* mara nyingi unapomaliza mgodi ambapo palikuwa na makazi ya watu, palikuwa na hospitali lazima kuna kitu kinaitwa *Resettlement Plan* ambayo lazima iwe ni sehemu ya makubaliano ya utekelezaji wa mgodi huo.

Kwa hiyo, mimi nadhani kama ni kweli *Environmental and Social Impact Assessment* imefanywa na *Settlement Plan* imefanywa na haikuzingatia mahitaji ya msingi ya wale wananchi ambao wanaathirika moja kwa moja na kuwepo ule mgodi, mimi nadhani labda hapo nilitafutie maelezo na ushahidi lakini nadhani hilo jambo linakuwa halikufanywa sawasawa.

Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Hamad Rashid kwamba katika Kamati ya Nishati ya Madini wakati wa kujadili Sheria mpya ya Madini hili jambo limezingatiwa sana na limehimizwa kwamba liwe ni jambo mojawapo ambalo kabla hatujaingia kwenye *MDA* lazima maslahi ya wananchi ambao wanaathirika na mgodi kisha mgodi ukishaanza yawe ni kipaumbele chetu katika makubaliano yoyote yanayofikiwa. *(Makofi)*

Na. 67

## Ujenzi wa Kituo cha Uhamiaji Kirongwe

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI** aliuliza:-

Serikali imekubali kujenga kituo cha Uhamiaji Kijiji cha Kirongwe Wilayani Rorya na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala alipotembelea eneo hilo alilahidi kuwa kituo chicho kilichoko mpakani kitaendelezwa ili kutoa huduma za biashara/soko.

(a) Je, mpango huo bado unaendelea?

(b) Je, Tanzania imejiandaa vipi kutumia fursa hiyo adimu katika kuanza mchakato mapema wa kuendeleza kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol asrungi, Mbunge wa Rorya, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimmiwa Sarungi, kwa jitihada zake za kufuatilia kwa umakini masuala mbalimbali yanayohusu jimbo lake la Rorya. Katika mkutanowa kumi na tisa (19) wa Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alipokuwa akijibu swali Na. 21 la tarehe 14 Aprili, 2010 kuhusu ujenzi wa kituo cha uhamiaji Kirongwe alieleza kuwa Wizara ya Mambo ya ndani ya Nchi inakusudia kuanza ujenzi wa kituo hicho katika mpango wa utekelezaji Ndani ya Nchi unakusudiwa inakusudia kuanza ujenzi wa kituo hicho katika mpango wa utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Sarungi kuwa nia ya Serikali ya kujenga kituo hicho cha Uhamiaji iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wananchama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekubaliana kuhakikisha kuwa biashara inafanyika kwa wepesi na watu wanavuka mipaka kwa urahisi kwa kuanzisha utaratibu wa vituo vya pamoja vya utoaji huduma mipakani *(One stop Border Post).*

Kutokana na umuhimu wa eneo la Kirongwe ambalo lipo mpakani mwa Tanzania na Kenya mara baada ya ujenzi wa kutuo kuanza Wizara yangu hii itaanza mchakato wa kuzungumza na Serikali ya Kenya kuona uwezekano wa kuanzisha kituo cha pamoja cha kutoa huduma mipakani. Namwomba Mheshimiwa Sarundi pamoja na wananchi wa Rorya wawe na subira kwani taarifa zitatolewa pindi mchakato utakapokalimika.

**MHE. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Rorya napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenye matumaini. Pamoja na pongezi hizo ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kwa kuwa majirani zetu upande wa Kenya wameanza ujenzi kwa kasi kubwa sana. Je Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa tayari kuanza ujenzi wa kituo hicho Julai 2010?

Swali la pili. Wakati wa kupima viwanja katika Kituo cha Kirongwe. Je, wakazi wa kijiji cha Kirongwe na vijiji jirani watapewa upendeleo maalum wa kuwa w akwanza kupatiwa viwanja hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Sarungi kwamba ujenzi wa kituo hicho anachokizungumza uko palepale kazi itaanza kama Julai, 2010 na itategemea pesa zitakapoingizwakwenye Bajeti lakini imewekwa katika *Vote 93* ya Uhamiaji.

Pili napenda nimhakikishie Mheshimiwa Sarungi kwamba nina hakika katika upimaji wa viwanja katika maeneo yale Wizara husika itatoa kipaumbele kwa wale ambao wako pale ambao Mheshimiwa Sarungi anataka wafikiriwe.

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa kutokuwa na kituo cha Uhamiaji katika kijiji cha Kirongwe Wilayani Rorya ni sawa kabisa na kutokuwa na kituo cha Uhamiaji katika Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro, yaani Loliondo na hali ambayo imekuwa ikipelekea Watanzania wa maeneo yale kuitwa Wakenya wakati ni Watanzania. Ni lini Kituo cha Uhamiaji kitajengwa katika Mji wa Loliondo au Waso ili kuondokana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ningependa kumjibu Mheshimiwa Telele, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana kwa namna ambavyo anafuatilia masuala ya Jimboni kwake na ningepende kueleza kwamba hata jana tumeongea na Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala hili. Kama nilivyoahidi jana tulivyoongea nitachukua nafasi ya kwenda kutembelea eneo na wataalam wangu na kuangalia uwezekano wa kujenga kituo muda utakapokuwa muafaka.

Na. 68

**Kukosekana kwa Matangazo ya TBC Rukwa**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mkoa wa Rukwa hususani Wilaya ya Sumbawanga, haupati matangazo ya *TBC* wakati wote kutokana na umbali uliopo toka vituo vya Mbeya na Kigoma. Kwa kuwa, tatizo hili ni la muda mrefu na wananachi wamekwishalalamika kwa vyombo husika bila kuwepo kwa maboresho yoyote.

(a) Je, kuna fahari gani kwa Mkoa huo kukosa matangazo kwa kipindi cha zaidi ya miaka 50 sasa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanakosa matangazomuhimu ya kuboresha kilimo, elimu na mengineyo na badala yake wanasikiliza radio za nchi jirani tu?

(c) Je, ni lini Mkoa wa Rukwa utapata mtambo wake wa *TBC* ili wananchi wapate elimu bora?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna fahari yoyote siyo tu kwa Mkoa wa Rukwa na hata mikoa mingine hapa nchini kwa kukosa matangazo yanayotolewa na shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* kwani kuwa na fahari kuna maana ya kujivunia jambo fulani kutokana na mafanikio yaliyotokea.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa kukosa matangazo muhimu yanayotolewa kuptia *TBC* Taifa, wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanakosa mambo mengi muhimu kama alivyotolea mfano wa masuala yanayohusu elimu, kilimo na kadhalika.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utoaji wa huduma hiyo Mkoani Rukwa, tayari ujenzi wa kituo cha kupokea matangazo umekamilika na kimejengwa eneo la King’ombe Wilayani Sumbawanga.

Hivi sasa ujenzi umekamilika na matangazo ya *TBC* Taifa na *TBC FM* yanaptikana. Napenda kuchukua nafasi hii kuwajulisha wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuwa Redio yao ya Taifa hivi sasa iko hewani mkoani humo. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Bado jitihada hizo kubwa zilizofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kuwajengea kituo cha kurushia matangazo. Je, Serikali itakuwa tayari kupokea pongezi na shukrani za wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa kazi hiyo kubwa? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Mbeya una kituo cha kurushia matangazo cha *TBC* Taifa pale Mbeya bado usikivu wa matangazo ya *Radio Tanzania* katika maeneo mengi ya Mkoa wa Mbeya si mzuri na hususan maeneo ya Kata za Isansa kule Mbozi, Kata za Kamsamba, Kapele Nyimbili lakini na maeneo mengi ya Wilaya ya Chunya.

Je, Serikali itafanya kazi, jitihada gani kuhakikisha kwamba kituo chetu cha kurushia matangazo ya *TBC* Taifa pale Mbeya kinapewa mitambo ya kisasa ili matangazo yasikike vizuri Mkoani Mbeya?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya Waziri wangu na kwa niaba ya Serikali nipokee pongezi za Mkoa wa Rukwa na nchi nzima kwa jinsi ambavyo *TBC* inafanya kazi nzuri ya kuendelea kuhabarisha Wananchi katika nchi nzima. Kwa hiyo, ninapenda nizipokee ni utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kweli kuwa kuna baaadhi ya Mikoa ambayo *TBC* haifiki. Lakini ninataka nimhakikishie Ndugu yangu kuwa kwanza kwa Mkoa wa Mbeya tayari Serikali imesha nunua mtambo mpya wa kuongezea usikivu katika maeneo ambayo ameyataja. Lakini kubwa zaidi ni kwamba ile Mikoa yote tisa iliyobaki, Mikoa hiyo ikiwa ni Shinyanga, Mkoa wa Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Mbinga, Rukwa kwa maana ya kuendeleza zaidi Mpanda,Mtwara, Ruvuma na wenzetu jirani Zanzibar tayari ifikapo mwisho wa mwezi wa *September TBC FM* itakuwa inasikika Mikoa yote. Kwa hiyo, hatutakuwa na Mkoa wowote katika nchi hii ambao hauna usikivu wa redio kwa maana ya *TBC. (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwamba muda wa maswali umekwisha na tunaenda kwa wakati kwa uendeshaji wa Sayansi na Teknolojia wa Mwenyekiti wenu wa Bunge. Sasa ni wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Tunae Mheshimiwa Balozi Robert Orr, Balozi kutoka Canada ambaye ni Balozi wa Canada nchini Tanzania na ameambatana na Dada Florence Mndolwa, Kamishna wa Biashara Ubalozi wa Canada karibuni sana Bungeni, Canada ni nchi rafiki karibuni sana. Tunao wageni wa Mheshimiwa Lawrence Masha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao ni Damary Komba, Rais wa Serikali ya Wananfunzi *CBE Mwanza.* Wengine ni Manusura Lusigaliye, Waziri Mkuu wa Serikali ya Wanachuo yule pale, Ndugu Emmanuel Magarinza, ambaye ni Rais wa Serikali ya wana chuo *CBE Dodoma* na Riziki Mvungi, Waziri Mkuu wa wananchuo *CBE Dodoma* karibuni sana vijana hili ni Bunge lenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, ambaye ni Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma

ambao ni pamoja na Ndugu Abbas Rashid Mpunga - nyoosha mkono, Ndugu Mkombozi Juma, Ndugu Jacob Anney na Ndugu Wilbruger Costantine. Pia kuna Wageni wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ni Isaya Japheth - Mwalimu, Ndugu Abubakar Kupaza Mwalimu, Ndugu Patrick Yohana - Mwanafunzi, Ndugu Raphael Mwambashi msimame wote wanafunzi, Ndugu Faraja Msuya, Ndugu Stephen Kigosi, Ndugu Rogers Augo, Ndugu Robert Haule, Ndugu Joyce Chedi, Ndugu Regina Mtunguja - karibuni sana wanajumuia ya Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Karibuni sana hapa Bungeni na mimi ndiyo muwakilishi wenu kwenye Baraza la Chuo Kikuu cha Dodoma. Nilitaarifu tu Bunge letu Tukufu aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye hotuba yake jana ni kweli chuo kinakuwa kwa haraka sana na udahili wa *September* na *October* mwaka huu 2010 kwa Chuo Kikuu cha Dodoma peke yake ni wanafunzi 10,000. Ukipata hiyo picha ya 10,000 ni kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inatekelezwa. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Professor Jumanne Maghembe, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni pamoja na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, Ndugu Mamboleo Teri, Diwani wa Ngujini Theresia Msuya, Diwani wa Kirya Twalib Kahungo Msuya, Saidani Mshana Mtendaji wa Kata ya Kirya, Fihiri Msuya Mtendaji Kata ya Kifula kule Ugweno na John Shigela, Afisa Mipango wa Wilaya ya Mwanga. Karibuni sana Ndugu zangu kutoka Mwanga. *Professor* tuko naye hapa na kazi yake mnaifahamu tuna tumaini mtaendelea kumwunga mkono, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, ni pamoja na Mwenyekiti wa Wazazi wa Wilaya ya Bagamoyo Ndugu Kassim Mrisho Gogo, ambaye amefuatana na mkewe Mama Kathe karibu sana. Wageni wa Bunge *Sports Club* kutoka *Serengeti Breweries LTD.* ni Ndugu Winston Kagusa, ambaye ni *General Manager Corporate Affairs* karibu sana, Ndugu Gerald Madala *PR Manager* wa *Northen Zone* na Ndugu Teddy Mapunda - *General Manager Media and Corporate* upande wa *PR* karibuni sana tunatumaini mtafanya kazi vizuri kwa kushirikiana na *Bunge Sports Club* ambayo ina *record* kubwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Godfrey Zambi, ambao pia wanatoka *UDOM* ni hawa wafuatao naomba wasimame wote kwa mpigo. Ndugu Anishie Nuhu, Ndugu Mziho Augustine, Ndugu Sambwilimwaya Emmanuel, Ndugu Mwakafilwa Waziri, Ndugu Paza Diana, Ndugu Leonard Shule, Ndugu Jesca Kwanga, Ndugu Andrew Namayala karibuni sana vijana kutoka *UDOM* Bunge hili liko karibu namaeneo ya Chuo chenu, kama nilivyosema mwanzo mnakaribishwa sana kujifunza na kutembelea Bunge lenu kila mnapopata fursa ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Tunajivunia sana mnapokuja mara kwa mara sasa hivi mko 15,000 wakiongezeka 10,000 mtakuwa 25,000 tunaamini Mabunge yajayo yatakuwa na wageni wengi zaidi kutoka *UDOM.* Mwisho ni mgeni wa Mheshimiwa Suzan Lyimo ambaye ni Ndugu

Boney Ngowi, ambaye ni mumewe na anastoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *(Statistics).* Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi za vikao vya Kamati na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wenyeviti wote walioitisha vikao hivi wameniambia kuwa vikao hivi vitakuwa ni vifupi sana kwa hiyo, muhudhurie bila kukosa. Kwanza ni kikao kinachoitishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama wakutane leo tarehe 17 Juni, 2010 saa tano hii asubuhi, katika ukumbi Namba 219.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anawaomba Wabunge wote wanawake wa CCM saa tisa alasiri kikao kitakuwa Ukumbi wa Pius Msekwa. Lediana Mng'ong'o saa tisa ambaye ni Katibu wa Wabunge Wanawake wa CCM kikao Ukumbi wa Msekwa. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo tarehe 17 Juni, 2010 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo kifupi kuanzia saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa (B). *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira inaombwa ikutane saa saba mchana jengo la Utawala ukumbi Namba 227 kwa kikao kifupi kikao hicho kinaitishwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Ndugai. Katibu kwa hatua inayofuata. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 - Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na orodha yangu kwa kweli ni kubwa ninaendelea kusisitiza dakika kumi ujikite kwenye mada ili na wengine wapate nafasi. Tunaanza kama tulivyosema jana Mheshimiwa Paschal Degera, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na wengine nitawataja kadri ratiba inavyonionyesha.

**MHE PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza leo hii ama asubuhi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza kuchangia napenda nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri kwa Hotuba yake nzuri sana. Aidha nimpongeze Waziri wa nchi TAMISEMI pia kwa hotuba yake nzuri ambayo ina uchambuzi wa kina. Pia nianze kuipongeza Serikali ya awamu ya nne kwa utekelezaji mzuri sana wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005 maeneo mengi ya Ilani hii yameguswa na yametekelezwa katika nchi nzima pamoja na Wilaya ya Kondoa,. Hata

hivyo, wapiga kura wangu pamoja na wananchi wa Wilaya ya Kondoa wamenituma nifikishe kero zao chache za Wilaya na Jimbo la Kondoa Kusini Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya kwanza ni ukubwa wa Wilaya ya Kondoa napenda kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya Kondoa na Hususani Jimbo la Kondoa Kusini kuishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa kuunda Kata 13 katika Wilaya ya Kondoa. Kata hizo 13 lengo lake ni kusogeza huduma za Serikali karibu na Wananchi kwa hiyo, napenda nishukuru na kupongeza hizo Kata 13 zilizoongezwa na kufanya Wilaya ya Kondoa kuwa na jumla ya Kata 48 hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na maombi ya Kata wananchi wa Wilaya ya Kondoa kupitia Halmashauri yao walituma maombi ya kugawa Wilaya ya Kondoa katika Wilaya mbili. Mwaka jana nilipokuwa ninachangia hotuba ya Waziri Mkuu nilieleza kwa kina matatizo wanayopata Wananchi wa Wilaya ya Kondoa kutokana na ukubwa wa Wilaya yenyewe na katika majibu yake Mheshimiwa Waziri Mkuu alikubali ama alikubaliana na hoja yangu kwamba Wilaya ya Kondoa ni kubwa sana na inahitaji kugawanywa. Lakini hadi sasa hatujaona matokeo yoyote na napenda nikumbushie tena kwamba tunahitaji ama tunaomba Serikali ichukue hatua za dhati kabisa ya kugawa Wilaya ya Kondoa katika Wilaya mbili lengo ni lilelile la kusogeza huduma karibu na wananchi kwa hiyo naomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia tetesi kwamba Serikali ina utaratibu wa namna hiyo ama kuna mchakato unaoendelea sasa pamoja na mchakato wa ujumla naomba na Wilaya ya Kondoa iwemo kwenye mchakato huo. Katika Jimbo la Kondoa kusini kero moja kubwa ni uhaba wa maji napenda pia hapa niipongeze Serikali kwamba kwa kutambua tatizo hili katika *programme* ya maji na usafi wa mazingira vijijini ambayo inagharamiwa na Benki ya Dunia jimbo la Kondoa kusini limepewa miradi 22. Miradi hiyo iko katika vijiji 22 navyo ni Kuru, Mtakuja, Jenjeluse, Mvunga, Goima, Songolo, Madaha, Hamai, Churuku, Kinkima, Jinjo, Jangalo, Bitolwa, Longia, Mapango, Chandama, Gorogoroti, Machiga, Magasa, Mwaikisape, Gonga na Lusangi ni vijiji 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tushukuru kwa *programme* hii lakini kinachogomba hapa ni kwamba utekelezaji bado unachukua muda mrefu sana vijiji hivi viliahidiwa tangu mwaka 2004. Lakini hadi sasa miaka mitano imepita miradi hii bado haijatekelezwa kwa niaba ya wapiga kura wa jimbo la Kondoa kusini naomba sana Serikali ichukue hatua ya kusukuma ama hatua za haraka kutekeleza miradi hii ili kero ya maji iondoke katika hivi vijiji nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza juu ya kero ya maji katika Jimbo la Kondoa Kusini, sasa niende kwenye ujenzi wa barabara. Barabara ya kutoka Iringa, Dodoma hadi Babati napenda niipongeze sana Serikali kuwa katika Bajeti ya mwaka huu imetenga pesa za kuridhisha kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Iringa hadi Dodoma. Lakini kitendawili kipo kwenye barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati nikirejea kwenye takwimu barabara ya Iringa Dodoma imetengewa shilingi bilioni 50.575 ni pesa ama ni kiwango cha kuridhisha kwa kweli na inawezekana mradi ukaanza

hivi karibuni lakini kwa upande wa barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati kiwango kilichotengwa ni kidogo mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shilingi bilioni 9.5645 kwa hiyo, ninao wasiwasi mkubwa kwamba huenda barabara hii ya kutoka Dodoma kwenda Babati ina puuzwa na Serikali kwa muda mrefu. Lakini kubwa napenda nikumbushie mwaka jana wakati tukijadili Bajeti ya Wizara ya Miundombinu Serikali ilipobanwa na maswali ya Wabunge Serikali kwa kauli moja kwanza kupitia kwa Waziri wa Fedha na Uchumi na kupitia kauli ya Waziri Mkuu iliahidi kwamba ingetenga shilingi bilioni 45 nje ya Bajeti na kuiwezesha ama kazi ya kuanza kujenga barabara ya lami kutoka Dodoma kwenda Babati iweze kuanza. Lakini ninasikitika kusema kwamba hadi leo ahadi hii haikutekelezwa sasa tunajiuliza hivi Serikali inatoa ahadi ambazo hazitekelezeki kwa nini? Si wangetuambia tu mwaka jana jamani eh! Hatuna pesa kwa hiyo mvumilie.

Lakini kauli ya kutuambia kwamba kuna bilioni 45 zitatengwa nje ya Bajeti ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami iliyotolewa mwaka jana ninashindwa kuelewa Serikali inataka kuwaambia nini wananchi wa maeneo haya. Naomba kwa kuwa ilikuwa ni ahadi na ahadi ni deni naomba basi Serikali itekeleze ahadi yake. Ninajua kuna hatua mbalimbali zimechukuliwa, naambiwa kuwa mpaka sasa kipande cha barabara kutoka Dodoma hadi Mayamaya imetangazwa na Mkandarasi amepatikana sasa sijui pesa hizo zitatoka wapi ili kazi hii iweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia kwako Serikali itekeleze ahadi yake. Jambo la mwisho linahusu usambazaji wa umeme vijijini na hasa katika Jimbo la Kondoa Kusini ninaipongeza pia Serikali kwa kuteua vijiji kumi vya Chandama, Jangalo, Mlongia, Mwailanje na Isusumya. Naunga mkono hoja. *((Makofi/Vicheko)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huu ni mwaka wa tano kama walivyosema Wabunge wenzangu na ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuweka mpaka tukafika siku ya leo kwa rehema zake ninamshukuru sana. Nina washukuru sana pia Wabunge wote, wa vyama vyote, wa rangi zote. *(Makofi)*

Nimeishi na ninyi kwa miaka mitano na nimejifunza mengi sana kutoka kwenu mmenifundisha mengi, ahsanteni sana. Muhimu ni kuwa nimetengeneza marafiki wengi sana ambao sikuwa nao kabla ya kuwa Mbunge ninawashukuru sana na kwangu mimi hii ni hazina kubwa sana katika maisha yangu ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Wananchi wa Chunya walionichagua na kwa miaka mitano hii, tumefanya kazi kubwa sana. Tumefanya kazi kubwa sana ya kuwabadilishia maisha wananchi wetu, kujenga mashule, kuboresha shule za msingi, kujenga shule za sekondari, kuchimba visima vya maji na kujenga zahanati. Ahsanteni sana Wananchi wa Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la muhimu kwangu ni kwamba, nawashukuru Wananchi wa Chunya kwa sababu wamenifundisha jambo jipya; wamenifundisha kutoa

na hii ni karama. Ni jambo kubwa sana mwanadamu mmoja kuwasomesha yatima 60 katika Wilaya yake. Hii ni karama kubwa ambayo Wananchi wa Chunya wamenifundisha; nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niseme tu kwamba, Chunya ni Wilaya kubwa sana; asilimia hamsini ya Mkoa wa Mbeya ni Wilaya ya Chunya, lakini kimaendeleo Chunya iko chini sana. Wakati Wananchi wa Mkoa wa Mbeya kipato chao kwa wastani kinaelekea karibu laki sita mpaka saba, Wananchi wa Chunya ni laki mbili, kwa hiyo inatakiwa Wananchi wa Chunya tukimbie wakati wenzetu wanatembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na Mheshimiwa Degera kwamba, kuiomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuigawa Wilaya ya Chunya ziwe Wilaya mbili kwa sababu ya ukubwa wa eneo lake. Najua Waziri Mkuu atatufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri pamoja na Waziri wa TAMISEMI. Ninaomba niseme machache kwenye Hotuba hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Kilimo Kwanza, naishukuru sana Serikali kwa kubuni jambo hili la Kilimo Kwanza kwani tuna rasilimali kubwa sana, inabidi tuitumie rasilimali yetu hii ili kuboresha maisha ya wananchi na kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mkoa wa Mbeya ilitembelea Nchi ya China yanapotoka matrekta, *power tillers*, nikagundua kwamba, kwenye viwanda ambavyo wanatengeneza matrekta hayo gharama ya kununua trekta, kuisafirisha na kuilipia Bima mpaka Bandarini Dar es Salaam haizidi milioni tatu, wakati matrekta hayo hayo hapa nchini kwa mawakala na madukani yanauzwa karibu milioni kumi. Ninaomba Serikali ifikirie wazo la kuruhusu Mkoa wa Mbeya na Mikoa mingine ambayo wanataka kwenda kununua kwenye *source* waruhusiwe wakanunue kwa sababu Sheria ya Manunuzi haikatazi kufanya *single sourcing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali kwa kuwa na vocha na pembejeo za ruzuku. Pamoja na nia nzuri sana ya Serikali ya kuweza kuwafikishia wakulima wetu pembejeo kwa bei nafuu, kuna tatizo la mawakala; mawakala bado ni kikwazo kwa sababu wao wanataka kufanya biashara na Serikali inataka kusaidia watu. Ninaomba katika mwaka huu wa 2010/11 kwenye msimu wa kilimo, tuangalie sana mawakala ambao wanachafua ile nia nzuri ya Serikali ya kuweka pembejeo za ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la Kilimo Kwanza, ninaomba Serikali ifanye mapinduzi ya mtazamo, tuwe tunahubiri yanayotoka moyoni na ambayo tunayatenda, kuanzia viongozi wa juu mpaka wa chini. Tukisema Kilimo Kwanza iwe Kilimo Kwanza kweli kweli, tunaweza kuiga hata kwa wenzetu wa Malawi; ni nchi ndogo lakini wamefanya Mapinduzi makubwa sana ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja wa shirika la nje alisema Malawi kuna njaa miaka miwili, mitatu iliyopita, nataka nilete chakula lakini Rais wa Malawi

alimfukuza yule mtu. Akataka wafanye mapinduzi ya kuondoa njaa wao wenyewe, sasa hivi Waziri wa Kilimo wa Malawi ni Rais mwenyewe, ina maana hadhi ya Waziri wa Kilimo ni kubwa. Hapa kwetu tuifanye hadhi ya Waziri wa Kilimo iwe juu kama ilivyokuwa hadhi ya Waziri wa Fedha ili tulete mapinduzi ya *mind set* kuhusu Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ni kuishukuru Serikali; katika Mkoa wetu wa Mbeya kuna Kata kama nne ambazo zimeinuliwa hadhi kuwa Mamlaka ya Miji Midogo. Katika Wilaya ya Chunya, Kata ya Makongorosi imekuwa Mamlaka ya Mji Mdogo; katika Wilaya ya Kyela, Mji Mdogo wa Kyela umeinuliwa hadhi kuwa Mji Mdogo; na katika Wilaya ya Mbozi, Kata ya Vyawa na Tunduma zimeinuliwa kuwa na hadhi ya Miji Midogo. Ninaishukuru sana Serikali kwa jambo hili, kwa sababu hii inaleta maendeleo karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinatutatiza na nitamwomba Mheshimiwa Kombani wakati anahitimisha hoja hii atupe ufafanuzi. Panapokuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo; je, Diwani wa hapo anakuwa na *status* gani; kunakuwa na Diwani ama hakuna Diwani? Je, mchakato wa kuja kuwa na Mbunge sehemu hiyo unakwendaje? Nitamwomba sana Mheshimiwa Kombani atupe ufafanuzi hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka niongelee matumizi ya Serikali. Bajeti yetu ni kubwa; shilingi trilioni kumi na moja. Ninataka nikuhakikishie kwamba, katika hii shilingi trilioni kumi na moja; karibu asilimia 80 inakwenda kwenye manunuzi yote, kwa hiyo ninaiomba Serikali ifikirie sana kuziba mianya kwenye manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jambo zuri sana la kuajiri na kufundisha wahasibu. Mwaka 2006 iliajiri wahasibu wengi sana ikawafundisha ikawapeleka kwenye Halmashauri, mwaka huu tena imeajiri wahasibu imewafundisha na kuwapeleka kwenye Halmashauri. Hili ni jambo zuri sana kwenda kudhibiti matumizi ya fedha kwenye Halmashauri zetu, lakini unapodhibiti matumizi ya fedha bila ya kumuweka sawa anayezitumia hizo fedha, unakuwa unatwanga maji kwenye kinu.

Ninaiomba sana Serikali iajiri na kuwafundisha wanataaluma ya manunuzi, hawa ndiyo wanaotupotezea sana fedha. Serikali iwaajiri na kuwafundisha wanunuzi ambao wanakwenda kwenye Halmashauri zetu kuitumia Sheria ya Manunuzi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, utaona Serikali yetu vyanzo vya fedha ni vidogo lakini matumizi hayapungui yanaongezeka. Wenzetu katika *Region* hii matumizi yao yanapungua sisi yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu amesema mwanzo wa mwaka huu katika Bunge la mwezi wa pili kwamba, Serikali itapunguza matumizi kwa kununua magari, lakini cha ajabu ndiyo ununuzi umeongezeka mara dufu. Ninaiomba sana Serikali tupunguze matumizi, ukinunua gari Moja *Land Cruiser VX G8* ni shilingi milioni mia mbili, wakati *Land Cruiser Standard* ambayo ni *four wheel drive* kama ilivyo VX ni shilingi milioni 140; sasa hii tabia ambayo tunayo mpaka uwe na VX naomba tuiache.

Wenzetu wa Rwanda walipiga mnada magari yote ambayo yana bei kubwa na wanatumia magari madogo.

Zambia gari ya Serikali ni Prado. Kenya gari ya Serikali ni vokswagen ni *four wheel drive* na gari ya kawaida tu. Sasa hii VX kila mtu awe ni Mkurugenzi VX, awe ni nani VX, naomba Serikali iliangalie sana hili ili kusaidia kupunguza matumizi ya Serikali, kwa sababu tofauti kati ya VX ni milioni mia mbili na *standard* ya milioni 140 ni milioni 60; hiyo inaweza ikaleta zahanati ngapi na ikajenga madarasa mangapi kwa wananchi wetu na wanafunzi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Victor Mwambalaswa. Kabla sijamwita mchangiaji anayefuata, nirekebishe kidogo tangazo la Mheshimiwa Suzan Lyimo ili kuliweka vizuri zaidi maana lilikuwa limekosewa kwenye maandishi hapa. Mgeni wake Ndugu Godwin Ngowi, ambaye ni Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha *Statistic* ni mume wake Mheshimiwa Suzan Lyimo; ninamwomba asimame, karibu sana Dodoma. *(Makofi*)

Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema baada ya kufanyiwa operesheni ya koo na hivyo sauti yangu kidogo imekuwa mbaya kama wajukuu zangu Wasukuma na Wanyamwezi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumpongeza Waziri Mkuu, kwa juhudi zake alizozifanya kuuweka Mkoa wa Lindi kuwa Manispaa. Nilikuwa najaribu kupiga kelele muda mrefu kuomba Mkoa wa Lindi nao upate heshima ya kuwa Manispaa na kutoka Wilaya ya Lindi mpaka Manispaa; hivyo namshukuru Waziri Mkuu kwa kuifanya Wilaya ya Lindi kuwa Manispaa na sasa hivi heshima itapatikana. Ninamhakikishia Waziri Mkuu kwamba, tutaheshimu na kuhakikisha Mkoa wa Lindi wanatumia kikamilifu fursa hiyo waliyoipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutufungulia na kutuzindulia Barabara ya Ndundu na Mingoyo, sasa hivi kipande cha Ndundu mpaka Marendegu ameshakizindua. Pia ninashukuru kwamba, barabara inaendelea na hivyo Wananchi wa Lindi na Mkoa wa Mtwara, watapata fursa ya kuitumia barabara kikamilifu na kuleta maendeleo na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Rais amezindua Daraja la Umoja, ambalo litaleta maendeleo na uunganishi na mawasiliano kati ya Tanzania na Mozambique. Daraja hili siyo kwa ajili ya Tanzania na Mozambique tu, barabara hii itakuwa na fursa kubwa sana kuanzia Afrika Kusini mpaka Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa muda mrefu ni mikoa ambayo imeonekana iko nyuma kimaendeleo, sababu kubwa ilikuwa kutokuwepo kwa miundombinu. Kutokana na fursa hii tuliyoipata ya uzinduzi wa Daraja la Umoja na barabara yetu kupitika kwa lami, sasa hivi kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi na Masasi na Mtwara ni saa sita tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu mfanyakazi akiambiwa anakwenda Lindi, alikuwa anaona kama anakwenda kupewa adhabu, lakini sasa hivi wanakimbilia huko na ukiwaambia waondoke hawataki. Hawataki kwa sababu kubwa tano; *natural resources* zote za Tanzania zinapatikana Lindi; fursa za Utalii zinapatikana; fursa za Kilimo zinapatikana na fursa zote unazozitegemea za uvuvi zinapatikana. Sasa ni kitu gani kitawatia kigugumizi wananchi kwenda huko, haiwezekani.

Karibu kila mmoja anakimbilia Lindi anaomba ardhi, anaomba sehemu ya kufuga wanyama, anaomba kufanya shughuli zote za maendeleo lakini tuziangalie hizo fursa kwa uangalifu sana. Wataingia wababaishaji wengi ambao watataka ardhi kwa ajili ya kilimo lakini hawalimi ni fujo tupu. Tuwapeleke wawekezaji ambao watakuwa wana nia kweli ya kuwekeza na kufanya ukamilifu katika uendelezaji katika suala la kilimo, utalii na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisahau vile vile kwamba, Lindi tuna madini ya kutosha ya dhahabu, *gypsum, limestone* na kadhalika. Mimi nikiwa kule Lindi ninaona wanajipenyeza Wathailand, Wahindi, Wachina na watu mbalimbali kutoka nje, wanaingia kule kwa fujo kwa vile wanajua kwamba kule bado ni shamba la bibi. Naomba tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani kuhusu Barabara za Kitaifa ambazo sasa hivi tumezipata naingia katika Barabara zetu za Halmashauri. Barabara hizo kwa kweli sasa hivi ni mbaya; hazipitiki na zinaleta kero kwa wananchi. Nashukuru sana katika Hotuba ya Waziri Mkuu amezungumzia kwamba, wametenga fedha nyingi sana za barabara, hizo fedha za barabara ninawaomba watumishi katika Halmashaui zetu wawe waangalifu na waihurumie hii nchi, inashangaza pesa zinakwenda nyingi lakini barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata huzuni ninapokwenda kwenye vijiji kwa mfano cha Mipingu, ninauliza barabara hii katika miaka arobaini inakuwaje katika mazingira haya lakini vifungu vya pesa vipo. Ningeomba baadhi ya watendaji wahakikishe hizi barabara zinapitika, wasingoje mpaka Waziri Mkuu au Mheshimiwa Rais aende kule barabara hizo ndiyo zikimbiliwe na kuanza kuchongwa. Kwa kweli hizi barabara ziko katika hali ngumu, ingawa pesa zimetengwa nyingi lakini Mikoa ya Lindi bado naona fungu la pesa zinazopelekwa kule ni dogo ukilinganisha na zile zinazopelekwa mikoa mingine.

Naungana na Mheshimiwa Lwanji aliyezungumzia suala la kupeleka fungu dogo katika baadhi ya mikoa, inaleta maudhi kiasi fulani, kujiona sisi hatuhitaji maendeleo.

Haya mafungu ya maendeleo yalete uwiano na yaangalie Mikoa ambayo ipo nyuma ingozewe ili na wao wapate tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongezea katika suala la Kilimo, Mkoa wa Lindi tuna ardhi nzuri, yenye rutuba na ilikuwa haijatumika kwa muda mrefu, lakini sasa hivi nimesikitishwa pia nakubaliana na wenzangu hili suala la ununuzi wa pembejeo hasa matrekta ya *power tiller* imekuwa kama ni kuleta udororaji wa maendeleo. Kumejiingiza baadhi ya wafanyabiashara ambao wanaangalia Tanzania inalenga wapi katika Kilimo Kwanza, wameingilia katika suala la ununuzi wa *power tiller,* badala ya shilingi milioni nne sasa hivi wanawauzia kwa shilingi milioni kumi. Je, hawa wafanyabiashara ambao wanatuletea kudorora Tanzania wanachukuliwa hatua gani?

Tusifikirie kuzungumza tu kila siku lakini waangaliwe, kuwaacha hivi kila siku wanatuletea *sabotage,* kwa kweli inaleta masikitiko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na hawa wanajulikana kuwa kazi yao wakijua hapa pana *loophole* basi wao wanaingiza miguu yao na kufanya shughuli ile idorore. Tukifanya mchezo, Kilimo Kwanza kitakuwa hakina maendeleo kwa ajili ya watu wachache ambao wanavuruga masuala ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda vile vile kuongolea suala la uwekezaji. Hakuna mtu asiyependa uwekezaji; uwekezaji ni suala la maendeleo lakini kama hatutauangalia vizuri, Tanzania itakuwa ni shamba la bibi. Narudia tena, hatutaki Tanzania kuwa shamba la bibi la kuleta ajira ya watu wa nje ambao hawana vigezo na wakaja kufanya shughuli zao hapa. Leo ukiingia ndani ya ndege kama unatoka Dubai, wamejaa watu ambao wanajua Tanzania kuna *loophole* za kuingia na kufanya uwekezaji bila ya kuwa hata na senti tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie suala la uwekezaji kwa ukamilifu; wengi wanaokuja kuwekeza Tanzania siyo wawekezaji ni wababaishaji. Wanakuja watu na *briefcase* hata senti tano hawana, lakini wanapewa mianya na baadhi ya viongozi na wataalamu kwamba fanya hivi, pita hapa, anawekeza akiwa hana hata senti tano. Baada ya muda yule mtu anaibuka kuwa tajiri mkubwa na kiburi kikubwa katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna watu wanawaficha watu kutoka Asia kama *cheap labour* katika majumba yao, wanafanya kazi. Zoezi la kuleta ajira Tanzania linakuwa dogo sana, badala ya kuhakikisha ajira inapatikana kwa Watanzania, inakuwa sasa hivi ni ajira ya Watu wa Asia na ukiangalia hata *Airport* wale watu hawana *passport* lakini wanapita. Kuna mianya mingi ambayo inaruhusu hawa watu kuingia Tanzania kuja kujionesha kama ni wawekezaji lakini siyo wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafika wapi kama Tanzania hatujihisi sisi wenyewe kwamba tunajikaanga wenyewe kwa mafuta yetu? Haiwezekani kumwona mgeni anathaminiwa kuliko Mtanzania; Mtanzania ana haki ya kupata haki yake na kuhakikisha

anafanikiwa.  Leo nchi ndogo kama Botswana, Sekta ya Utalii inamnufaisha Mbotswana, lakini Mtanzania hanufaiki na Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wababaishaji wameingiza miguu yao katika Sekta ya Utalii kulipa *concession fee* hawalipi, kulipia masuala madogo madogo kama ya maendeleo hawatoi.  Watatoa pesa kwa ajili ya ngoma za kienyeji na sehemu ambazo wanajua hazitamnufaisha Mtanzania.  Kama zile pesa zingepelekwa kwenye Sekta ya Kilimo, Afya na Elimu, nafikiri tungenuifaika.  Juhudi za makusudi wanazifanya ili kuhakikisha Tanzania haifanikiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kuzungumza, nilikuwa na haya tu ya kuchangia.  Ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, nami niweze kuchangia hoja iliyotolewa na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Iringa, kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  Pia nawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa katika kipindi chote hiki na ninawashukuru viongozi wote wa Mkoa wa Iringa, kwa ushirikiano mkubwa ambao mmeniwezesha kutekeleza majukumu ambayo nilikuwa nimepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri, lakini pia kwa utendaji mzuri wa kazi ambao ameuonesha katika kipindi kifupi alichopewa kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali.  Ameonesha uongozi uliotukuka na umahiri mkubwa, tunakupongeza sana, nina uhakika Wananchi wa Mpanda wanajivunia sana wewe kuwa mwakilishi wao na hawatafanya makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nimpongeze Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Celina Kombani, kwa kazi nzuri aliyoifanya na kutuwakilisha wanawake wote na kuonesha kwamba, wanawake wanaweza pale wanapopewa nafasi. Hii ni pamoja na wanawake wote waliopewa nafasi za uongozi. Nampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwanri, kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya na viongozi wote wa Wizara akiwemo katibu Mkuu, Mama Tarish, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nitakuwa sina fadhila kama sitampongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Iringa, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini, kwa kuuongoza vizuri Mkoa wetu na kuweza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Pia nampongeza Mama Getrude Mpaka, Katibu Tawala wa Mkoa wetu, kwa kazi nzuri akishirikiana na Viongozi wote wa Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nianze moja kwa moja kwenye suala la Kilimo Kwanza. Naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuweza kuhimiza mageuzi ya kilimo na mageuzi haya ndiyo yanayoweza kutuondoa kwenye

umaskini. Mageuzi haya yatawezekana pale ambapo wataalam wa ugani, huduma za ugani zitaboreshwa na kuwawekea mazingira mazuri, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kupata nyumba, vyombo vya usafiri na kupunguza matatizo waliyonayo, tukizingatia kwamba wanafanya kazi katika mazingira magumu na hasa sehemu za vijijini.

Kwa hiyo, tukiboresha haya pia tutakuwa tumeboresha Kilimo Kwanza kwa kuangalia wataalam. Juhudi kubwa zinazofanywa za Serikali kuweza kutenga Mikoa ambayo itakuwa ndiyo kama kitovu cha kuzalisha chakula, zinahitaji kupongezwa. Kwa kweli tunajivunia na sasa hivi tumeanza kuona kilimo kinaendelezwa, kilimo kilikuwa kimesahaulika.  Tunaipongeza sana Awamu ya Nne katika utekelezaji huu ambao unaendelea kwa sasa.

Pamoja na kuhimiza ununuzi au uboreshaji wa zana za kilimo, ikiwa ni pamoja na kununua matrekta madogo kama *power tiller*, naomba nitoe ushauri kwamba, haya matrekta yaendelee kufika kwenye ngazi za chini ikiwemo na kwenye vikundi vya wanawake ili waondokane na jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa huduma nzuri iliyofanya kwa kuweza kuwapatia Wananchi wa Mkoa wa Iringa *Voucher* za Pembejeo na wananchi wameitikia vizuri, wameboresha kilimo.  Hili ni suala la kujivunia,i ambaye anapinga kwamba maendeleo hayajaonekana huyu ana ajenda yake nyingine. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa kwa asilimia kubwa na lazima wananchi tujivunie mafanikio yetu sisi wenyewe. Tunapokuwa tunafanya maendeleo ya wananchi wote tuwe kitu kimoja.

Nina uhakika wananchi wana macho wanaona, wanalinganisha kabla ya Awamu ya Nne kuingia tulikuwa wapi na sasa tuko wapi. Kwa hiyo, tujivunie mafanikio ambayo tunayo.  Kwenye *voucher* wananchi wamelima na wameona mabadiliko makubwa. Ila napenda kutoa ushauri kwamba, *voucher* ziendelee kutolewa mapema hasa kwenye Wilaya kama ya Makete, ambayo inaanza maandalizi ya kilimo kuanzia mwezi Julai. Pia ziongezwe katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la elimu. Naipongeza Awamu ya Nne chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuhakikisha kwamba, watoto wengi wanapata elimu. Sote tunatoka vijijini; hebu angalieni kama kusingekuwa na Sekondari za Kata watoto wetu wangekuwa wapi sasa hivi na hasa watoto wa kike? Sasa hivi watoto wengi wako shuleni na haya mafanikio ni ya kujivunia. Wote wamepata elimu, muda wa miaka michache ijayo watoto wote walioko vijijini, kiwango cha chini kitakuwa kidato cha nne; hiyo ni hatua kubwa sana.

Watoto wengi pia wameweza kujiunga na elimu ya juu na tunapongeza uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ambacho Mwenyekiti wewe pia ni mmoja wa Wajumbe wa Bodi ambapo sasa hivi kama ulivyosema, mwaka huu jumla ya wanafunzi 10,000 watasajiliwa; ni hatua kubwa sana. Kama isingekuwa imefanyika hatua hii, hawa watoto wangekuwa wapi?

Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa uamuzi alioufanya wa kuanzisha Chuo Kikuu na Chuo cha Mfano. Pongezi kubwa kwa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Benki ya Wanawake. Napongeza sana kwa kuanzishwa Benki hii ya Wanawake na Benki ya kwanza ambayo inahudumia wanawake, lakini pia na wanaume. Sasa Benki hii imeanza vizuri na ni hatua nzuri sana. Nilikuwa napenda nitoe ushauri ili wanawake wengi waweze kufikiwa, wakiwemo wanawake wa vijijini. Benki hii inatakiwa ianze kuwa na matawi Mikoani. Kama haitakuwa na matawi moja kwa moja Mikoani, basi iende kwa hatua ianze kuwa na matawi kwenye kanda ili tuhakikishe kwamba huduma zinasogea karibu na wanawake ambao wako vijijini, ambao wengi wao hawapati fursa za kuweza kupata mikopo katika taasisi za fedha zilizopo.

Pia elimu ianze kutolewa ili wanawake waweze kuelewa ni njia gani ambazo wanaweza kutumia kujiunga na benki hii na nina uhakika kwamba, vyama vya kuweka na kukopa vya wanawake vitaweza kuhamasishwa ili viweze kupata mikopo kupitia benki hii na kama ikiwezekana, ziwepo huduma zinazokwenda vijijini hata kama benki haijapanuka basi wananchi hasa wanawake waweze kuelewa na wanawake wa vijijini wafikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la UKIMWI. Naipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo imekuwa inafanywa katika kupambana na tatizo kubwa la UKIMWI ambalo linaikabili nchi yetu. Kama tunavyoelewa, kila mwaka fedha za Mapambano Dhidi ya UKIMWI zimeendelea kupungua.

Ninaomba Serikali ishughulikie kwa haraka iwezekanavyo suala la kuanzisha Mfuko wa Mapambano Dhidi ya UKIMWI kama ilivyoainisha katika Sera ya UKIMWI. Mfuko huu unaweza kutusaidia kutatua matatizo mengine pindi ambapo fedha za wafadhili zinaendelea kupungua. La sivyo, tutajikuta kwamba huduma zitakuja kupungua na tukizingatia kwamba tuna wananchi ambao wanatumia dawa na watatumia dawa katika muda wa maisha yao yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nichukue fursa hii, kwanza kabisa, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uhai, umri na hatimaye leo kuwa hapa katika kuchangia hotuba hii nzuri iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu pamoja na Mawaziri wanaomsaidia TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, baada ya kumshukuru Mola, naomba niwashukuru na Viongozi wangu wa Chama cha Mapinduzi, Wilaya ya Mafia, chini ya Mwenyekiti wake Mzee Ali Faki Myeka na Katibu, Bwana Salehe, aliyekuwepo pamoja

na Wajumbe wote wa Kamati ya Siasa na Wanachama wote walioko kule Wilaya ya Mafia, kwa imani yao waliyonipa katika kuwakilisha Bunge hili kuwa mwakilishi wao katika Wilaya ya Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii pia kuwashukuru Viongozi wote wa Kiserikali, tukianzia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Hajati Amina yuko pale; Mheshimiwa *DC* wangu, Bwana Mangochie; Mkurugenzi, Bwana Shimwela; na Watalaam wetu wote wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, kwa ushirikiano mzuri walionipa katika kutekeleza yale yote ambayo nimeweza kujaliwa kwa kushirikiana nao katika Wilaya yetu katika kuhakikisha kwamba, wananchi wanaondokana au kupungukiwa na matatizo yaliyokuwepo pale Wilayani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana na kuyashukuru Mashirika yote yaliyoweza kunisaidia mimi katika kutekeleza yale yote niliyoyafanya kama vile *Mafia Island Development Foundation (MIDEF),* chini ya Mwenyekiti wake Mzee Ali Mwatanda. Naishukuru *NGO* moja kutoka Marekani inayoitwa CHARA, chini ya Mwenyekiti Mama Caroline MacDonald na mumewe Bwana Ron MacDonald. Ninaishukuru *ICAP* kwa kutusaidia sana katika shughuli za kuhakikisha inakarabati hospitali yetu na kutusaidia mambo mengi hata kutupa gari la kutusaidia katika shughuli zetu za kiafya pale Wilayani Mafia.

Naendelea kuwashukuru Shirika la *Islamic Help* la Uingereza, limeweza kutusaidia visima virefu 70 ambavyo sasa hivi vinaendelea kuchimba na tulishachimba 17 bado vingine vinaendelea. Tunategemea mpaka dakika hii hata kile kiwango cha Kiserikali cha asilimia 66 ifikapo mwaka 2010 Wilayani kwetu pamoja na washirikisha wenzangu, tulishafikisha zaidi ya asilimia 77.

Hiyo ni juhudi kubwa ambayo imetokana na msaada wanaotupa hawa ndugu zetu wa *Islamic Help*. Vilevile ninayashukuru mashirika yote yaliyotusaidia katika kuhakikisha kwamba, matatizo yanapungua Mafia na mengine na kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naomba nimshukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kwa imani yenu mliyonionesha ya kuniwezesha kuwa Kamishna wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Juhudi zangu binafsi na washirika wangu, mmeweza kuziona jinsi Bunge letu lilivyoboreshwa na kuhakikisha maslahi yenu na ya watumishi yanakuwa mazuri. Yote ni juhudi zetu na mimi nikiwa mmojawapo kama Kamishna wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba niwashukuru familia yangu kama wenzangu wanavyofanya; namshukuru sana mke wangu Bi. Samira, ambaye yupo hapa Dodoma na kila siku anakuwepo. Siwezi kumsahau pia na Bi. Naila, ambaye yuko Mafia, ambaye pia na yeye yupo huko katika shughuli za kuisaidia jamii hii ya Wananchi wangu wa Mafia katika kufanya shughuli hizo. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba pia unipelekee salamu kwa Katibu wa Bunge na Watumishi wote wa Bunge, maana inawezekana tusipate muda wa kuwashukuru. Naomba niwashukuru sana kwa ushirikiano walionipa; Katibu Mkuu, Makatibu wote na Watumishi wote wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru Wananchi wote wa Wilaya ya Mafia, kwa imani yao; walionipa kura za ndiyo na hata za hapana. Naamini wale waliotoa za hapana walikuwa wanajaribu. Mambo yaliyofanyika Awamu ya Nne anajua Mungu mwenyewe jinsi tulivyofanya. Hata mmoja wa Viongozi, Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC,* Mheshimiwa Dr. Slaa, alipotembelea alibaini kazi nzuri tuliyoifanya na yeye mwenyewe ali-*appreciate* yale tuliyoyafanya katika Wilaya ya Mafia.

Kwa hiyo, naamini Wananchi wa Mafia wanaelewa yale yote ambayo yamefanywa na pia hawatababaika na hawa *mavuvuzela.* Jana Afrika Kusini walipiga sana matarumbeta lakini bahati haikuwa yetu au yao. Tunaamini kwamba, yale ambayo tunategemea nchi nyingine za Afrika zitatuwakilisha, kwa kuwa mechi bado zinaendelea basi na wao Mungu atawasaidia. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya mengi katika kuhakikisha kwamba, jamii hii tunaisaidia upande wa afya, maji, elimu, ajira, uwezeshaji kwa maana vijana na akina mama, miundombinu, kila mtu anafahamu nini kimefanyika. Sasa yote haya baada ya kushukuru kwa sababu bila kushukuru sisi kuna hadithi inasema *"Malamyashukurunas laa yashukurullah";* asiyeweza kumshukuru binadamu mwenzake hata Mungu hawezi kumshukuru. Kwa hiyo, nasema kwa niaba ya Wananchi wa Mafia, nakushukuru na kuishukuru Serikali chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri waliyoifanya na Wizara zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilikuwa nataka kuzungumzia suala nyeti la uvuvi ambalo linatugusa katika Wilaya yetu. Kama tunavyofahamu, asilimia 70 ya Wananchi wa Mafia ni Wavuvi. Mimi mwenyewe niko katika Kamati ile inayoshughulikia masuala ya uvuvi; lakini kila ukiangalia mipango ambayo inapangwa na Serikali ni kamata, nyang'anya, piga, choma moto kitu gani. Sasa hili linatupa mtihani.

Kwa kuwa nia yetu ni kulinda mazingira, tunaiomba sana Serikali na tumeshauri kwenye Kamati na tutazidi kushauri kwamba, sasa hivi ifanyike Programu Maalum ya kuhakikisha kwamba, wavuvi wote si wa Mafia tu, kuanzia Tanga mpaka Mtwara pamoja na Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na Mito yote na Mabwawa, tusaidiwe kupata nyavu kwa bei nafuu.

Serikali kupitia mipango yake kama *MANCEP* na mingine, ihakikishe inasaidia iwepo Programu Maalum kwa sababu sasa hivi ukienda dukani nyavu, mashine na vifaa vyote ni ghali. Sasa uwepo utaratibu maalumu wa kuhakikisha kwamba, inawasaidia wavuvi ili waweze kupata nyenzo hii kwa bei nafuu. Tunasema zinakuwa ghali kwa

sababu juzi tulilalamika kwamba, Bajeti Kuu ya Mheshimiwa Mkulo haikutamka kwamba, zana za uvuvi zimesamehewa, kumbe zana za uvuvi zilikuwa zimesamehewa. Binadamu husahau kwamba, inatakiwa itamkwe kama ilivyotamkwa matrekta na vifaa vingine vya kilimo na vifaa vya uvuvi kwamba vimesamehewa ili jamii iweze kufahamu. *(Makofi*)

Leo mashine ya uvuvi ya *power* 30 inauzwa shilingi milioni nne mpaka tano; kuna sababu gani. Watu wa matrekta wamesema trekta mpaka likifika Dar es Salaam shilingi milioni tatu au nne; kwa nini liuzwe kwa shilingi milioni kumi? Faida hii haramu anayoipata yule kwa nini Serikali inakaa kimya? Sasa tunaomba sana kwamba, pakiwa wazi watu wataweza kufahamu bei ya vifaa hivi na wataweza kumudu kununua. Kwa sababu ikiwa ndogo hata haya mashirika au taasisi kama *MANCEP* inapokwenda kuchukua badala ya kununua mashine 10 kwa msamaha ule basi na wao watapata 15. Kwa hiyo, jamii itazidi kufaidika katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi zaidi ya kutoa shukrani tena kwa Wananchi wangu wa Mafia. Mimi nipo, nina afya nzuri, kichwa timamu na nitahakikisha kwamba, jamii yote ya Mafia inapata maendeleo.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninamshukuru kwa dhati kabisa kwa kuupa hadhi Mji wa Nzega kuwa Halmashauri ya Mji. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naamini maendeleo ya wananchi yatakuwa yamesogea karibu na naamini kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi itakimbia zaidi. Napenda kuomba kwamba, hatimaye baadae Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ndala pamoja na Mji Mdogo wa Nata. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Watumishi wako wote, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa jinsi ambavyo muda wote nilikuwa nalilia kupata Halmashauri ya Mji wa Nzega. Ninakuahidi ukija Nzega utapata *mchele wa tule na bwana*. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu haukuwa mzuri sana kwenye suala la kilimo hasa mazao ya chakula. Wananchi wa Nzega wamenituma; kwanza, pamoja na kuomba msaada wa chakula ni kweli lakini wameomba utaratibu wa mbolea ya ruzuku isiwe mbolea ya ruzuku katika baadhi ya maeneo tu. Utaratibu wa mbolea ya ruzuku pamoja na pembejeo kwa maana ya mbegu na vitu vingine, iweze kutandaa hata Wananchi wa Wilaya ya Nzega waweze kupata ruzuku ya mbolea. Wakaniamba wakati ulipokuja kwenye ziara uliahidi kwamba, ruzuku ya mbolea itakuwa hata kwa wakulima wote wa mahindi. Kwa hiyo, wamenikumbusha utekeleze ahadi yako ambayo ulikuwa umeahidi wakati wa ziara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wameniambia kwamba, nikumbushe suala la kilimo cha umwagiliaji. Yapo mabonde mazuri sana katika maeneo yetu; mfano, Bonde la Mto Manonga ambalo linaweza kufaidisha maeneo ya Kata za Nata, Lusu, Nzega

Ndogo na Wela. Yapo pia mabonde mengine mazuri tu, kwa mfano, Nkiniziwa kule Budushi; nashukuru Serikali imechimba bwawa kubwa sana kwa ajili ya mifugo na umwagiliaji.

Ningeomba maeneo mengine yaweze kuongezeka kama kule Milambo, Itobo, Magengati na Puge, kwa ajili ya umwagiliaji ili wananchi waondokane na njaa ya mara kwa mara ambayo mara nyingi inawasumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la manufaa ambayo wangeweza kupata hasa kwenye mazao ya mifugo ambayo inauzwa kule kwetu bado wanauza kwenye minada ya kizamani. Napendekeza minada hiyo ibadilishwe na pia ukamilishaji wa kiwanda cha nyama pale Shinyanga uharakishwe ili mifugo hiyo iweze kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Jimbo la Nzega wanaishukuru sana kwa Serikali kwa kupata mkandarasi wa kupeleka umeme Ndala. Tayari hadi naondoka mkandarasi alikuwa ameshafika *site* na wameniomba nimkumbushe Waziri pamoja na shukrani hizo kwamba, wangetamani sana tarehe 9 mwezi Desemba, Siku ya Uhuru, umeme uwe umeshawaka pale Ndala waweze kufurahia matunda ya uhuru wao.

Kwa hiyo, ningependa kutuma salamu hizo za wananchi, wanaomba umeme huo ufike Ndala kwa sababu tayari mkandarasi yupo ni kiasi tu cha kusukumwa ili utekelezaji ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi pia wanashukuru sana na sasa nasema wananchi wa Mkoa wa Tabora wanaishukuru sana Serikali kwa kuzitangaza barabara za Mkoa wa Tabora, barabara ya kutoka Tabora kwenda Manyoni, barabara ya kutoka Tabora kwenda Urambo na barabara ya kutoka Tabora kwenda Nzega. Tabora ni mji ambao ni mkongwe, mji wa zamani sana, mji ambao bila barabara hauendelei kabisa na wananchi wanaomba pamoja na kutangazwa huko kwa barabara hizo, ni lini Mkandarasi ataingia kwenye *site?* Wangependa kabla ya bajeti ya Waziri wa Miundombinu wawe wameweka saini mkataba wa mkandarasi ili wakandarasi hao mpaka mwezi wa Kumi wawe *site* ili wananchi wa Mkoa wa Tabora waweze kufunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani Mkoa wa Tabora ukifunguliwa kwa barabara kutoka Mkoa wa Kigoma kuja Tabora mpaka Manyoni kwa maana ya barabara kutoka Nzega kuja Tabora, Tabora kwenda Sikonge, Sikonge- Ipole, Ipole – Mpanda kwa maana ya Tabora – Ipole, Ipole –Mbeya, Tabora tunaifanya kama *hub* ya Mikoa ile ya Magharibi. Mikoa ile ya Magharibi ina uwezo mkubwa sana ya kiuzalishaji, ina uwezo mkubwa sana kiuchumi.

Kwa hiyo, kwa kukosekana barabara katika Mkoa wa Tabora inamaanisha Tabora tunaufanya uwe mji ambao umezubaa na hauendi vizuri kwenye maendeleo kama Mikoa mingine ilivyo. Hivyo kupitia kwako namwomba sana Waziri Mkuu suala hili la barabara la Mkoa wa Tabora sasa hivi imekuwa ni kero, kila bajeti Wabunge wa Mkoa wa Tabora tunasimama kusemea juu ya barabara zetu za Mkoa wa Tabora. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ifikie tamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru imetangazwa vizuri, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba mchakato wa kuwapata wakandarasi uharakishwe ili waweze kuingia *site* mara moja, isije tena kusema kutokana na ufinyu wa bajeti, kutokana na sababu zisizozuilika, hatutaelewa na unatujua sisi Wabunge wa Mkoa wa Tabora ni wapole sana sana lakini ukituchokoza hatutakaa vizuri. Naomba kabla Waziri wa Miundombinu hajasema awe ameshaweka mkataba na wakandarasi. Sababu zingine zozote kwa kweli hatutazivumilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo juu ya suala la Kitaifa hasa suala la reli na hata suala la shirika la ndege. Mashirika haya makubwa ya usafirishaji katika kipindi hiki chote yamezorotesha sana huduma zake mpaka sasa hivi kumekuwa na sababu za kucheleweshа uanzishaji wa usafiri wa reli ambao unategemewa sana na Mikoa ya Magharibi, Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Tabora na hata Sumbawanga wanategemea sana usafiri wa treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Shirika la Ndege la Taifa ambalo kwa kweli nalo limezorota sana kwa muda huu uliopita nalo linazidi kupata sababu tu sasa hivi *Boeing* nayo haifanyi kazi na Serikali bado haijatamka namna gani na ni lini mashirika haya yatakuja kufufuliwa. Hii ni hasara kwa Taifa lenyewe lakini vile vile ni hasara hata kwa uchumi. Shirika la reli lilikuwa linafanya usafirishaji mzuri sana hasa kwenye Kanda ya Maziwa Makuu na kupatia nchi yetu pesa kwa uchumi lakini kwa muda mrefu sasa hivi imekuwa baada ya kuingia kwa mkataba na mwekezaji limekuwa ni shirika ambalo linazorotesha sana mambo hayo ya uchumi na usafirishaji. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kusema anafanya nini juu ya Shirika la Reli pamoja na Shirika la Ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuwaomba Wabunge wenzangu, namshukuru Mungu nimekuwa Mbunge mara ya tatu, nitarudi tena *Inshallah*, lakini CCM ilitoa wazo la kuwapa watu fursa ya kutangaza nia, bahati mbaya sasa waliokuja kutangaza nia wameonyesha nia, badala ya kutangaza tu wameanza kuonesha nia. Nawaomba Wabunge wenzangu tulieni, fanyeni kazi, hizi zihesabuni tu kama kelele za mavuvuzela, mavuvuzela yana kelele kweli, yanaweza yakakubabaisha ukaacha kufanya kazi za wananchi, ukaacha kufanya kazi zako za Kibunge, ukabaki kupiga kelele na wewe kama wao.

Wewe tulia, Mwenyezi Mungu anajua, kazi ulizofanya wananchi wanajua, utarudi tu. Wabunge wenzangu mara nyingi wengi wanababaika, lakini lazima theluthi moja itoke na theluthi moja inapotoka itokane humu humu na nawaombea dua wenzetu waliokaa pale mbele ndio watoke wao, warudi wana CCM wote na mimi nawaambia hakuna masika yasiyokuwa na mbu, mbu ndio hao. Kwa hiyo, kelele za mlango zisikufanye usilale, tupambane tutashinda.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini vile vile hawa ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi wanasifia sana utekelezaji wa Ilani yao, sasa kwa mtazamo wangu, naona kwamba inabidi waseme kwa sababu wasiposema wao nani atakayesema na naamini kabisa maneno wanayoyasema yanatoka mdomoni, hayatoki moyoni. Kama yanatoka moyoni ama hawaijui Ilani yao au hawaisomi Ilani yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo, kwa sababu kwa kuwa mjadala wetu unakwenda kiilani ilani na kwa kuwa ilani ambayo tunaambiwa inatuongoza ni ya CCM lazima na sisi tujadili Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Lakini vile vile napenda niwaambie ndugu zangu, ilani sio sera, ilani kama umesema ni miaka mitano unatakiwa ndani ya kipindi cha miaka mitano uwe umetekeleza, kama haujatekeleza inabidi urudi kwa wananchi uwaambie nimetekeleza haya machache, naomba radhi haya nimeshindwa. Kwa hiyo, tusitake kupotosha kwa watu kwamba hii ni sera, hapana, hii ni ilani ya miaka mitano, mliomba kura, mkashinda kwa kishindo kama mnavyosema, sasa mje mtueleze mmetekeleza vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikia mnaandika nyingine, itabidi mtumie hii hii kwa sababu hii haijakwisha. Nianze kwa machache kwa sababu nikisema kwamba niangalie yote haya hata dakika ishirini hazitatosha. Nikiangalia kwenye kilimo ukurasa wa ishirini na tatu, Ilani ya CCM inasema ikifika 2010 kilimo kitakuwa kwa asilimia 20. Leo hii ni 2010, kilimo kinakuwa kwa asilimia tatu. Miaka miwili iliyopita kilimo kilikuwa kinakuwa kwa asilimia 4.5, kwa hiyo, nyie jinsi mnavyoendelea kutawala na kuleta ajenda za kilimo ndivyo ambavyo kilimo kina-*fail*.

Wananchi wana haki ya kujua haya na mambo ya kutuambia kwamba kuna ajenda ya kilimo kwanza, wakati ukiangalia bajeti ya maendeleo zimetengwa bilioni 103 tu kwenye shughuli za maendeleo. Sasa kama tunatenga shilingi bilioni 103 kwenye shughuli za maendeleo, kibaya zaidi inatoka shilingi bilioni tatu tu, bilioni mia moja zote tunategemea wafadhili. Mfadhili akiamua asilete, maanake wananchi wetu maskini huku maisha yao hayasogei. Lazima tuwe wakweli, tuache unafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye suala la utalii, walisema kabisa kwamba watahakikisha wanalifufua Shirika la Ndege ili tuwe na *national flag*. Wakati awamu hii ya nne inaingia madarakani tulikuwa tuna ndege nne, sasa hivi tuna ndege moja, shirika liko kwenye hali mbovu (*ICU)*, kuliko ambavyo ilikuwa zamani. Tuliambiwa kwamba Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuendeleza ubinafsishaji na ukodishaji wa viwanda vya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya *CAG* inaonesha kwamba mpaka sasa hivi mashirika ya umma pamoja na viwanda 366 vimebinafsishwa. Mwaka jana *CAG* alifanya *special audit* ya mashirika ambayo yamebinafsishwa. Katika yale makampuni 60 ambayo ni *sampling* nzuri sana katika haya makampuni 366 ni makampuni 12 yanayofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo inatuambia nini? Hiyo inatuambia kwamba sera ya ubinafsishaji imefeli. Lazima turudi kwa wananchi tuwaambie jamani tumeshindwa, tutafutieni misaada mingine au wapeni Kambi ya Upinzani, kwa sababu kwa miaka nenda rudi tumekuwa tukiwapa mawazo mbadala, mengine mnayaiga kama *UDOM*,mengi mnashindwa kuyafanyia kazi kwa sababu ya mawazo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhusiana na *UDOM*, ile bilioni 800 Serikali mliyoichukua, mwende mkaingie mikataba na haya mashirika, mmetumia ubabe wenu, mmevuta zile pesa hakuna maandishi yoyote yanayoonesha makubaliano baina yenu na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Jamani hii Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni madundulizo ya hawa Watanzania maskini. Sasa tusije tukafikia hatua mifuko yetu ikafilisika, wazee wetu wakastaafu, wakakosa fedha za kulipwa. Wamesifia sana kwamba ndani ya miaka mitano mambo yamekuwa mazuri, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye masuala ya elimu, maana elimu hii ndio kila mtu akisimama anazungumzia madarasa, lakini ni lazima mjue kwamba haya madarasa yalijengwa kwa ushirikiano na wananchi. Mje hapa mtuambie asilimia ngapi ambayo wananchi wamechangia na Serikali kwa kukusanya kodi mmechangia ngapi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, taratibu kidogo. Unaweza kuendelea. (*Kicheko*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, itabidi hiyo dakika moja uifidie. Miaka mitano iliyopita, sijui minne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete aliahidi kwamba angehakikisha kila Wilaya ndani ya Ilani ya miaka mitano ya Chama cha Mapinduzi inajengewa chuo cha ufundi. Sasa leo mniambie kwenye Wilaya zenu vyuo vya ufundi vingapi vimejengwa, hakuna. Mkakati wa MMEM ambayo ndio sehemu ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ilisema ingejenga nyumba za walimu 22,000, leo hii zimejengwa 400. Mnatakiwa mrudi kwa wananchi muwaambie tumeshindwa, tusitumie maneno ya kinafiki hapa kuji-*please* kwamba tumetekeleza ilani wakati hata ilani yenu hamuisomi na hamuijui. Tuache unafiki sisi ni wanasiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la *gender* ili nije kwenye ajenda nyingine. Ilani ya CCM inasema kwamba itahakikisha maisha ya mwanamke yanaboreka. Sasa hivi tunavyozungumza kuna tofauti kubwa ya kipato baina ya mwanamke na mwanaume kuliko ambavyo imewahi kutokea. Mwaka 2006 wakati mmepewa mamlaka kwa kishindo na *synovate* nasikia inaendelea kuwafagilia, najua mtashindwa kwa jina la Mungu. Nafasi ya Tanzania kwa tofauti ya kipato baina ya mwanamke na mwanaume, mwaka 2006 ilikuwa ya 26 kati ya nchi 134 zilizofanyiwa

utafiti. Utafiti wa mwaka 2009 unaonesha kwamba Tanzania imeporomoka kutoka nafasi ya 26 mpaka nafasi ya 73 katika tofauti ya kipato baina ya mwanamke na mwanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaambiwa Serikali ya Awamu ya Nne imeboresha, hatuzungumzi maboresho ya kutuongezea Viti Maalum, hatuzumgumzi maboresho ya kuongeza Majaji, hapana. Sisi tunachotaka ni yule mwanamke maskini kule chini aboreke na haya mambo yanawezekana kama tukitumia rasilimali zetu vizuri. *CAG* amekuwa akilalamika kila mwaka kwamba, kuna uvujaji mkubwa wa fedha. Fedha za Umma hazitumiwi vizuri, Serikali haichukui hatua, tunakaa tu tunapitisha bajeti, mwaka umepita trilioni moja imekwenda chini, haijulikani ilipokwenda. Taarifa ya *CAG* ya mwaka jana inaonesha kwamba kuna masuala yenye thamani yakaribia shilingi trilioni 155 hayajashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Mimi hii ndio Kamati yangu, tuko na Shoka na makubaliano yetu ni kuunga mkono. Mimi nimpongeze sana Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68, 67 hapana, 68 (7).

**MWENYEKITI:** Naomba uichukue Kanuni uisome mwenyewe.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Kanuni vipi na nilishasema hapo? Haya nifungulie haraka, haya lete. 68(7), hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka, ukae chini tu. hukuwa umejipanga vizuri kinachotakiwa ni utumie kanuni 68(1) kwa alichosema. Kwamba Mbunge anaweza kusimama wakati wowote na kusema kuhusu utaratibu. Sasa kwa kutokujua kwako Kanuni basi bahati mbaya tunaendelea. Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unilinde na dakika zangu. Kamati ya Sheria na Katiba tuna msimamo. Nimeunga mkono hoja lakini nimewapongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri Tawala za Mikoa na Serikali na wafanyakazi wote wa Ofisi hizo. Nipongeze na nishukuru viongozi wangu wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, *RC*, *DC* wangu dada yangu Chiku; *DAS*, Mama Mcha, kwa ushirikiano mzuri sana. Niseme kwamba tumefaulu, Chama chetu cha Mapinduzi

kimefaulu kwa kiasi kikubwa kutekeleza Ilani. Awamu ya Nne tumefaulu sana sana, lakini nikumbuke kwa ruhusa yako kuna nyimbo za zamani, kuna wimbo mmoja alikuwa anautumia sana Mzee wetu wa Dar es Salaam. Unasema, mtoto acha kupiga mayowe, waache watu waone wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeunga mkono lakini nakuja kwenye mchango wangu. Imeelezwa hapa kwa asilimia karibu 92, Chama cha Mapinduzi kimefanya vizuri, tumetoa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa nchi nzima. Huu ni ushahidi tosha kuonesha kwamba Chama cha Mapinduzi kinakubalika na kinatekeleza yale yanayotakiwa. Lakini nirudi hapo hapo niombe Serikali Kuu ijaribu kuangalia hawa Watendaji wetu wa Serikali za Mitaa kwenye masuala ya usafiri, masuala ya ofisi, masuala ya vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kule Temeke ninalo tatizo pale Kurasini, tuna mradi mkubwa tu mzuri wa kuimarisha Bandari yetu na kuhakikisha tunakuwa na sehemu kubwa kwa ajili ya masuala ya maendeleo. Sasa tatizo langu kubwa liko kwenye Mtaa wa Kiungani. Tathmini ilifanyika Aprili, 2008 malipo yalianza kulipwa Desemba 2008 lakini cha kusikitisha kulikuwa na makubaliano, wale wananchi walipwe na wapewe viwanja. Lakini hadi leo hawajapata viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaa wa Kurasini walifanyiwa tathmini 2009, lakini hadi leo hawajalipwa fidia zao. Mtaa wa Mivinjeni walifanyiwa tathmini 2008, mpaka leo hawajapatiwa viwanja ambavyo waliahidiwa. Kwa hiyo, naomba Serikali waliangalie hilo kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilwa Road, Barabara ya Kilwa, wananchi wale walikuwa na kesi 2004, kesi ile walishinda 2008, lakini hadi leo hawajalipwa fidia yao. Naomba Serikali waliangalie kwa makini. *Jet*, *Davis Corner*, Mwenyekiti niishukuru sana Serikali, barabara ile imeshaanza kujengwa na ilikuwa ni kero kubwa. Lakini bahati mbaya wasiokitakia Chama Cha Mapinduzi mema, nimeona juzi kwenye magazeti wanasema, Mbunge aliahidi atajenga barabara, barabara haijaanza. Lakini barabara ile imeshaanza na madaraja sasa yanajengwa na kampuni ya Nyanza kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe daraja la Kigamboni, tunajua taratibu zake zote zimeshakamilika, lakini wananchi wa Dar es Salaam wangependa kumsikia mkandarasi tu akitangazwa. Hilo ni ombi la wananchi wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Dar es Salaam. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kazungumzia, lakini naomba tulipe mkazo wa hali ya juu. Hali ya Dar es Salaam, msongamano ni mkubwa. Kwa hiyo tuhakikishe Serikali wanaongeza mapato kwenye barabara za Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za *National Housing*, tuna nyumba pale Keko, Chang'ombe na Tandika. Tulipitisha katika bajeti iliyopita, nyumba zile zianze kuuzwa

kwa wananchi kama *apartment.* Kwa hiyo, wananchi wanauliza utaratibu umekwama wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuwashukuru wananchi wa Temeke kwa kunipa imani kubwa ya kuwa Mbunge wao na katika miaka mitano sikuwaangusha. Nimetekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa asilimia 90. Nina uhakika asilimia 10 iliyobaki tutaimaliza kabla ya uchaguzi mkuu. Nawatakia kila la kheri wananchi wa Temeke nawahakikishia niko nao pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uvuvi, wenzangu wamesema. Lakini bora tukaangalia umuhimu wa kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapa mikopo ya kununua vitendea kazi imara vinavyohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo tatizo pale kijiji cha Wavuvi Kurasini. Ndugu zetu wa *TAZARA* waliuza maeneo pale. Nawashukuru ndugu zangu wa Temeke.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka, taarifa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 68(viii).

**MWENYEKITI:** Bado, endelea kukisoma, kisome tu, nakuruhusu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Vile vile Mbunge yoyote anaweza kusimama mahali pake na kusema taarifa na kwa ruhusa ya Spika, atatoa taarifa na ufafanuzi kwa Mbunge anayesema, ambapo Spika atamtaka Mbunge anayesema aketi kusikiliza taarifa hiyo.

**MWENYEKITI:** Nilishalifanyia maamuzi, lakini nakupa nafasi uzungumze.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi. Mheshimiwa Mtemvu ni Mbunge mwenzangu ambaye namheshimu sana lakini eo amenisemea uongo kuwa tumekubaliana kwamba tupitishe taarifa hii. Mie sijasema na aseme tulikokubaliana. Hatujakubaliana mahali popote. Kwa hivyo, afute usemi wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Alichosema Mheshimiwa Mtemvu ni kwamba yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria na Utawala na kwamba kwa kuwa wao ni Wajumbe wa Kamati hiyo wamepitia haya masuala ya Bajeti kupitia kwenye Kamati hiyo na Wajumbe hao mkakubaliana kuhusiana na yaliyomo humo baada ya kuyachambua na kuyajadili na Mwenyekiti wenu Mheshimiwa Lubeleje amekuja mbele ya Mbunge hapa na taarifa yenu na wewe ukiwepo na kuwataja majina ya Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwamba kazi mliyofanya katika Kamati ni hiyo. Kwa hiyo sijaelewa unamtaka Mheshimiwa Mtemvu sasa azungumze nini. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Sasa Mheshimiwa Mwenyikiti ikiwa ni maoni ya Kamati kwa nini anitaje mimi Mbunge peke yangu, ana ajenda gani. Hakusema Kamati kasema Mheshimiwa Shoka akiwemo.

**MWENYEKITI:** Sasa naamua, naamua kwamba tuendelee na shughuli za Bunge, naona tunapoteza muda tu hapa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Mtemvu kwa uliyoyazungumza na hasa uliposema kwamba mtoto acha kupiga mayowe, acha watu waje waone wenyewe. Naamini *message sent and delivered.* *(Makofi)*

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Misungwi. Kwanza kabisa, nichukue nafasi nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumpa asilimia 100 katika bajeti hii ambayo ameiandaa vizuri sana kwa ushirikiano wake yeye, Mawaziri pamoja na Wakuu wa Mikoa na timu yake yote kwa pamoja. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na suala ambalo limekuwa ni tatizo kubwa katika Jimbo la Misungwi. Tatizo hilo ni maji. Leo napenda nihitimishe kwa kusema kwamba kero hiyo ambayo ilikuwa ni tatizo kubwa sana katika Wilaya yetu ya Misungwi limeshapatiwa ufumbuzi na maji sasa hivi kutoka Nyahiti mpaka Misungwi kwenye tenki yameshafika. Tunachosubiri ni uzinduzi tu. Ninaposema hivyo nina maana kwamba, hiyo yote ni utekelezaji wa Ilani wa Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo ambayo yatakuwa yamebakia. Kuna kijiji cha Mwajombo, Igokelo, Iteja, Mwambola, kuna ng’ombe ambao wapo *package* moja. Sasa niombe tu kwa sababu kuna uhakika kabisa wa kwamba wananchi wa Misungwi hawana matatizo na tutarejea hapa kuja kuyakamilisha hayo, basi Serikali iendelee kuyaandaa katika mazingira ili tuweze kukamilisha hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu nirejee katika zao la pamba. Zao la pamba ni zao ambalo lina matatizo makubwa sana. Bei zake mara kwa mara huwa ziko chini. Niombe tu Serikali iliangalie hilo, itakapotangaza bei basi iendane na mtiririko ambao najaribu kuupendekeza hapa. Bei kwenye soko la dunia sasa hivi iko kati ya senti 74, 75, 76 mpaka 78. Nimepiga mahesabu yangu nimechezea kwenye senti 75 tu. Ukichukua ile *formula* ya kilo moja mara 2.20462 mara senti 75, unapata kwa kilo moja

unapata 1.6531850. Ukizidisha mara *exchange rate* ya 1,450 sijafika kwenye 1,500, unapata 2,397.118 na kuendelea.

Hizi ni sawa na kilo tatu za pamba ya kawaida. Kilo moja unaipata kutokana na kilo tatu za pamba mbegu. Kwa hiyo, ukigawanya kwa tatu hii 2,397.11, unakuta iko kwenye 799. Hapo hujaweka mbegu na masuala mengine. Niombe kabisa, Serikali basi mwananchi wetu huyu mkulima wa zao la pamba apewe bei ya shilingi 800 kwa kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishaitoa hiyo shilingi 800 bado kuna *VAT* ambayo inapashwa sasa ili angalau tuweze kumlinda huyu mfanyabiashara mwingine umtolee kwenye *transportation* ya marobota kutoka hapo kwenye jineri kwenda mpaka kwenye upakiaji pale bandarini. Hapa tayari utakuwa umeshajenga ile hoja kwamba mnunuzi naye hana matatizo na mwananchi wangu atakuwa ameshapata ile shilingi 800. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ilione hilo na fomati tumejaribu kukokotoa hapa wala hatukufika kwenye *exchange rate* ambayo ipo mpaka sasa hivi. Lakini kuna suala moja katika utaratibu wa ununuzi wa zao la pamba, kuna ile mizani ya *steel yard* ile ambayo tumekuwa tukiitumia kwa muda mrefu. Niombe sana basi iendelee kutumika hiyo, isiendelee kutumika hii ya saa. Katika mkutano wa wadau pale Mwanza walilalamikia sana suala hili. Lakini hakuna barua ambayo imetoka kwa ajili ya kufuta maelekezo hayo mengine ili tuweze kutumia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie elimu. Elimu ombi langu nadhani mmeshalifikisha kwa Waziri wa Elimu. Kuna shule moja ya Nyabumanda ambayo wameshakamilisha kila kitu na wanafunzi ambao wameegeshwa kwenye shule zingine. Hilo nina imani na Mheshimiwa Waziri atalifanyia kazi. Hilo sitaki nichukue muda mrefu, alifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara za Mkoa, nimpongeze Mkuu wa Mkoa ambaye yeye ndiye Mwenyekiti wa Bodi hiyo ya Mkoa wetu wa Mwanza, Abbas Kandoro anafanya kazi nzuri sana. Mgawanyo wa barabara za Mkoa hatuna matatizo na Wabunge wote wa Mkoa wa Mwanza. Anasimamia vizuri, barabara zitaanza kujengwa. Nina uhakika barabara kuanzia Mwanangwa, Misasi mpaka Salawi itaanza kujengwa katika kiwango cha changarawe cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo cha msingi, ombi tu kuanzia Buhingo kwenda Ihelele ni tatizo kubwa sana. Kwenye kikao cha mwisho cha Bodi ya Barabara tuliiomba ipandishwe hadhi. Hata katika kulelewa tu na Wizara au tuseme na *Tanroad* ya Mkoa ipate fungu. Tumeomba *special request* ya milioni 400 ili tuweze kuitengeneza kuanzia Buhingo mpaka Ihelele ili tuweze kufikisha madawa kwenye chanzo chetu cha maji ambayo yanakwenda mpaka Kahama na Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Halmashauri ni tatizo kubwa sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ile barabara ya Mondo mpaka Mwaniko bado ni tatizo kubwa sana katika eneo la Nguge. Nimwombe Mheshimiwa Kombani aliniahidi akanipa

milioni 60. Lakini katika bajeti alikuwa ameweka milioni 65 nyingine, hazikufika, wananchi wa Mondo wanateseka sana katika eneo la Nguge. Naomba tatizo hili litafutiwe ufumbuzi wa haraka sana ili wananchi hawa waweze kutoka katika tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la ardhi katika Wilaya yetu ya Misungwi lakini niseme kwamba hilo niliache kwa sababu Mkuu wa Wilaya analishughulikia kwa sababu kuna wananchi ambao wanalalamikia *compensation* wanayopewa ya shilingi laki nane kwa heka ni ndogo sana. Lakini kwa sababu ameshalichukua Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya na Timu yake inafanya kazi, tuliache kwanza halafu baadaye tulifanyie kazi katika utaratibu ambao Wilaya inafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze tu Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa kusikia kilio changu ambacho nilikileta hapa. Wananchi wa Misungwi kuhusu Chuo chao cha Misungwi walikuwa wanahitaji sana msaada wa kurudishiwa kile cheti ili kiweze kutolewa katika Chuo chao cha Misungwi. Mmelisikiliza hilo na mmeshatoa uamuzi na sasa hivi tuwakaribishe tu wananchi ili waje kusoma kwa *level* ya cheti na d*iploma* inapatikana kwenye chuo chetu cha Misungwi. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mifugo mwenzangu amelizungumzia. Lakini bei yake bado iko chini sana. Ufumbuzi wa tatizo hili ni kuwa na soko ndani ya nchi yetu. Tuna ujenzi wa machinjio ya kisasa pale Ruvu. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu tupia jicho katika kiwanda hicho ambacho kinajengwa. Mheshimiwa Rais alishaweka jiwe la msingi pale. Zinadaiwa kama bilioni tano ambazo ziko kwenye bajeti na kwa sababu bajeti tumekwishaipitisha, muanze kuona uwezekano sasa wa kuruhusu pesa hizo ili ujenzi uweze kuendelea ili wananchi baadaye waweze kuvuna mifugo yao na kuuza nyama nje ya nchi badala ya kufanya vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi maalum. Wilaya ya Misungwi ina matatizo ya nyumba za watumishi. Tumeshapeleka maombi maalum katika Serikali yetu, naomba myashughulikie, ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri milioni 500, nyumba 10 za watumishi milioni 500. Maji mjini baada ya kufika kwenye tenki la Misungwi ambalo ni dogo, tunaomba kama milioni 900 hivi ili baadaye tuanze ujenzi wa tenki kubwa na baadaye tutengeneze mtandao wa maji pale Misungwi, maana sasa hivi yanapoteremka yale maji yana kasi kubwa sana, kiasi kwamba mtandao uliokuwepo unapasuka. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iweze kutukumbuka kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia tu kwa kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Misungwi, wamenipa msaada mkubwa sana bila kuwasahau Waheshimiwa Madiwani wote na niendelee kumshukuru Mheshimiwa Celina Kombani kwa kuona matatizo yaliyokuwepo kwa wananchi wangu na kutupa Kata saba zingine. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa jirani

yangu Jenista Mhagama kwa msiba uliompata wa kufiwa na mume wake. Nina imani Mwenyezi Mungu atamtia imani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo naomba nichangie kuhusu masuala ya mimba ya watoto wa kike mashuleni. Katika nchi yetu tuna sheria moja tu ambayo inaweza ikawabana watoto kwenda shule ambayo ni Sheria Na. 25 ya mwaka 1978 inayomtaka mtoto aweze kwenda shule. Lakini hakuna Sheria inayoonyesha kwamba mtoto atakapopata mimba kuna utaratibu gani unaoweza kuchukuliwa. Lakini naomba kuelewa kwamba mtoto anapofikisha miaka 18 tayari tunasema ameshakuwa mkubwa. Kama amekuwa mkubwa ana maamuzi yake, anaweza akapata mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kuna utaratibu gani kuleta sheria ambayo itaweza kuwasaidia hawa watoto wa kike wa *primary* na *secondary* ili kuweza kuwalinda na hata atakapopata mimba akienda Mahakamani kuwe na Sheria maalum, sheria hiyo iweze kuwasimamia wasichana ili wasiweze kupata mimba. Yaani iwepo Sheria maalum ambayo itaweza kuelezea suala la mimba kwa watoto wa shule. Tofauti na sasa hivi ambapo watoto wanapopata mimba wale watu wanakamatwa lakini yule mtoto wa kike anaweza kusema nilikuwa na maamuzi ya kupata mimba. Tayari ana miaka 18, huna maamuzi ya kuweza kumchukulia hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la kilimo cha tumbaku. Naomba nitoe mawazo au nitoe malalamiko ya wakulima wa tumbaku. Wakulima wa tumbaku katika Kata ya Ufuruma, Wilaya ya Uyui wanatoa malalamiko yao kama ifuatavyo:- Katika kilimo cha tumbaku kwenye mche wa tumbaku, mche mmoja una matawi manane. Kama una matawi manane, lakini gredi ya kununua tumbaku na gredi ziko 65. Ukichukua gredi 65 ukigawanya kwa nane kwa maana kila tawi moja, lina gredi nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui na wao wanapokwenda kuuza hiyo tumbaku wanauza kwenye hizo gredi nane kwa kila tawi moja. Lakini inakuwa ni tatizo zaidi kwa sababu kama mche mmoja una matawi manane na kama una matawi manane huyu mkulima unamwambia unaigredi tumbaku yake kwenye gredi 65, kama utazigredi 65 maana yake huyu mkulima tayari umeshambana na wewe utakapokwenda kuuza ile tumbaku hutauza kwenye gredi zote hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, je, kuna utaratibu gani wa kuweza kuzigredi zile tumbaku ambazo wanauza kwenye gredi nane, pia kama ziko kwenye matawi yale ambayo yaliyokuwepo sawasawa katika mche ule. Kwa hiki ni kilio chao kikubwa cha wakulima wa tumbaku. Lakini la pili, kilio chao kikubwa mwanzo walikuwa hawajaelewa kuhusu masuala ya dola. Lakini sasa hivi wameweza kuuza tumbaku yao kwa dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wengi si wasomi kama tunavyoelewa. Anapokwenda kuuza tumbaku yake anaambiwa leo dola imepanda, kuanzia yule anayepeleka tumbaku yake asubuhi anaambiwa dola sasa hivi ni kiasi fulani, anayepeleka saa sita anaambiwa dola saa hizi imepanda. Kwa hiyo, bado wakulima kwa utaratibu huo

kuhusu suala la ununuzi wa dola wanahangaika na hawapendi wanajiona kuwa wanadhulumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia nyuma tayari wananunua pembejeo kwa dola, na huwa wanakopa, akishakopa siku ya kwenda kulipa anaambiwa leo dola imepanda. Kwa hiyo, akiambiwa dola imepanda tayari yule mkulima anajihisi kuwa ameweza kudhulumiwa kwa sababu utaratibu wa dola kupanda na kushuka wao hawauelewi vizuri. Kwa hiyo, nina imani suala hili litaweza kuchukuliwa ili kuweza kwasaidia wananchi hawa na hasa wakulima wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la afya. Mara mbili au mara tatu katika Bunge hili naongelea kuhusu afya ya akinamama. Akinamama hawa wanapokwenda kujifungua wanapata shida sana hasa inapokuwa ni usiku, hakuna taa wala nini, lakini yule mzazi anapokwenda kuzaa ni lazima aende na pesa ya mafuta ya taa kama shilingi 1,000 au shilingi 500. Lakini je, Serikali ina utaratibu gani wa kuweka *solar* katika zahanati zetu na vituo vya afya ambavyo viko vijijini? Ni vigumu zaidi kwa mwanamke anapojisikia uchungu wa kwenda kuzaa, bado akafikiria na pesa ya mafuta ya taa na vitu vingine. Kwa hiyo, ni namna gani mwanamke anavyoweza kupata shida kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hilo katika bajeti iliyopita nilikuwa nimeomba Serikali iweze kutoa kodi kwenye *solar*. Itakapofanya hivyo itakuwa imewasaidia sana wananchi hata wa vijijini na wao kuwa na uwashaji wa taa hata ile ya *solar*. Sisi leo tuko hapa mjini na tuko kwenye Bunge hili, taa tunaona saa hizi inatumulika na ndio mchana, lakini wenzetu hata usiku mwanga huu hawaupati. Sisi pamoja na kuwa ni mchana bado tunaongeza na taa lakini wao wa usiku hawauoni hata huu mwanga ambao sisi tunauongeza mchana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, basi Serikali ifikirie kutoa kodi kwenye *solar* ili wananchi wale waweze kupata urahisi na wao wa kununua *solar* kufunga katika majumba yao, kufunga katika zahanati na hata zahanati zetu ziweze kuhifadhi damu; mwanamke anapopungukiwa damu, basi iweze kuchukuliwa pale pale na kuwekwa katika mwili wake. Nina imani tutakuwa tumepunguza vifo vingi sana vya wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *SIDO*. Nina imani kuwa *SIDO* ni chombo ambacho tuna imani kitawasaidia akinamama katika maeneo mbalimbali, lakini bado naona *SIDO* inahitaji kuongezewa nguvu. Tumewapa akinamama mafunzo mengi sana ya utengenezaji wa batiki, utengenezaji wa sabuni Tabora pale na vifaa mbalimbali, masomo yale tumewapa kama Wabunge, kuweza kuwasaidia wengine Dar-es-Salaam, wengine Shinyanga na maeneo mbalimbali.

Lakini bado mafunzo yale wameyapata ili kuondokana na umaskini na kama wanaondokana na umaskini basi hata Serikali iweze kusaidia. Kama Wabunge tumeweza kuwasaidia kwa kutumia pesa yetu kuwapa elimu na wao watumie pesa ya Serikali kuweza kusaidia vikundi mbalimbali vya akinamama ili kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kuwa tutawawezesha wanawake kuondokana na umaskini, nawapongeza Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi na wengine wote ambao wameweza kuwasaidia wanawake katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, wale wanawake na wao wanahitaji kuongezewa nguvu ili waweze kupata mitaji ya kuendeleza maisha yao na watoto wao. Tuna wanawake wengi wajane na watoto yatima wengi. Kwa hiyo, pale atakapowezeshwa mwanamke mmoja katika maisha yake na katika mazingira yake, itaweza kusaidia watoto wao wakasoma na maendeleo katika maisha yao yakakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu suala la miradi inayoibuliwa. Miradi ambayo inaibuliwa na Serikali, tuna imani kuwa tuna wataalam wetu na kama tuna wataalam wetu, pale wataalam wanapowasaidia wananchi kuweza kuibua miradi mfano ya majosho na miradi ile baadaye ikawa haifanyi kazi, naomba niseme kuwa Serikali inahitaji kuwawajibisha wale wataalam ambao wamewapotosha wananchi kuibua miradi na kutumia pesa ya Serikali na pesa ya michango ya wananchi lakini baadaye ile miradi ikawa haiwezi kuendelea. Kwa sababu tayari na wao watakuwa ni wahujumu uchumi kwa sababu hawakutenda haki kuweza kutimiza miradi ambayo itakuwa imekaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba niwapongeze wanawake wa Mkoa wa Tabora kwa kunipa ushirikiano na kufanya nao kazi vizuri, nina imani wao wenyewe wanaelewa ni namna gani tumefanya kazi kwa pamoja. Lakini pili nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara yake ambayo ameifanya katika Mkoa wa Tabora, ambayo imetupa matumaini makubwa na wananchi wamefurahi zaidi kwa suala la kusimamia maji katika Wilaya ya Tabora Mjini. Pamoja na Rais, ameweza kusaidia zaidi, wananchi wamekuwa na imani kuwa maji safi na salama yataweza kupatikana kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pia nami niwashukuru wananchi wa Jimbo la Sikonge kwa kunipa nafasi hii ya kuwepo humu. Nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wasaidizi wake wote kwa hotuba yao nzuri, yenye mafanikio, iliyoonesha changamoto mbalimbali. Lakini kwa namna ya pekee nataka niipongeze sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, chini ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tumetekeleza Ilani kwa kiasi kikubwa sana. Nataka niwaambie wenzangu wale pale, ndugu zangu, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, ni ya Chama Cha Mapinduzi na kwa maana hiyo nimeona sasa kila mtu anabeba tu kitabu hiki anazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Waislamu ndio wanaojua *Quran*, wanajua *Quran* unaanzia kusoma kushoto kwenda kulia. Wakristu nao wanafahamu vizuri sana kusoma Biblia, kwa hiyo mtu mwingine tu ukipewa Biblia hiyo, ukaisoma mstari mmoja, inawezekana ukawa na maana tofauti kabisa. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba, Chama cha Mapinduzi kimefanya kazi kubwa sana, kinatekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kiwango kikubwa sana, mwenye macho haambiwi tazama. Kama huwezi kufahamu, nenda vijijini ukaone kazi nzuri iliyofanyika. Tumejenga mashule, tumejenga zahanati, sasa kama tunakaa mjini tu hatuoni kazi nzuri iliyofanyika,

nawakaribisha twende vijijini tukaone kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tumefanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kwa 92% Chama Cha Mapinduzi kimeshinda. Sasa Upinzani haujapata hata 10%, hutakiwi kwenda kwa mganga wa kienyeji kupiga ramli ili kujua ni chama gani ambacho kinaendelea kupendwa na wananchi wengi. Kwa hiyo, haya ni matumaini makubwa kwamba CCM inakubalika na haya ni matumaini makubwa kwamba Uchaguzi Mkuu ujao CCM itapata ushindi mkubwa sana wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niongelee ya kwangu. Changamoto, kila palipo na maendeleo kuna changamoto. Tumeongeza shule nyingi za msingi, tumeongeza shule nyingi za sekondari, tumejenga zahanati nyingi, tuna vituo vingi vya afya na ndio maana leo tunapata changamoto hapa. Sasa changamoto yangu ya kwanza, naiomba Serikali, vyote hivi tulivyoviweka hapo kwa wananchi sasa tunahitaji watumishi wa kutosha. Tembea huko vijijini na haya ni maendeleo watu wanafahamu, wale wa miaka ya nyuma wanajua, tulianzisha *UPE* kwa sababu tulikuwa na shule nyingi tumeanzisha kwa pamoja.

Kwa hiyo, sasa niiombe sana Serikali tujitahidi kuhakikisha kwamba tunatoa vijana wengi wanaomaliza katiika vyuo mbalimbali na kuwapeleka huko na sasa tunataka tuwaone vijijini. Nimeona kwenye mipango yenu ya maendeleo, mmeweka kwa idadi kubwa sana, watumishi tutawaandaa, lakini kwa namna ya pekee sasa niwaombe waende vijijini wakafanye kazi ya kusaidiana na ndugu wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la miundombinu. Naishukuru sana Serikali kwa kupandisha hadhi barabara zetu mbili pale Wilayani Sikonge, ile barabara inayotoka Sikonge – Mibono – Kipili na barabara ya Tituwo – Mole – Izimbili, mmezipandisha hadhi kuwa barabara za mkoa. Naomba sasa barabara hizi zitengenezwe ili zilingane na hadhi ilizopewa. Lakini nishukuru jitihada za Serikali katika utengenezaji wa barabara zetu za Taifa. Barabara ya kutoka Tabora – Rungwa, imetengenezwa angalau ni kwa kiwango cha changarawe, lakini imetengenezwa vizuri na inapitika, lakini bado barabara ya kutoka Tabora kuja Sikonge kwenda kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara inayopitia pale Sikonge kuelekea maeneo ya Koga mpaka Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa. Tunafungua barabara zetu Itigi – Tabora na barabara ya Nzega – Tabora, barabara ya Tabora – Urambo, kwa kiwango cha lami kwa matumaini ya baadaye, naomba sana ili tuweze kuufungua Mkoa wa Tabora, ni lazima vile vile tuendelee kufungua barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa – Mbeya na barabara ya Ipole – Koga – Mpanda, kupitia huko kwa jirani yangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, naiomba sana Serikali tuufungue Mkoa wa Tabora, sisi Mkoa wa Tabora kwa kweli ndio tumebaki barabara za lami tunazisikia, ukiacha ile barabara inayopita katika maeneo ya Nzega. Naomba sana kwamba barabara hizi zitengenezwe ili tuweze kufika mahali tuwasaidie wananchi wetu kusafirisha mazao yao na wao wenyewe kusafiri kwa uhakika zaidi. Hata wale wanaopiga kelele, basi wanaweza wakapita katika barabara hizo hizo zinazotengenezwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo kuhusu suala la kilimo. Naipongeza Serikali kwa kutupatia mbolea ya ruzuku, Wilaya ya Sikonge miaka miwili tumepata mbolea hii, imetusaidia sana kuongeza uzalishaji wa kutosha. Niiombe Serikali ijitahidi kuongeza kasi ya kuleta mbolea hizi mapema lakini vilevile vocha ziwahi na mbegu ziwahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo suala la tumbaku. Tumefanya mageuzi makubwa sana kwenye sekta hii ya tumbaku. Bei imeongezeka kwa kiwango kikubwa, basi niombe tu kwamba tumefanya mageuzi mengine ya kutenganisha huduma ya pembejeo kwa wakulima na wanunuzi wa tumbaku, lakini wakati wa soko anayeuza anashuhudia tumbaku yake inavyonunuliwa. Sasa yale ambayo kwa kweli yamepatikana kama matatizo katika msimu huu uliopita, niombe katika msimu huu ujao yasipatikane tena. Kwa mfano, wakulima wetu wengi katika kipindi kilichopita cha msimu wao wa kilimo wameshindwa kupata nyuzi kwa uhakika, wameshindwa kupata magunia kwa uhakika na vitu hivi baadaye tukaviona walanguzi wanawalangua wakulima wetu, wanaviuza kwa bei ya juu sana. Niiombe Serikali iwe makini sana katika kuwasaidia wakulima katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nimshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Amefika eneo linaitwa Kitunda, kwenye Tarafa ya Kiwele yeye amekuwa ni Rais wa kwanza kufika katika eneo lile tokea uhuru, amevunja rekodi. Wananchi wa Sikonge tunamshukuru sana, wananchi wa Tarafa ya Kiwele wanamshukuru sana. Nina uhakika yale yote aliyoyaahidi pale Serikali itayafuatailia katika kuhakikisha kwamba yanatimizwa ili wananchi wale waweze kufaidika na maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabisa niwashukuru wananchi wa Sikonge kwa kunipa nafasi hii. Ni matumaini yangu makubwa kabisa kwamba tumeshirikiana vizuri, tumefanya kazi nzuri na ni matumaini yangu makubwa kabisa kwamba watakichagua Chama Cha Mapinduzi katika uchaguzi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa wakati huu ili nichangie hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uislamu tunaamini kwamba Mwenyezi Mungu kaumba Mbingu, akaumba ardhi, akaumba na vyote vilivyokuwemo ndani yake na akamuumba binadam, akampa utukufu wa aina ya pekee. Juu ya utukufu huu, kwa bahati akatutofautisha, wapo watu wanafahamu, wapo watu hawafahamu, kuna watu wanafahamu mara moja na kuna watu wanafahamu baada ya kuchukua muda na kukaa na akazingatia. Kwa hiyo tusishangae na kustaajabu sana kuona kwamba kuna baadhi yetu wakawa hawaoni au hawatambui yale ambayo yanatendeka katika nchi yetu hii hasa katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niendelee kwa kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba pia ku-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii ambao tunashughulikia masuala ya elimu na afya. Sasa katika hotuba yangu hii ningeomba kuchangia zaidi kwenye suala la elimu. Nataka niipongeze Serikali kwa lengo ililolifikia na juhudi kubwa ambayo imepitishwa katika kufanikisha masuala ya elimu. Sio hivyo tu, lakini kwa vile katika masuala ya elimu Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anatoa hotuba yake, alizungumzia kuhusu *UDOM;* maendeleo yaliyokuwepo, kujengwa kwa chuo kwa kasi ya ajabu, hii ni dalili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwa kweli kuwapongeza viongozi wa *UDOM*, kwa sababu japokuwa wamepewa hii dhamana lakini wamekubali kuichukua dhamana hii na wanaitekeleza na kwa hiyo kwa asilimia mia moja nawapongeza sana kwa juhudi zao na nawatakia kila la heri, Mwenyezi Mungu awajalie wazidi kuwa na moyo huo huo wa kuendeleza elimu ya juu katika chuo hiki cha *UDOM. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusiana na elimu. Tunajua kwamba elimu ya juu kwa mujibu wa Katiba yetu ni chombo cha Muungano. Kwa muda mrefu nimekuwa nikilizungumzia suala la Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam kuhusu ujenzi wa *Institute of Marine Sciences* kule Zanzibar, Buyu. Ilikuwa inasikitisha sana kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tunakuja mbele ya Bunge lako hili Tukufu na kuuliza ni kwa nini chuo hiki hakijengwi, kinachukua muda wa miaka 10 takriban na kuanzia mwaka 2006 mpaka leo magofu yale yaliachwa hivi hivi bila kutengenezwa. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara, kwamba taarifa ambayo nimeipokea ni kwamba, safari hii chuo kile kimetengewa fedha na kitaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini wazi kwamba ujenzi huu hautasimama kama ulivyosimama katika kipindi hiki cha pili. Niwatakie kila la heri wale wajenzi na niwaombe wakandarasi warudi kwa imani kwamba sasa utekelezaji wa ujenzi wa *Institute of Marine Sciences* za bahari utaendelea kujengwa. Kwa hivyo, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waziri wa Elimu kwa juhudi zao kubwa za kufanikisha mara hii kuendelea na ujenzi wa chuo hiki cha taasisi za sayansi za bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu *Chuo Cha Mwalimu Nyerere Foundation*, kilichokuweko Kivukoni. Nitashukuru sana na hasa kama ikiwa tutamaliza muda wetu huu tukiona kwamba, chuo kile tunaendelea na kukihifadhi hasa kutokana na mmomonyoko mkubwa unaokikabili chuo kile. Naiomba sana Serikali zaidi ya yote na kwa kuzingatia heshima aliyokuwa nayo Mwalimu Julius Nyerere, basi tuhakikishe kwamba na kile chuo kinalindwa na kuhifadhiwa kufuatana na uharibifu mkubwa wa mazingira na mmomonyoko. Naamini kwamba ikiwa tutakiacha baada ya siku mbili, tatu, chuo kile tunaweza tukakipoteza na tukapoteza hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningelizungumzia mbali na masomo, nataka niishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kufikiria masuala ya kuleta *CDCF*. Lakini napenda kuiomba Serikali kwa kule Zanzibar, kulizingatia suala na ni jinsi gani fedha zile za *CDCF* zinavyokwenda. Mpaka hii leo naamini kwamba wenzetu wa Bara mmeshaanza kuzitumia lakini kule kwetu hatujaanza kuzitumia, kwa hiyo ningeomba ni kitu gani na utaratibu unastahiki ili ufanywe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Muyuni kwa juhudi kubwa ya kushirikiana na mimi katika kufanikisha maendeleo ya katika Jimbo letu la Muyuni. Naamini watu wa Jimbo la Muyuni ni katika jamii ile ambayo inafahamu mara moja sio katika ile jamii ambayo inataka ikae muda izingatie mpaka ichokonolewe ndiyo ifahamu.

Kwa hiyo, nawashukuru sana, naamini kwamba pale ambapo tumefikia na ushirikiano ambao tumekuwanao tutazidi kuuendeleza katika awamu zijazo na kwa wale wote ambao tunakuwa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunaleta maendeleo yetu katika nchi yetu hii ya Tanzania ikiwa ni pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba tena niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Elimu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jinsi wanavyotekeleza ahadi ambazo tumeziweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo napenda kuchukua nafasi kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza ambaye ametuwezesha kusimama hapa leo ili kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kusema kwamba Waswahili wanasema macho si mboni, unao ni moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunaambiwa Wapinzani hatuoni yaliyotendeka lakini sisi tuna moyo, tunayaona mengi sana na kwa sababu Mpinzani ndiyo kioo cha Serikali wenzetu lazima mkubali kwamba mna mapungufu na sisi ndiyo tunaopaswa kuyasema mapungufu na mnatakiwa mjirekebishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwenye suala la uchaguzi, sasa hivi tunaelekea kwenye uchaguzi na ndiyo maana nikaja moja kwa moja kwenye *point* hii. Uchaguzi ni sehemu muhimu ya maisha yetu na ni sehemu muhimu ya uongozi katika nchi na ni sehemu muhimu kwa kuwepo kwa Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Tanzania yetu tuna Sheria mbili za Uchaguzi, Sheria ambayo inafanya kazi Zanzibar ambayo ni (*ZEC)*, Tume ya Zanzibar, tuna Tume ya Uchaguzi ya Taifa (*NEC)*. Kule Zanzibar tunaingia katika uchaguzi wa Jimbo kwa kutumia sheria mbili, wanaoandikishwa kupiga kura katika daftari la uchaguzi la wapiga kura tunatumia *ZEC*. Lakini *ZEC* inaandikisha wapiga kura ambao wanachagua viongozi wote, Mbunge, Mwakilishi, Diwani, Rais wa Zanzibar na Rais wa Tanzania yaani Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule anayeandikishwa ni Mzanzibar mkazi ambaye lazima awepo katika eneo lake la uchaguzi si chini ya miezi 36 na huyu Mzanzibar mkazi anapatikana kwa shida kwa sababu sheria inayotumika ni kwamba lazima uwe na kitambulisho cha ukazi ambacho kupatikana kwake ni tabu sana, kuna vikwazo vingi pamoja na kelele nyingi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar tunamshukuru sana lakini watendaji wake hawaonekani kama wako *serious* katika kusimamia yale maagizo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Tume ya Taifa ya *NEC* iko kule inaandikisha wapiga kura, lakini hapo hapo wakala wao ni Tume ni ya Uchaguzi ya Zanzibar, *that means* wao wanakwenda kuwaandikisha watu ambao hawajaandikishwa katika daftari la Zanzibar. Sasa juzi nilimsikia Mheshimiwa Mkurugenzi akizungumza kwenye semina fulani akisema kwamba wataandikishwa wale wote ambao hawajaandikishwa, ni sawa, wale wote ambao wamefikia umri wanayo haki ya kuandikishwa, ndiyo wataandikishwa, ni sawa sawa.

Lakini je, wakishaandikishwa hao hoja yangu ni kwamba, hao wanakuja kumchagua Rais wa Muungano tu au na ile haki ya kumchangua Mbunge itakuwa ipo? Kwa sababu wao wameshaandikishwa kwenye daftari la uchaguzi la Zanzibar ambalo ni wakala wao. Sasa wale ambao wataandikishwa huku je, watakuwa na haki ya kumchagua Rais au watakuwa na haki ya kumchagua pia na Mbunge, kwa sababu kule tayari wameshaandikishwa ambao wanamchagua Mbunge, sijui nimeeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hoja ni kwamba, Mbunge wa Handeni na Mbunge wa Tumbatu au Mbunge wa Kojani wanachaguliwa kwa sheria mbili tofauti? Wote hawa si Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano? huu ni utata ambao unapaswa tuushughulikie na tuutolee uamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo utakuta kuna watu ambao wameachwa katika daftari hilo ambalo kuna kura za Mbunge ambazo atazikosa, kwa mfano, Jimbo la Kojani, mwaka 2005 waliandikishwa watu 10,503. Sasa hivi kwa kupitia sheria hiyo ambayo ukazi umetumika wameandikishwa watu 7,444, kama hao watapiga kura ya Rais ina maana kura za Mbunge hapo zinakosekana, tumemnyima haki Mbunge wa Zanzibar, tumemnyima kura zake Mbunge ambaye sawa na Mbunge wa Handeni au Mbunge wa Geita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumzie ni suala la uwazi na uwajibikaji, katika Tanzania tuna viongozi waliopatikana kupitia vyama tofauti lakini kinachoonekana ni kwamba kuna baadhi ya viongozi huko katika ngazi za vijiji na mitaa hawashirikishwi katika maamuzi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna miradi ambayo inatekelezwa katika wilaya ya Geita katika vijiji fulani, ukitaka ushahidi nitauleta, Wenyeviti wanalalamika kwamba wao miradi hiyo inashughulikiwa na Diwani na watendaji wake na wao hawashikirishwi na miradi inatekelezwa wale wenyeviti ndiyo ambao wamechaguliwa na wananchi, kwa hivyo lazima washirikishwe katika miradi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ningesema niliongelee ni kwamba tunazungumzia sana suala la elimu, tumeambiwa kwamba elimu imepiga hatua mashule mengi tumejenga ni sawa shule nyingi za Sekondari zimejengwa, je kuboresha elimu ni kujenga mashule tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba tumejenga mashule ni sawa lakini je, walimu wapo wa kutosheleza, wako walimu ambao wamewekwa vizuri na wanaweza kufanya kazi zao wakiwa na mudi nzuri ya kufanya kazi, sisi sote hapa tusingekuwepo kama si mwalimu, tuko hapa sote kupitia mwalimu. Kwa hiyo, ni lazima tumtunze mwalimu, tumpe heshima, tumpe hadhi, tuwajengee nyumba walimu, tunapojenga shule tujenge na nyumba ambazo watakaa walimu hao lakini si hilo tu na tunapoletewa walimu huko vijijini tuwaheshimu, tusiwapige.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wanapigwa kiholela kwa sababu za kijinga jinga tu. Tumfikirieni mwalimu huyu atakuwa na uwezo wa kufundisha kweli katika eneo hilo? Atakuwa na uwezo wa kufanya kazi yake? Ni lazima Mheshimiwa tuhakikishe kwamba mwalimu analindwa kwa heshima yake ipasavyo, mwalimu anapewa hadhi yake na kama kuna watu ambao wamevunja sheria kumchapa mwalimu viboko, kumuumiza mwalimu kwa njia moja au nyingine tuhakikishe kwamba hao wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye maridhiano ya Zanzibar, sasa hivi Zanzibar tunamshukuru Mwenyezi Mungu tunaishi kwa amani na utulivu, tunawashukuru viongozi wetu wakuu, Mheshimiwa Rais Amani Karume, kwa uongozi wake mahiri na kwa ujasiri wake kwa kukubaliana na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Self Sharif Hamad na wakaleta maridhiano ya Zanzibar, Wazanzibar tunaishi kwa amani na kwa utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuelekea uchaguzi ujao naomba sana Jeshi la Polisi lilinde heshima hii na maridhiano haya yaliyopo ili tuingie katika uchaguzi na tumalize uchaguzi uwe wa huru na wa haki. Mara nyingi Jeshi la Polisi ndiyo linalotumiwa vibaya pamoja na kuwapigia kelele sana wapewe mafao yao, wapewe maposho yao wasidhalilishwe, wapewe haki zao ambao zinastahiki ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Vinginevyo watatumika vibaya, wanatumika kwa kushirikiana na vikosi vya SMZ ambao inaonekana Jeshi la Polisi hufika mahali likazidiwa nguvu na vikosi vya SMZ kama KMKM. Msaidizi wa *IGP* ana ushahidi, nilimpigia simu wakati fulani kuzungumzia masuala hayo, askari polisi unamwita, anaogopa kuondoka mguu mmoja kwenye KMKM. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu, hoja ya Waziri Mkuu mwaka 2010/2011. Nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala* aliyenijalia uzima niwapongeze wananchi wa Jimbo la Mtambile kwa ushirikiano wao mzuri wa kila siku, Mwenyezi Mungu *Inshallah* awabariki tuendelee kuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kwa kusema kwamba mwaka 2010 ni mwaka wa uchaguzi lakini kabla ya mwaka 2010, mwaka 2009 tulikuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa ilidhihirika na ilibainika kwamba uchaguzi ule hasa Watendaji wa Mitaa hata na Vijiji baadhi yao walitumika vibaya. *(Makofi)*

Walitumika vibaya katika taswira nzima ya kubambikizwa kesi, wanachama wetu wengi walibambikizwa kesi na kwa bahati mbaya sana taswira hiyo hivi sasa imechukua sura nyingine, kila wakati tunapata taarifa kwamba kuna viongozi wa *CUF*, wanachama wa *CUF* wamekamatwa na wanatakiwa waende Polisi. Kwa kweli hili si jambo zuri, ni vyema tuelewe kwamba Wakuu wa Wilaya tuna jukumu kubwa, Wakuu wa Jeshi la Polisi ndani ya Wilaya tuna jukumu kubwa, wote ni walezi wa vyama vyote tusiwe na upendeleo wa aina yoyote, nawaombeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni sana kwa viongozi wa ngazi mbalimbali ama wawe wa Kata, wa Wilaya, wa Serikali, kutoa taarifa sahihi kwa mambo yafuatayo: Watoe taarifa kwamba hasa kuna ujambazi umekithiri, wananchi wamechoka na ujambazi, watoe taarifa kwamba kuna meli za kigeni zinavua isivyo halali, Serikali inakosa mapato, watoe taarifa ya aibu tunayoipata ya kuchakachua mafuta, hayo ndiyo mambo ya msingi lakini kuvifuata fuata Vyama vya Upinzani kila wakati kubambikiza kesi si halali, haipendezi, viongozi wa juu wa Jeshi la Polisi, hili wanalijua nami wakati huu nikiongelea wanafahamu nini ninachoongelea, tunashauri kwa vyombo vya ulinzi na Usalama wawe makini kwa kipindi hiki kuelekea uchaguzi Mkuu wakati huu ambapo kuna watendaji wanapenda kubambikiza kesi hasa Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja sasa kwenye suala zima la nidhamu na matumizi ya fedha za umma, wiki iliyopita Serikali ilitupa taarifa kwamba fedha nyingi za Halmashauri, fedha za maendeleo zimerundikwa kwenye akaunti bila kutumiwa, Serikali haikutuambia kwamba ni Halmashauri gani hizo na haikutuambia kwamba wahusika watafanya au wamefanywa nini? Hii ni tabia mbaya, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifanya majumuisho, alieleze Bunge hili Tukufu kwa niaba ya Watanzania, Halmashauri hizo ambazo hazikutumia fedha za maendeleo kipindi kilichopita ni ngapi na waliohusika watafanywa nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30 mwaka 2007 ilionyesha kuna upotevu wa fedha na mali wa jumla ya shilingi bilioni 2.3. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2008, ilionesha kuna upotevu wa fedha na mali bilioni 3.5 na ripoti hiyo hiyo kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2009, ilionesha kuna upotevu wa fedha na mali jumla ya shilingi bilioni 3.1, unajiuliza mabilioni yote haya ambayo yanachukuliwa yanapotea Serikali haijui, inakuwaje? Ni kwa nini haikuchukua hatua madhubuti tukafuata ushauri wa *CAG*? Hizi ni fedha za umma fedha za wanyonge walala hoi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashangaa sana nchi hii unapokwenda kwenye magereza unawakuta watu ambao wamefungwa miaka mitano kwa sababu wameiba ng’ombe au mbuzi, wengine wamefungwa miaka sita, sheria ya mifugo iliyoletwa. Lakini wale ambao wanachukua mabilioni ya fedha wanadunda, kumbe nchi hii ukiiba kweli hufungwi, kila mtu anachukua chake mapema, haipendezi. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naelewa ninachokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limechukua sura nyingine tangu zamani, kuanzia mwaka 2001 mpaka 2006, wizi, ubadhirifu na ufisadi umefanyika kwa jumla ya shilingi bilioni nne, milioni 403 taarifa rasmi ya Bunge tarehe 31 Januari, 2008 tunayo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikienda Mahakamani ikashtaki kesi 321, Serikali inashinda kesi 14, ni aibu kubwa, Serikali ina wataalam wa kutosha, ikabwagwa Serikali Mahakamani inakuwaje bilioni nne hazikupatikana lakini Serikali ikatujibu hapa Bungeni ikasema kwamba fedha hizo hazikupatiana kwa sababu wahusika wametoroka,

ni aibu kubwa na fedheha. Lakini ikasema baadhi ya ushahidi haukupatikana, chukueni *Hansard* tarehe 31 Januari, 2008, Serikali msome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka niongelee katika hili, taratibu za ukusanyaji mapato ni nzuri, tunaipongeza *TRA* kukusanya angalau bilioni 390 kwa mwezi, ni jambo nzuri. Lakini utaratibu wa kukusanya mapato tuangalie vizuri yaliyotokea Tunduru tarehe 9 Juni, ambapo watu wawili waliokaa katika mgahawa Mgesa wakapigwa risasi na Polisi katika mchakato wa kutafuta kodi, wakati wa kukusanya kodi baina ya *TRA* na Polisi na hao mabwana wapo kwenye hospitali ya Ndanda Masasi, Kelvin na Adamba wapo, haipendezi, si vizuri hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa haraka haraka niangalie na suala la wastaafu, wastaafu wetu hali zao ni mbaya kila wakati, hapa Bungeni tumekuwa tukipiga kelele, lakini imedhihirika kwamba bado kima cha chini cha pensheni cha wastaafu shilingi 50,000 hakitoshi, wastani wa shilingi 1,670 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi kuliko yote kinachoonekana hata wakati wa kukokotoa mafao hayo, wastaafu wanapunjwa, ukiangalia majalada ambayo yamechukuliwa ya aina mbalimbali katika mwaka 2008, 2007 unaona ukokotoaji umewapunja wastaafu na ushahidi upo kwenye ripoti ya *CAG*, hili si jambo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tuwapunje wazee wetu au hakuna wataalam wa kutosha, kila siku tumekuwa tukipiga kelele, utaratibu huu mpaka lini utamalizika, inakuwaje lakini? Tusemee wapi sisi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja amegusia hapa katika Uislamu, kwenye Uislamu pia unasema mnaamrisha watu kufanya mema hali yakuwa ninyi wenyewe mnasahau nafsi zenu. Ilani yenu hii ndiyo mliyoeleza humu mambo mengi lakini hayaelezeki angalieni vizuri kuna mambo humu hayatekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na umri iliyoniwezesha leo kusimama katika Bunge lako Tukufu na nikachangia hoja. Lakini pia napenda sana kuwashukuru sana wanawake wa mkoa wa Pwani kwa kunipa ushirikiano wa muda mrefu na upendo na urafiki ambao naamini utazidi kudumu hata kwa kipindi kinachokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kuanzia tu napenda kusema naiunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mengi yamesemwa ambayo na mimi ningekuwa niyaseme, kwa hiyo nisingependa kurudia, kwa hiyo, nayaunga mkono kwamba

tumetekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa kasi kubwa kabisa, kwa ari kubwa na kwa uwezo mkubwa yaliyobakia hayo ni mashimo tu madogo madogo ambayo nina hakika kwa kipindi kifupi kinachokuja tutatekeleza yale yaliyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mkazi wa Mafia, nimekuwa Mafia zaidi ya miaka thelathini na sita na kilio kikubwa cha watu wa Mafia ilikuwa ni *gati*. Kwa muda wa uongozi wote wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, watu wa Mafia walikuwa wanalilia. Mimi nikiwa mmojawapo nikichangia Bungeni lakini na Viongozi waliopita pia ilikuwa neno lao kubwa ni *gati*. Sasa nitakuwa sitendi haki kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama sikuchukua nafasi hii, kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa niaba ya watu wa Mafia na hasa akina mama ambao walikuwa wakipata taabu sana wakati wa kusafiri. Naomba tu Mungu ajalie yale yaliyotamkwa humu kwamba gati la Mafia linajengwa na hivi sasa ndugu zangu napenda kuwaambia kwamba gati limeanza na linakwenda kwa kasi kubwa sana. Kwa kweli, tunashukuru na kuna nadhiri mbalimbali ambazo watu wa Mafia tumeziweka kwa gati hii na nina hakika na naomba Mungu na mimi nikiwa mmojawapo nilione gati hili na meli ikiweka nanga pale. Nina hakika, kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hili litafanywa. Lakini kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja Mafia kwamba gati litajengwa na kweli inajengwa ndugu zangu wala siyo hadithi, kwa hiyo, nategemea kilio cha Mafia kwenye gati kitaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea suala la kiwanja nalo litafuatia kwani Mafia ni sehemu ya utalii, tunahitaji ndege zitue ili kuweza kuhimiza masuala mazima ya utalii wa ufukweni. Kwa hiyo, nina hakika, kwa Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi na hili litatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kweli si kwa Mafia tu, ahadi zake nyingi ambazo ameziahidi yeye kama Rais, zimetekelezwa na zinaendelea kutekelezwa, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia napenda kumshukuru sana Mama Salma, ndiyo, kwenye mafanikio ya mwanaume na mwanamke yuko nyuma. Lakini huyu Mama siyo tu yuko nyuma bali anatembea, ametufanyia kazi kubwa sana sisi akina mama na watoto, ametembea karibuni Tanzania nzima kusaidia vifaa vya Zahanati kwa ajili ya uzazi salama kwa akina mama lakini pia anakemea masuala ya mimba za watoto wa kike mashuleni. Mama Salma anasema “mtoto wa mwenzio ni wako”, hii ni kauli yake ya kudumu. Huyu mama jamani mimi nasema namshukuru sana na Mungu ampe afya njema, azidi kumsaidia Rais wetu lakini na moyo wake wa kujituma. Mungu ampe afya aweze kuyafanya yale yote anayodhamiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye Kilimo Kwanza, nashukuru Mheshimiwa Mwandosya aliwahi kusema kwamba kilimo ni maji. Sisi Mkoa wa Pwani tuna bahati kwani tuna maji ya kutosha kabisa, tuna mito kama mto Ruvu, Rufiji na Wami. Sasa ndugu zangu wa Kilimo Kwanza wakati Mheshimiwa Mwandosya anaongelea habari ya maji ya kuvunwa, sisi Mkoa wa Pwani tuna maji ya kudumu na yanaingia baharini. Hatujayatumia vya kutosha kwenye suala la kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi katika mikakati yake ya Kilimo Kwanza, hatujachelewa, kilimo cha umwagiliaji kifanywe kuwa mfano ndani ya

Mkoa wa Pwani kwani maji yapo, wala siyo ya kutafuta, ni zana tu na utaratibu ambao unatakiwa kitaalamu ili kuweza kuyatumia maji haya kwa kilimo cha mpunga na mazao mengine ambayo yanahitaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuliongelea, ni suala la Mfuko wa Wanawake na Vijana. Kuna baadhi ya Halmashauri zimekuwa sugu, nakuomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, zichukulie hatua. Hizi pesa si zao, ni pesa za Wanawake na Vijana, ni *percent* ambayo imehalalishwa. Wamezitumia wapi na wanataka tuwafanye nini sisi Kamati ya *LAAC.* Kila siku tunatoa maagizo, tunaomba ifikie mwisho, wawape pesa zao akina Mama na Vijana. Tunaongelea umaskini lakini Serikali inajitahidi kuweka mipango mizuri lakini baadhi ya wachache wanaikalia, wanawaadhibu Vijana na Wanawake. Hizi Halmashauri kama arobaini, naomba Waziri mhusika uzichukulie hatua, watoe pesa za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwaongelea Madiwani. Wanafanya kazi kubwa tu. Sisi tukiingia Bungeni kitu cha kwanza tunakopeshwa gari, sasa naomba kwa utaratibu wowote ule, Madiwani wakiingia tu kwenye Udiwani, jamani wakopesheni angalau pikipiki isiwe tu labda mtu kafanya hivi na vile. Lakini wapeni pesa mtu atakayeweza kununua pikipiki au anaweza kuongeza mwenyewe kwa kutumia mkopo wa aina yoyote kuweza kununua gari ili waweze kufanya kazi zao vizuri kama tunavyofanya sisi, wanapata taabu. Madiwani ni watu ambao wanapata taabu, posho yao ni ndogo, tunakubali. Basi hata kuwakopesha vitendea kazi? Tunaomba hili Mheshimiwa Waziri ulione na uweze kuwatengea fedha kidogo za kuweza kuwakopesha pikipiki au kuongezea kununua vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijitendei haki na wala sitakuwa nawatendea haki watu wa Mafia ninakoishi muda mrefu kuliko sehemu nyingine kwamba ni moja ya Wilaya ambayo iko katika mazingira magumu. Tunajua Mheshimiwa Waziri umesema kuna Wilaya ambazo zimetengewa fedha, tunashukuru nyumba za watumishi zinajengwa lakini bado tunahitaji msaada zaidi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaamini yale ambayo nimeyaomba, yatatekelezwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunakushukuru, Mheshimiwa Florence Kyendesya atafuatiwa na Mheshimiwa Michael L. Laizer.

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii adimu ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Waziri Mkuu ambayo inaleta matumaini kwa Watanzania endapo ufuatiliaji utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa utekelezaji wake mzuri na imara wa Ilani ya Chama cha Mapunduzi uliofanywa kwa kipindi chote hiki kuanzia mwaka 2005. Hawa wanaobeza, ni haki yao waibeze lakini naomba waelewe kwamba hii ni Serikali inayoendelea siyo kila kitu kinatekelezwa kwa wakati mmoja. Hata ndani ya familia huwa tunafanya mipango lakini haitekelezwi kwa kipindi hicho hicho, naomba waelewe hiyo. Wengi wamesoma kwenye shule zilizojengwa na Serikali ya Awamu ya Nne, barabara wanazopita ni Serikali ya Awamu ya Nne imetengeneza, Zahanati na Hospitali wanakotibiwa na familia zao, zote zimejengwa na Serikali ya Awamu ya Nne, naomba tuipongeze wote na tuache kupiga kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na fadhila kama sitawashukuru wanawake wa Mkoa wa Mbeya, kwa imani waliyonipa kwa kipindi hiki cha nusu ya awamu, kwa kuwa sijamaliza kipindi chote. Nimekaa kwenye Bunge hili kwa nusu kipindi tu naamini wataniona na watanifikiria tena, hawataniacha, bado nina imani nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijikite kwenye hoja ambayo nataka kuizungumza kwenye Bunge lako Tukufu. Katika Mkoa wa Mbeya, tuna kilio kikubwa sana kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe. Tumekuwa tukiongelea mara nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mbeya wamekuwa wakipiga kelele kuhusu suala hilo. Huyu Mkandarasi, Kundasin, aliyepewa jukumu la ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe, ni jeuri. Nasema ni jeuri kwa sababu kwanza alikwenda Zanzibar wakamfukuza kwa sababu ya ubabaishaji. Mkandarasi huyo huyo ndiye aliyepewa jukumu la kujenga barabara ya kutoka Mbeya – Lwanjiro - Chunya hadi Makongorosi, ameshindwa na kesi iko Mahakamani. Mkandarasi huyo huyo ndiye aliyepewa tena kazi ya kujenga Uwanja wa Songwe wa Mbeya, hatekelezi ahadi au makubaliano yaliyo ndani ya mkataba na mkataba unasema hivi atakayesimamia kazi hiyo ni Mhandisi lakini wanasimamia *Technicians* hivyo kuna ugomvi kati ya huyo Mkandarasi na Msimamizi Mkuu wa kazi hiyo. Sasa ya nini tuendelee naye, kuna nini? Naona Serikali imenisikia na hali halisi ndivyo ilivyo, naomba ufuatiliaji uwepo vinginevyo huyu atatuacha kwenye mataa, naomba aondolewe na awekwe mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hili ningekuwa nalia machozi hapa lakini nikilia Kanuni itanibana ila nitakuwa natoa machozi kimyakimya tu, ni kuhusu vitendo vya ukatili na kinyama vilivyofanywa katika Wilaya ya Rungwe vya ubakaji wa watoto wadogo wa kike wenye umri wa miaka miwili, minne hadi mitano. Vimetokea vitendo sita katika eneo moja mfululizo. Hawa wanaume wenye ukatili ambao hawana huruma, wanawabaka wale watoto wadogo wa kike na kuwanyonga shingo, maiti zinaokotwa zinaning'inia miguu, hili kwa kweli linatia uchungu mkubwa sana. Naipongeza sana Serikali ya Mkoa wa Mbeya, chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa, Ndugu John Mwakipesile, wakiwa pamoja na Viongozi wa Dini zote, Maaskofi na Masheikh, walifanya kongamano kubwa sana kule Rungwe na walilia kwa machungu kutokana na vitendo vichafu ambavyo havina huruma yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpongeze kabisa kwa dhati Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Ndugu Jackson Msomi, nadhani Waziri Mkuu umelisikia hilo jina, huyu kwa kweli pamoja na kwamba baadhi yao wamekamatwa lakini yeye mwenyewe baada ya kuona ukamataji wake haridhiki nao, unasuasua na mtuhumiwa yupo, yeye mwenyewe alimkatama na kumkabidhi kwa *RPC*. Mimi ninashauri hawa waliokamatwa, kesi zao zingeshughulikiwa kama zilivyoshughulikiwa za wauaji wa Walemavu wa Ngozi yaani Maalbino, kesi zao zimekwenda vizuri na upelelezi ulikwenda vizuri na hukumu ilitolewa nadhani Watanzania wengi tumeridhika nayo, naomba iwe hivyo, naona limeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba wengi humu tumesikia tukizizungumzia Halmashauri zetu, kwa kweli Halmashauri ndiyo roho ya Taifa na ndiyo injini ya Taifa. Tunazungumzia maendeleo hapa lakini kama Halmashauri zetu hazitakuwa makini, tutakuwa tunaongelea mwaka hadi mwaka. Mimi ninaomba au ninashauri kwamba hawa Wakaguzi wa Ndani wasiwe wanakagua tu kwenye makaratasi Ofisini, wasiwe Mangimeza, wawe wanakwenda mpaka kwenye *site*, wanalinganisha fedha iliyotumika na mradi unaotajwa, ndipo kwa kweli wanaweza kuona hali halisi ilivyo kuliko sasa kukaa mezani na kuanza kufanya ukaguzi wao. Mimi naona hii kazi haitakwenda vizuri maana Watanzania wengi maendeleo yako kwenye Halmashauri, utekelezaji wa Halmashauri ukiwa mzuri, hapa ndani kelele hazitakuwepo. Mimi ninaomba Wakaguzi wa Ndani wawe wanakwenda kwenye *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nizungumzie kuhusu hawa watoto yatima. Nampongeza Mheshimiwa Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, yeye anasomesha watoto yatima 60, kwa hili, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *NGOs* nyingi ambazo zimefumuka zinashughulikia watoto yatima ambao wazazi wao wamekufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI, utakuta watu binafsi wanasema tunakwenda kuwasaidia watoto yatima ambao wazazi wao wamekufa kwa ugonjwa wa UKIMWI, sasa kila mmoja huko huko kwa kuwa mashirika ya kimataifa yanaleta pesa, hawa yatima wengine, je, waende wapi? Waende wapi? Kuna wengine wamefiwa na wazazi wao kwa ajali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Tayari Mama Kyendesya!

**MHE. FLORENCE E. KYENDESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Michael L. Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Makwetta, naamini yupo na baada ya hapo, Mheshimiwa Benson Mpesya ambaye simuoni humu ndani, atafuata.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Waziri Mkuu na natanguliza kusema kwamba naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya siasa, mimi nitayaacha kwa sababu umebaki muda mfupi twende kwenye majukwaa na hii Ilani ya Uchaguzi tutaipeleka huko kwenda kuinadi kwa wananchi na wananchi ndiyo wanajua tumefanya nini na nani apewe nchi aongoze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana wafuatao waliotusaidia kutokana na ukame uliotukumba mwaka jana. Jimbo la Longido, lilikumbwa na ukame mkubwa sana lakini namshukuru sana Rais alifika Jimboni na kuona hali hiyo, namshukuru Waziri Mkuu naye alifika Jimboni, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Phillip Marmo naye alifika, namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Peniel Lyimo, naye alifika na ninaishukuru sana Serikali kwa kuwapa chakula, hakuna aliyekufa kwa njaa, wananchi walipata chakula. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa msaada huo. Ninawashukuru sana kwani juzi walitoa shilingi milioni 107 kulipia usafiri wa chakula hicho. Namshukuru na Mkuu wa Mkoa kwani amekuwa msaada sana, alikuwa akifika mara kwa mara na amekuwa akitoa taarifa ya hali ya njaa ilivyo katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukame huo ulikuwa ni ukame ambao hatujawahi kuuona, mifugo ilikufa kwa 65% na mpaka sasa kuna familia ambazo hazina mifugo kabisa na siyo wakulima. Hiki Kilimo Kwanza tunachokisema katika Jimbo langu tunasema kwamba ni Mifugo Kwanza kwa sababu kuna maeneo ambayo huwezi kulima. Kwa hiyo, mifugo imekufa na hawana chakula mpaka sasa lakini nashukuru Waziri Mkuu na Serikali inajua kwamba kuna watu ambao wameathirika hawana chakula. Nategemea kwamba Serikali itatafuta namna ya kuwalisha hawa watu, asilimia kubwa hawatakuwa na chakula kwa sababu kuna waliobakiwa na mifugo na kuna wengine ni wakulima wamelima na vyakula vimeanza kupatikana lakini kuna wale walioko katika maeneo ambayo siyo maeneo ya kilimo, Serikali iwaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kuzungumzia, ni hali ya Jimbo la Longido. Kama mnavyojua Wilaya ya Longido, ni Wilaya mpya ambayo bado haina miundombinu mingi, kwa mfano, hatuna hospitali ya Wilaya, katika maombi yetu maalumu, tuliomba kwamba tujengewe hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Ufundi *(VETA)*, Wilaya ya Longido, ni miongoni mwa Wilaya 28 ambazo zimependekezwa kujengewa chuo cha *VETA* katika awamu ya kwanza. Mpaka sasa hatujui kinachoendelea kwamba chuo kitajengwa lini, lakini tunategemea kwamba kama Serikali inavyofanya kazi kwa awamu, inawezekana na sisi tukahesabiwa wakati mwingine. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ninaomba Ofisi ya Waziri Mkuu, fedha zinazopelekwa Halmashauri ni nyingi sana lakini sio zote zinazokwenda katika miradi ya wananchi nyingi zinaingia katika matumizi mabaya, tunaomba ofisi yako isimamie sana hizi fedha zinazokwenda katika Halmashauri zote. Kamati ya Bunge ya Hesabu za

Serikali za Mitaa *(LAAC)*, wakileta taarifa ya upotevu wa fedha, tutagundua kuwa ni mabilioni na mabilioni, fedha hizo zingefanya kazi za wananchi, naomba Serikali kwa kweli iangalie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara. Wilaya yetu ya Longido hatukuwa na barabara kabisa, ukiondoa barabara ya lami inayotoka Arusha kwenda Nairobi, barabara zingine ni mapito ya mifugo, sasa tunataka na sisi kufungua barabara zinazounganisha Kata na Tarafa. Kama tulivyoomba katika bajeti maalum, tunaomba tupewe fedha ili na sisi tuweze kufungua barabara za Jimbo la Longido ili wananchi waweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ujenzi wa Kituo cha Polisi au Makao Makuu ya Polisi. Kituo cha Polisi kilichopo pale Longido, kilijengwa na Wakoloni kabla hatujapata uhuru. Hakuna jengo hata moja ambalo limeongezwa, ni majengo yale yale ya wakati ule wa Ukoloni na hapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya. Hivi jamani, toka hatujapata uhuru, sijui zimejengwa mwaka 1954, kwa kweli sijui zimejengwa mwaka, kwa hiyo, ingefaa sasa kama Wilaya tuwe na Makao Makuu ya Wilaya ya Polisi na hii ni Wilaya ambayo iko mpakani, suala hili muhimu sana lizingatiwe ili Serikali iweze kulinda wananchi pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Nipende tu kusema kwamba katika Wilaya yetu, watoto wa wale watu ambao wamekuwa maskini hawako shuleni tena, wameshindwa kabisa kulipa ada, wengi wamerudi nyumbani. Sio kwamba wamerudi kwa sababu wazazi hawataki kuwasomesha, ni kwa sababu hawana uwezo na wengine hawana hata fedha ya kununua *uniform* za shule. Kwa hiyo, naomba Serikali itazame hali hiyo iliyojitokeza ambapo ni madhara yaliyotokea baada ya ukame. Naomba Serikali iangalie hali hiyo, najua imekwishapata taarifa hiyo na mmekwishafanya vikao namna ya kuisaidia Wilaya hiyo ya Longido na msifananishe Wilaya ya Longido na Wilaya zingine za wafugaji kwa sababu hata ukame haukufanana katika maeneo yote. Hali ya ukame iliyoko kule Kenya imefika mpaka Longido. Kule Kenya hakuna tena mifugo, wanategemea mifugo kutoka Longido. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie hali ya Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na narudia kusema kwamba naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana. Mheshimiwa *Senetor* Jackson Makwetta anaweza akawa msemaji wetu wa mwisho mchana wa leo.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii adimu na ningependa kutumia nafasi hii kukupongeza wewe na Mwenyekiti mwenzako, Spika na Naibu Spika, kwa kazi nzuri mnayofanya ya kuendesha Bunge hili. Usimamizi wenu mzuri wa Bunge hili, unatupa heshima sisi Wabunge na wananchi ambao tunawawakilisha, dumisheni tabia hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninapenda kutumia nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wanaomsaidia, Katibu Mkuu na Wataalam wote, Wakuu wa Mikoa na Ma-*DC*, kwa kazi nzuri wanayofanya ya kusimamia utekelezaji wa Ilani katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, imejibu baadhi ya maswali magumu ambayo tumekuwa tukiuliza hapa na kwa kuwa yeye ni mratibu, *approach* hii nadhani ingedumishwa kwa sababu wengine wanashughulikia yale maeneo yao ambayo ni *specific*. Sasa kwa kuwa, mimi ni Mbunge, ninapenda vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uamuzi wake wa kuongeza mbolea ya ruzuku katika ile Mikoa minne. Kwa mazingira haya ambayo tunayaona hivi sasa katika Tanzania, bila uamuzi ule, hali yetu ya chakula ilivyo na inavyoelekea, ingekuwa ngumu zaidi. Wakati mwingine katika mambo mengine, ni vizuri kuamua hata bila kujali *democracy*, kwa sababu ukisema ugawanye mbolea kwa kila mtu ili iwe nini? Kwa miaka 20 katika nchi hii, utabiri wa hali ya hewa unaonyesha kwamba mvua zimekuwa za uhakika katika Majimbo hayo ambako mbolea imepelekwa kwa wingi zaidi kuliko mahali pengine na ripoti ya *FAO*, inaonyesha kwamba kwa miaka ijayo wapi kutakuwa na njaa zaidi katika Tanzania. Kama ninavyopendekeza kila wakati kwamba, haya mabonde kama ya Kilombero, Lwiche, Rufiji, ni maghala yetu ya chakula, tuyatumie kuzalisha chakula badala ya kupeleka ng’ombe lakini utekelezaji unakuwa mgumu, tunataka *democracy*, haiwezekani, itabidi mambo mengine tuamue kwa manufaa ya watu. Mahindi yanayopatikana Songea, Mbeya, Iringa, ni kwa Watanzania wote kama ungelima mahindi Dodoma na ukaleta mbolea ya ruzuku kwa mazingira ya mwaka huu tungepata mahindi, nadhani nimeeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, napenda kuwapongeza wananchi wa Wilaya ya Njombe kwa ujumla na hasa wa Jimbo langu la Njombe Magharibi, kwa kutekeleza vizuri maagizo ya Kilimo Kwanza na kutumia vizuri mbolea ya ruzuku na tunaomba sasa kutokana na uzoefu na matoekeo haya, tuongeze mbolea ya ruzuku na tuongeze usimamizi na kuboresha utaratibu na tupeleke mbolea mapema. Kwetu sisi mbolea ya ruzuku ni MKUKUTA, ni njia ya kuondoa umaskini kwa haraka zaidi na ni njia ya kuwahakikishia Watanzania kwamba tuna chakula, bila chakula hakuna amani. Mnaweza kuwa na Polisi kila mahali kwa lengo la kudumisha amani, lakini kama kuna njaa, hawataweza. Kwa hiyo, ulinzi *number one*, ni chakula na risasi inafuata baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni kutokana na Ilani ya Uchaguzi ambayo ni ya Chama cha Mapinduzi, tunabishana bila sababu, sisi ndiyo tunaotawala, tumeweza kuitekeleza vizuri katika Wilaya ya Njombe kwa ujumla, kilimo cha miti, chakula, barabara, zahanati, nyumba bora, maji, umeme, nadhani mnaotembelea Njombe, katika nchi hii nadhani Njombe ni kama kisiwa katika shughuli za maendeleo. *It is ever green* na ndiyo chanzo cha mito kama Ruaha, Kilombero na kwa sababu ya *attitude*, mvua ni za kuaminika zaidi. Ni sehemu ya Tanzania na ni vizuri wakati mwingine bila kuwa na ubinafsi wa kupindukia kuelekeza nguvu pale ambapo uhakika ni mkubwa zaidi. Wananchi wa Njombe wana historia ya bidii katika kazi na uaminifu na kwa pamoja na viongozi wao tumeweza kujenga Njombe na kuiweka katika ramani ya maendeleo ya

nchi hii. Leo Njombe ni *synonymous* na neno maendeleo, ama sivyo, kuna miti ya mbao, viazi mviringo, sidhani hapa kuna Mbunge asiyeijua Njombe. Kama huijui nenda kasome ramani na ukasome uzalishaji wa mazao kama viazi na miti katika nchi hii uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile muda hauruhusu, ningependa kusema tu kwamba kwa pamoja tushirikiane tusibweteke. Mafanikio haya, yawe ni kichocheo cha kutufanya tufanye mambo makubwa zaidi na kama kuna matatizo kama wanavyojaribu kusisitiza baadhi ya watu, sidhani kwamba kuna maeneo yasiyo na matatizo, maendeleo hayana mwisho na matatizo hayana mwisho, yanabadili sura tu kutoka sura moja kwenda sura nyingine, vinginevyo maendeleo bila matatizo au dunia bila matatizo labda ni Mbinguni tu baada ya kufa. Kwa hiyo, ninachozungumzia hapa ni kiwango cha maendeleo na kiwango cha kutatua matatizo ya watu kwamba kuna Serikali itashika madaraka ikaondoa matatizo yote, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, niseme tu kwamba imani huzaa imani na kushukuru ni kuomba tena. Kwa hiyo, wananchi wa Njombe tunaomba tudumishe umoja wetu kwa lengo la kuongeza kasi zaidi kwa sababu misingi tumeiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa muhtasari, nitoe ushauri na mapendekezo yafuatayo. Moja. Tunaomba mji mdogo wa Makambako ambao ndiyo mji unaokuwa kwa kasi kubwa kuliko mji wowote Kusini mwa Reli ya Kati, upewe hadhi ya Mji Kamili, vinginevyo matatizo yatazidi kuongezeka mpaka mtakapokuja kuitikia wito, hali itakuwa ngumu zaidi. Taratibu zote zimefuatwa, mimi pamoja na viongozi wetu tumefika kwenye ofisi ya TAMISEMI mara kwa mara, tulidhani mambo kama haya hayahitaji tena mjadala lakini kama kuna sababu za kimsingi basi tuko tayari kuelezwa tuitimize ili kusudi tukidhi nia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napendekeza kwamba kutokana na hali ya mbolea ilivyo, tuongeze zile stakabadhi za mbolea ya ruzuku katika Mikoa ile kwa lengo la kuifanya nchi hii isiwe na wasiwasi katika suala la chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nina ushauri kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba vijiji vyetu hivi vilitungiwa sheria mwaka 1975, baada ya pale kulikuwa na Kamishna wa Vijiji na Maendeleo Vijijini mpaka hivi sasa, vijiji ni kama havina mwenyewe. Napendekeza kwamba, Kamishna wa Vijiji, arudishwe na ikiwezekana tuunde Wizara ya Maendeleo Vijijini, kwa sababu ardhi ndiyo nguzo kuu ya uchumi wetu katika nchi hii. Kwa sasa hivi matumizi ya ardhi inaelekea tunavyopanua miji ni kuongeza njaa mijini na kuongeza umaskini. Kwa sasa hivi kwa mfano, vijiji vinajengwa kiholela holela tu na wakati mwingine kwenye ardhi nzuri. Kule Njombe kuna vijiji zaidi ya 40, vyenye ukubwa kama Mji Mdogo wa Kibaigwa, hivi sasa na Mheshimiwa Waziri Mkuu akiangalia kutoka Njombe kwenda Makete kuna vijiji zaidi ya 20, nyumba zimeungana au kutoka Makambako mpaka Njombe, vimeungana kama Konabeshe. Sasa anahitajika mtu ambaye atakuwa anasimamia shughuli hizi kila siku na kurekebisha mambo kuliko tukaachia tu kila mtu kwa sababu *everybody's business is nobody's business.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine namalizia najua muda hauniruhusu ni nyumba za Walimu. Kwa nini hili liwe ni tatizo? Kuna wakati tulijenga viwanja vya michezo katika Mikoa yote, mfano Majimaji na kila mahali kwa kutumia Wakuu wa Mikoa. Leo nyumba ya Mwalimu wa Elimu ya Msingi *is an issue*. Kwa nini tusiamue ukawa mradi wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na *centre* ikatoa mabati na saruji, kwa miaka miwili tukatatua tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Seneta Jackson Makwetta. Tunashukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji wa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, unaendelea vizuri na jioni hii tutaendelea, wale wote walioomba kuchangia ninawaomba wawepo ili wapate fursa ya kuchangia kama walivyokwishaomba.

Kwa kuwa wakati uliobaki ni mdogo sana, hautoshi kwa mchangiaji mmoja kuweza kuutumia ipasavyo, basi ninaomba nichukue fursa hii, kusitisha shughuli za Bunge hadi leo jioni, saa kumi na moja kamili.

*(Saa 6.56 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Zubeir A. Maulid) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Ahsante Waheshimiwa Wabunge, katika orodha niliyonayo kwenye Meza kwa jioni ya leo, mchangiaji wetu wa mwanzo ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Zainab Gama ajiandae. Mheshimiwa Masolwa simuoni, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka naye simuoni labda niwataje watu kama 10. Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale. Sasa kwa hapa, ninayemwona ni Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya. Sasa nampa nafasi ili aweze kutupa mchango wake, karibu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, napenda kusikitika kwamba kuna viongozi wa kisiasa ambao wamekuwa wakitumia Vitabu Vitakatifu na kuwafananisha wafuasi wa Chama cha Mapinduzi na wafuasi wa Yesu. Kwetu sisi Wakristo ambao tunamwamini Yesu Kristo, wafuasi wa kisiasa wanaongea uongo na ni wanafiki, wale ni Watakatifu, hawaongei uongo, kwa hiyo, naomba jambo hili likemewe na waache mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu tumekuwa tukilalamika kwamba maadili yanaporomoka, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu jana katika hotuba yake amesema kwamba watu wasiongee matusi katika majukwaa ya kisiasa. Ni jambo la kusikitisha, kiongozi mkubwa wa Chama cha Mapinduzi, ambaye ni Katibu Mkuu, anasimama kwenye majukwaa na kuwafananisha Wapinzani na Paka. Hili ni jambo la aibu kwa kiongozi mkubwa kufanya hivyo sijui anawafundisha maadili gani watoto wetu? Hivi watoto wenye hekima wakipita wakamwita “Mtu Mzima Hovyo”, atathubutu kusema wale watoto hawana maadili? Aliyeporomosha maadili ni nani? Kwa hiyo, tunamshukuru Waziri Mkuu, naomba azidi kukemea na aanze na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ambayo ina rasilimali nyingi, tuna maliasili ambazo hazipatikani mahali popote duniani, lakini kwa kusikitika Tanzania bado ni nchi ya 10 kutoka chini duniani kwa umaskini na umaskini umezidi kuongezeka kutoka mwaka 2001, kwa sasa hivi tuna maskini Tanzania wanaofikia zaidi ya milioni 1.2. Hili ni jambo la aibu ukizingatia Tanzania ni nchi ya tano kwa kuzalisha dhahabu. Napenda kuuliza, je, Watanzania tunafaidikaje na dhahabu ambayo inapatikana hapa Tanzania? Mtu aliyeko chini kabisa katika ngazi ya kijijini, anafaidiakaje na dhahabu yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imezidi kuwa maskini lakini vipaumbele vyetu tunavyovipanga haviendani na matakwa ya Tanzania. Katika hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, ameongeza kodi katika sigara, vinywaji vikali na vya baridi lakini tunaona Mheshimiwa Waziri wa Afya, amekuwa akielimisha watu kwamba wakivuta sigara wataugua na wakinywa pombe watapata saratani. Tukumbuke kwamba kila shilingi moja inayotumika kwenye sigara shilingi tatu inatumika kwa ajili ya kumtibu mgonjwa anayepata madhara kwa ajili ya matumizi ya sigara. Sasa ninachotaka kuiuliza Serikali, je, wananchi hawa wakipata elimu ya kutosha na wakaacha kunywa pombe na kuvuta sigara, ina maana nchi yetu itaingia katika mtikisiko mkubwa sana wa uchumi? Kwa hiyo, nafikiri ni wakati sasa Serikali iangalie ni namna gani ya kuweza kuweka vipaumbele vyake kulingana na matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia viongozi wakiwa wanasikitika nchi imezidi kuwa maskini, hata hivi majuzi tuliona kuna kiongozi ambaye alikuwa anauliza kwamba hivi Watanzania tuna nini, ametuloga nani? Hamna sababu ya kutafuta mchawi, mchawi ni Chama cha Mapinduzi ambacho kimeshindwa kabisa kupanga mipango yake vizuri na kutumia rasilimali zetu vizuri ili Watanzania waweze kufaidika nazo na hatimaye tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, kuna mchangiaji ambaye amechangia hapa asubuhi akasema tusitumie Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya CCM sio Msahafu wala sio Kitabu Kitakatifu ni ahadi walizozitoa, tutazidi kuitumia na tutazidi kuichambua. Wengi wamekuwa wakijisifia hapa kuhusu elimu kwamba wamejenga Shule za Kata nyingi, lakini zile shule zilijengwa na wananchi na sisi Wabunge wa CHADEMA tumekuwa tukizunguka Tanzania nzima katika Operesheni Sangara, wamenituma niulize wakiwa ni pamoja na wana-CCM, wana-CHADEMA na wasio na

vyama, wanataka kujua Wizara ya Elimu walichangia kiasi gani katika kujenga shule? Sio Wabunge wa CCM wanasimama tu na kusema wametekeleza Ilani, tunataka kujua pia katika hizo shule, ni vyuo vingapi vimejengwa kwa ajili ya Walimu? Ripoti ya *CAG* inaonyesha kwamba kwa sasa hivi kila Mwalimu anafundisha wanafunzi 355, lakini uwiano wa kawaida unatakiwa kuwa Mwalimu mmoja wanafunzi 54. Kwa hiyo, tunaomba Waziri atueleze ni kiasi gani wametenga kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Walimu ili shule hizo ziweze kupata Walimu na sio kutoa sifa tu hapa kwamba tumetekeleza Ilani wakati shule zenyewe zilijengwa na wananchi wote wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, naomba tu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii au Waziri Mkuu ajaribu kutoa tamko. Mimi nikiwa kama mdau wa utalii, tumekuwa tukipata maswali mengi kutoka kwa wageni kwamba Tanzania sasa hivi kuna *outbreak* ya *Dangue Fever* ambayo inaletwa na mbu na dalili zake ni homa, mafua, kupata vipele, kutapika na kadhalika. Sasa wageni wamekuwa wakielezana na wanapelekeana habari kwamba ukienda Tanzania kuna ugonjwa ambao uko Dar es Salaam na Zanzibar, kwa hiyo, wanaogopa kuja Tanzania. Tungependa Mheshimiwa Waziri atoe tamko hili ili wananchi wetu waweze kujikinga na ugonjwa huo kwa sababu ni *viral disease* na vile vile wageni waweze kuelezwa kwamba madhara yake ni mabaya kiasi gani ili waweze kuja Tanzania bila woga wowote na hii itatusaidia kwa ajili ya watalii wa nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, katika hii hii Ilani ya CCM, ukurasa wa 48, inasema itafufua viwanda mama, cha kusikitisha pale Kilimanjaro kuna kile Kiwanda cha *Mashine Tools* ambacho ni kiwanda mama na tangu nimeingia katika Bunge hili mwaka 2005, nimekuwa nikizungumzia kile kiwanda mpaka leo hakijafanyiwa kitu chochote, bado wanasema wanatafuta mwekezaji, huyu mwekezaji asipopatikana, nini kitafanyika, kile kiwanda kitazidi kubaki kama kilivyo. Hapo hapo, tunaongelea mambo ya Kilimo Kwanza, ili kuweza kuendeleza wakulima walioko vijijini, lazima tuwasaidie na viwanda vidogo vidogo. Kile Kiwanda cha *Machine Tools,* kingekuwa ndicho kiwanda ambacho kingeweza kusaidia kutengeneza viwanda vidogo vidogo. Sasa hiki Kilimo Kwanza bila kwenda na viwanda vidogo vidogo ambavyo kila kitu kitakuwa *processed* hapa nchini, je, yule mkulima kule chini ataweza kufaidika na hicho Kilimo Kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika letu la *Air Tanzania,* ni jambo la kusikitisha wakati *Air Tanzania* ikianza ilikuwa na ndege tisa, sasa hivi imebaki ndege moja. Ndege hii kwa sasa hivi ndio inazunguka kila mahali. Mimi naomba kuiuliza Wizara, ndege hii iko *due for major checkup* lini na kama ikienda kwa *major checkup,* kuna ndege ambayo imekwishaandaliwa kwa ajili ya kuli-*replace* hii ndege moja*? Air Tanzania* inatakiwa ifufuliwe. Kwa sasa hivi kuna ile ndege ya *Air Bus* iliyokuwepo imekwenda kwa *major checkup* huko Tulis, Ufaransa. Ipo kule lakini yule aliyetukodishia ndege, anadai zile Dola zake laki tatu, mia tatu ishirini na tano kila mwezi na ndege ile iko Tulis, haifanyi lolote. Sasa hivi, Shirika lile linadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 30 lakini ndege ile bado haijarudishwa kwa mwenyewe. *Air Tanzania* bado inadaiwa na ile ndege sijui kwa nini hawairudishi huko Equador, imekaa tu pale, inazidi

kutuingizia hasara, sijui Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba inafufua Shirika lile. Ni jambo zuri kweli tunatengeneza Viwanja vya Ndege, mnasema Kiwanja cha Dar es Salaam kimetengenezwa vizuri, ndiyo, Mashirika mengi yatakuja Dar es Salaam, sasa *connection* za kwenda kwenye hivi viwanja vidogo vidogo kama Kigoma, Arusha na kadhalika wataendaje? Tunategemea tu ndege moja ya *Precision Air* wakati hatuna ndege ya Taifa? Sasa hivi *Precision Air* imekuwa ni *monopoly*, ukienda *Airport* unakuta ndege imekuwa *cancelled*...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii. Kwanza, ukisikia paka anapiga kelele na anakukwangua makucha, ujue amekanyagwa mkia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa kuchangia kuhusu Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza kimeletwa ili wananchi wapate manufaa, Serikali ipate maendeleo na kila mmoja katika nchi hii ya Tanzania apate manufaa lakini Kilimo Kwanza kimekuwa sivyo hivyo, nitasema kwa nini? Mimi tangu niingie Bunge hili inapata miaka mitano sasa tunamalizia, kilio chetu cha watu wa Kilwa, ni kuhusu mazao yao hasa ufuta lakini suala hili bado halijatatuliwa. Mara nyingi wafanyabiashara wanakuja kununua ufuta kwa bei kubwa zaidi ya Chama cha Ushirika, lakini Chama cha Ushirika au Vyama vya Msingi, vinataka kununua kwa bei ya chini. Mwaka huu, ufuta, Chama cha Ushirika kinataka kununua kwa shilingi 700/= wakati wafanyabiashara wananunua ufuta kwa shilingi 1,300/= na imekuwa si ruhusa mfanyabiashara kununua. Sasa hiki Kilimo Kwanza ni kwa ajili ya nani? Ninapenda kujua Kilimo Kwanza hiki ni kwa ajili ya nani, ni kunufaisha Taifa au Serikali peke yake wakati wananchi wanaolima zao lile hawanufaiki? Napenda suala hili liangaliwe, limekuwa ni tatizo na kero kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi hususan Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumapili ya tarehe 5, wananchi wa Kilwa walifanya maandamano ku-*protest* suala hili la kununua ufuta kwa shilingi 700/= ili wauze ufuta wao kwa shilingi 1,300/=. Nasikitika kusema kwamba, kuna viongozi ambao hawako kwa ajili ya wananchi, wako kwa ajili ya maslahi yao. Nitatoa mfano, kuna kiongozi mmoja ambaye amempigia simu Waziri wa Kilimo na kumwambia, wale wamefanya maandamano kwa ajili ya mimi Mbunge ambaye nanunua Kilwa na kwa ajili ya Mwenyekiti wa CUF, kitu ambacho sio kweli. Mimi sio mfanyabiashara na sinunui ufuta. Utani wa kuchomekeana kwenye maslahi ya wananchi uwe mwisho. Haya ni maslahi ya wananchi. Kama ni mwana-CCM basi mimi namwita mwana-CCM huyo CCM maslahi, hayuko kwa ajili ya wananchi kwa sababu anatakiwa aseme jambo ambalo lina ukweli. Nasikitika sana na naomba Serikali iwaangalie wananchi wa Mikoa hii juu ya ufuta huo. Hivi kweli inaingia akilini shilingi 700/= na shilingi 1,300/=?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea sehemu ya pili, ninapenda kuuliza, nini faida ya kuwepo Mwanasheria wa Serikali katika Halmashauri zetu. Mimi nilifikiria Mwanasheria wa Serikali, ndio mwongozo wa Halmashauri zetu pale tunapopotoka, lakini ni tofauti na Halmashauri nyingine. Mfano, Halmashauri ya Kilwa tuna Mwanasheria lakini si Mwanasheria kwa sababu hafanyi kazi zile zinazomhusu. Jambo lolote la kisheria yeye anaogopa kulitatua na akisindikizwa na wanasiasa kwamba hili lipotoshe hivi, nafikiri anakwenda hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mmoja wa mji mdogo ulioanzishwa Wilaya ya Kilwa, Kilwa Masoko, wameingizwa wajumbe ambao hawana sifa ya kuwa wajumbe. Ni jambo la kusikitisha wajumbe hawa, mmoja ni mfungwa, amefungwa japokuwa hajawekwa ndani ya jela, lakini amekuwa mjumbe wa Halmashauri na mwongozo wa sheria unasema kwamba wajumbe wa Mji Mdogo wanatakiwa wawe wajumbe wa Halmashauri, wajumbe hawa ambao wamewekwa sio wajumbe wa Halmashauri. Wakati wa kujibu hoja zetu, nataka nipate jibu kuhusu wajumbe hawa, mmoja wakati anateuliwa amefungwa. Mwanasheria anasema yeye hawezi kulitatua suala hili, kama mnataka nendeni Mahakamani.

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mwanawetu, amefungwa yaani yuko jela, amechukuliwa jela kuja...

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba hayuko jela lakini ana hukumu ya kifungo.

**MWENYEKITI:** Hajafungwa huyo.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Alihukumiwa kufungwa au kulipa faini na amelipa faini, kwa hiyo, yuko hatiani.

**MWENYEKITI:** Sio kifungo hicho.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Ahaa! Kama asingelipa faini angefungwa.

**MWENYEKITI:** Naomba uendelee.

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Wanasheria walioko kwenye Halmashauri za Wilaya…

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa Blandes!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Kanuni ya 68.

**WABUNGE FULANI:** Soma inasemaje?

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Mbunge anaendelea kuchangia, amezungumza maneno ambayo yanamshutumu kwa kiasi kikubwa Mwanasheria, nadhani wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na shutuma hizo ni nzito sana ambazo tukiziruhusu bila ya kumpatia nafasi Mwanasheria wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, ni kinyume kabisa na taratibu na tutakuwa hatujamtendea haki, asihukumiwe wakati hawezi kupata nafasi ya kuja kujitetea humu ndani, naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nimekusikia, nadhani pana tatizo la Kiswahili kidogo hapa. Huyu mchangiaji nadhani hawezi kutofautisha baina ya mtu aliyehukumiwa kifungo na mtu aliyeambiwa atoe faini. Hili ndilo tatizo alilonalo Mheshimiwa. Kwa hiyo, nafikiri tumemwelewa kwamba yule mtu ametozwa faini na ukitozwa faini hujafungwa. Kufungwa ni jela. Kwa hiyo ni Kiswahili tu kinamsumbua nafikiri aendelee tu, namruhusu amalizie kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba dakika zangu ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina suala lingine linahusu *TASAF*. Tunashukuru kwamba *TASAF* imetuendeleza katika Wilaya ya Kilwa na Mkoa mzima wa Lindi lakini kuna kitendo ambacho kimetokea mwezi Desemba, bado mimi kinanishangaza na nataka nikieleze hapa. Mwezi Desemba, kuna vijiji nane ambavyo vilipata fedha za *TASAF* baada ya kuibua miradi yao lakini baadaye wakaambiwa kwamba fedha zile zirudishwe, zipelekwe kwenye akaunti kwamba zimekosewa, mimi nashangaa wanakosea vipi akaunti mpaka majina ya vile vikundi? Fedha hizo zimerudishwa kwenye akaunti, yaani wanazichukua wao wenyewe wana kikundi halafu baadaye wanazirudisha kwao, hadi leo ninavyozungumza yule aliyeamrisha zirudishwe, zimekosewa, bado hajazitoa kwenye hiyo akaunti na vile vile licha ya kuzitoa kwenye ile akaunti vile vile bado hajatueleza vikundi hivyo kama vilikosewa hizi fedha ni za vikundi gani? Napenda hili suala lifuatiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Siku zote nimekuwa nikiimba wimbo huu kwamba Halmashauri ya Kilwa si maskini, ina kila kitu. Pamoja na kwamba Halmashauri hii ina kila kitu lakini hali sio nzuri, nafikiri fedha zinaingia mifukoni tu. Kuna wengine makusanyo na vyanzo vya mapato wanavijua wao binafsi, wafanyakazi wa eneo la Uhasibu, si vitu ambavyo viko wazi, kuna vijiji ambavyo vimeomba kukusanya ushuru lakini vijiji hivyo vimekuwa vikikusanya ushuru zaidi ya makisio. Hapo awali, watu wengine walikuwa wanakusanya ambao ni wakala, walikuwa wanakusanya chini ya kiwango ambacho kimekisiwa. Lakini cha kushangaza, sasa kwa sababu Halmashauri haipati nafasi ya kuzipata zile pesa, basi wanataka vile vijiji ambavyo vinakusanya juu ya kiwango ziache kukusanya, wakusanye wakala kwa sababu wao wanao uwezo wa kuwaamrisha vyovyote ili pesa ziingie

mfukoni mwao. Nazungumzia hili lakini kuna mengi zaidi lakini nataka Serikali kwa kupitia TAMISEMI iende ikaangalie Halmashauri ya Kilwa. Halmashauri ya Kilwa, ni mbovu mno, akaiangaliwe. Kuna mapato mengi lakini mapato haya hayafiki Serikalini, yanaingia mifukoni mwa watu. Hilo ndiyo ombi langu kwenye Halmashauri ya Kilwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana, nadhani Mheshimiwa Waziri amesikia na Mbunge mwenzio wa Kilwa namwona na yeye yumo, naye kakusikia vilevile.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia machache yale ambayo ninayo lakini nianze kwa kusema tu kwamba, naunga mkono hoja kwa ujumla. Lakini hapo hapo, naomba niipongeze Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Hotuba ya Wizara ya TAMISEMI na wote ambao wamehusika katika kuandaa hotuba hiyo, kwa kweli ilikuwa ni hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kidogo katika kuchangia kuhusu mambo ya mashamba, naomba nianzie na Ilungu. Katika Jimbo langu la Mbeya Vijijini, kuna sehemu ambayo *TANAPA* ilichukua na ilipochukua maeneo yale, wale watu hadi leo hawajapata mafanikio ya kulipwa fedha zao. Ni miaka miwili imepita na kumekuwa na malalamiko makubwa sana hasa kwa sababu kwanza, hawana maeneo ya kulima na pili hawana maeneo ya kuchungia ng'ombe na wamejaribu kufuatilia lakini mafanikio hakuna. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iwafikirie kuwalipa hao watu haraka sana kwa sababu hawana maeneo ya kulima na kama wangelipwa bila shaka wangeweza kununua au wangeenda mahali kokote kule wakahamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kibaya zaidi ni kwamba kuna maeneo ambayo yametengwa na kuwa hifadhi ya kawaida lakini eneo hili lilikuwa ni eneo ambalo wananchi wale wenyeji walikuwa wanachungia mifugo yao pale na kila wakati wamekuwa wakikamatwa hasa wanapokwenda kuchunga mifugo yao na baada ya kukamatwa wanalipishwa hela zaidi. Kwa mfano, anaweza akalipishwa laki moja lakini akaandikiwa hela kidogo labda shilingi 30,000/- au shilingi 40,000/-. Ninaiomba Serikali ijaribu kufuatilia suala hilo. Nimejaribu kuongea na Waziri akasema kwamba anafuatilia, lakini naomba nitoe tamko leo kwamba naomba Serikali kwa bidii zote iweze kufuatilia suala hili kwa sababu wananchi wamejaribu kufuatilia kwa *DC* na mahali kwingine lakini juhudi zao zimeshindikana. Naomba hilo suala lifuatiliwe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, ninaomba mashamba yale ya *Tanganyika Packers,* najua pale kile Kiwanda cha Nyama kimejengwa miaka ya 1970 na mpaka leo kiwanda kipo lakini hakifanyi kazi, sasa hivi yamebakia kuwa magofu. Lakini kuna maeneo ambayo wananchi wanalima pale na wanalima kwa kutozwa hela. Naiomba Serikali kama inawezekana kwa sababu kiwanda bado hakijaanza na kama baadaye watakifufua basi hawa wananchi wanyang'anywe haya mashamba lakini kwa wakati huu naiomba Serikali kama inawezekana wapewe maeneo ya kulima bila kutozwa hela.

Waorodheshwe majina yao, walime pale mpaka hapo Serikali itakaposema kwamba sasa kiwanda kinafufuliwa, ndipo wanyang'anywe hayo maeneo. Lakini sasa hivi kumekuwa na kero kubwa, wanaenda kule wananyanyaswa. Naiomba Serikali kwa hilo pia ilifikirie. Hilo ni eneo la *Mbalizi Tanganyika Packers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo limenisumbua sana na wananchi wamekuwa wakinipigia simu kila wakati lilikuwa ni eneo la Chuo cha Ufundi cha Mbeya *(MIST).* Eneo hili lilikuwa limechukuliwa miaka mingi ya nyuma na kwa kweli wameendelea nalo lakini juzi juzi imejitokeza kwamba wanataka kuchukua eneo lingine katika eneo la Iyunga. Lakini kile Chuo cha *MIST* kiko katikati ya Mbeya Mjini na Mbeya Vijijini, sasa inaelekea ni kama *MIST* inataka kuchukua eneo kubwa zaidi kuliko lile ambalo lilikuwa limeshachukuliwa. Sasa wananchi wamekuwa na malalamiko makubwa sana kwamba hata yale maeneo ambayo walikuwa wameyakodisha wanalima sasa wanataka kuchukua maeneo mengine, waweze kutukodishia tena mashamba yetu. Kwa hiyo, ninaomba pia Serikali ingelifuatilia suala hili ione kwamba ukweli uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, Serikali ilikuwa imeahidi kwamba itatekeleza ahadi yake ya kuendeleza mradi wa maji pale Iwindi, Igale na maeneo ya Songwe lakini naona hatua za Mkandarasi zinachukua muda mrefu kiasi ambacho ahadi ilikuwa kabla ya uchaguzi wangeanza kufungiwa maji lakini mpaka leo hii wala hakuna dalili kwamba kutakuwa na maji yanakwenda pale. Hapa Mheshimiwa Waziri wa Maji, aliniahidi sana akasema Wizara yake itakuwa ni ya kwanza kupewa hela na *World Bank* kwa ajili ya kuendeleza mradi huo wa maji lakini mpaka sasa hivi sioni kama kuna matunda yoyote. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ijaribu kuangalia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ambalo nataka kuliongelea ni kuhusu fidia ya kahawa. Kulikuwa na fidia ambayo walilipwa mwaka jana kwa kahawa ambayo ilikuwa ni ya mwaka 1995 pamoja na pamba. Ni kweli, naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua kwa kufidia wale watu lakini kulikuwa na upungufu mwingi sana. Naiomba Serikali kama inawezekana pia kwa haraka haraka ijaribu kufuatilia suala hili na kuona kama, je, kuna uwezekano wa kufanya uhakiki ili wale ambao kwa kweli walipaswa walipwe na wao walipwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano, ni kuhusu barabara ya Ilembo. Barabara hii ya Ilembo wakati Rais amekuja kutembelea kule, aliahidi kwamba barabara hii ni vizuri ikafanya kazi kwa wakati wa kiangazi na wakati wa masika. Kidogo mwaka huu imetusumbua lakini pamoja na hayo nimejitahidi kufuatilia *TANROAD* Dar es Salaam na kwa kweli wamejitahidi kutoa hela kwa ajili ya kutengeneza maeneo ambayo ni korofi lakini ninaomba kwa sababu barabara hii ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa kule, kule wanalima sana mahindi, kule kuna *dry farming* na ni mahali ambako ni kuzuri sana kwa kilimo lakini barabara isipopitika inakuwa shida. Nimeenda mahali kuna watu wana mazao yao, wanashindwa kupeleka mazao yao kwenye masoko kwa sababu barabara hakuna. Ninaiomba Serikali pia ijaribu kuangalia na hasa barabara zile za kwenda vijijini. Kwa hiyo, ninaomba kwamba hili nalo liangaliwe na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba lazima itapitika wakati wote lakini imenisumbua sana kufuatilia hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sita, Mbeya vijijini ni wakulima wazuri wa mahindi lakini mwaka huu tunaishukuru Serikali ilitusaidia lakini bahati mbaya kama nilivyosema maeneo mengi ya Mbeya Vijijini hasa kule Nyanda za Juu, Tarafa ya Isangati, maeneo yale wanalima mahindi mwezi huu wa sita na wa saba. Kwa maana hiyo wangepaswa waanze kupewa mbolea mapema sasa ile mbolea ya msimu wa kawaida inachelewa na inakuta mahindi yameshakuwa tayari. Naomba kama inawezekana, Serikali ijaribu kutafiti na kuona ni namna gani mbolea inaweza kupelekwa kule kwa wakati muafaka. Ninaomba hilo lifuatiliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la saba, ninaomba kama tulivyosema au kama ilivyo kauli mbiu ya Serikali kwamba Kilimo Kwanza, naiomba Serikali, hili suala la kilimo cha umwagiliaji lingekuwa ni muhimu sana. Labda Serikali ingejaribu kubainisha maeneo yote yale ambayo yanafaa kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kama pengine mradi huo hauwezi kutekelezwa sasa hivi lakini ibainishe tujue kwamba ni wapi na wapi na ndipo baadaye kazi ianze kufanyika. Ninaomba maeneo hayo yabainishwe na itasaidia sana kujua kwamba ni wapi Serikali itaweza kutekeleza miradi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na ni kweli watu wanaweza kusema na kulaumu lakini kwa ujumla watu wanafahamu ni nini ambacho kimefanyika, Serikali imefanya mambo mengi sana na mimi kwangu nashukuru kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo kwa kweli Serikali imenisaidia. Kila nilipoenda kufuatilia, nimeona Serikali yangu ni sikivu kabisa, wamejitahidi kwa kila hatua kuhakikisha kwamba wananisaidia na maeneo yale niliyoomba wameweza kunipatia hela na kufanya kazi ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, naishukuru Serikali, kwa Wizara ya Nishati kwa mpango wake wa kupeleka umeme kule Ilembo. Naamini kabla ya uchaguzi bila shaka umeme utakuwa umefika kule. Hapo sina budi kumshukuru Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Serikali kwa ujumla hasa kwa juhudi zake na kazi nzuri ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yote kwa ujumla, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushuruku. Kipekee namshukuru Mwenyezi Mungu, ametupa tena uhai, tunaweza kujadili mambo ya maendeleo katika nchi yetu. Nitakuwa sijajibu haja ya nafasi yangu, kama sitawashukuru wanawake wa Kilimanjaro walionifikisha hapa Bungeni kwa kunichagua niwatete. Nawashukuru sana na ninawaambia kwamba bado nipo pamoja nao na nitaendelea kutetea yote yale yanayotuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie maeneo mawili tu. Lile la Kilimo Kwanza na lile la Ujasiliamali. Katika Kilimo Kwanza, tumeelezwa kwamba kuna nguzo kumi za Kilimo Kwanza. Nguzo hizo zikiwa ni Dira ya Taifa ya Kilimo, kugharamia Kilimo Kwanza, Muudo mpya wa taasisi kwa ajili ya usimamizi wa Kilimo Kwanza, mabadiliko ya mfumo wa kimkakati wa Kilimo Kwanza, ardhi kwa ajili ya

Kilimo Kwanza, vivutio kwa ajili ya Kilimo Kwanza, viwanda kwa ajili ya Kilimo Kwanza, Sayansi, Teknolojia na rasilimali watu kwa ajili ya Kilimo Kwanza, miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza na ile ya kumi ambayo nitaizungumzia ni uhamasishaji wa Watanzania kwa ajili ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji wa Watanzania katika Kilimo Kwanza, ni jambo ambalo mimi linanisumbua na hasa ninapoangalia Mkoa wangu wa Kilimanjaro kwa ujumla. Wengi wa wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro, ni wakulima wadogo wadogo ambao kwa kweli wanavishamba vidogo au wana maeneo ambayo tunaita vihamba. Ukimkuta mwenye kihamba kikubwa sana labda ni heka tano, lakini vingi ni eka moja na nusu, eka mbili mpaka eka tatu. Hapo wanajipatia chakula cha kutosha na pia unakuta wakati mwingine wana eneo la eka moja mbali na pale nyumbani kwa ajili ya kulima mahindi. Hao wanaolima mahindi, Serikali imewaona na imetoa ruzuku na vocha kwa ajili ya kuendeleza kilimo hiki ambacho ni kilimo cha msimu. Sina tatizo na hilo na naomba nichukue fursa hii, niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeona umuhimu wa kutoa vocha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kuna tatizo la vocha hizi, kupata mbolea kwa wakati ule inapotakiwa. Kamati zile za kugawa vocha au kugawa mbejeo, ziko vizuri lakini pembejeo hizi haziko karibu na wananchi ambapo akishapata mara moja anakwenda kupata vocha hiyo na kupatiwa mbolea. Hapo anatakiwa afunge safiri, afuate mbolea hiyo mbali na pale alipo. Je, Serikali imejipanga vipi kuona kwamba wananchi wanapata pembejeo hizo karibu zaidi na majumbani mwao? Najua kuna watu ambao ni ma-*agent* wamejipanga lakini nataka ifahamike kwamba ma-*agent* hawa hawako karibu na maeneo yale. Napendekeza endapo inawezekana yajengwe maghala karibu na mashamba au karibu na maeneo ambayo wananchi hawa wanaweza wakapata pembejeo hizo ili wasiingie gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudi sasa kwa uelewa wa wananchi wetu na hamasa ya kufanya kilimo kiwe kizuri zaidi, ni muda sasa tumekuwa tukizungumzia kuboresha mashamba na tumezungumzia sana Maafisa Ugani lakini mimi pekee nimejiuliza endapo watu hawa wanapenda hasa na wanajisikia kulima kilimo cha kisasa na wenyewe wakahamasika, hivi kweli wangechukua vocha wakauza? Ni wazi kwamba hawajapata elimu ya kutosha. Ninaiomba Serikali iweze kuweka msisitizo katika kuelimisha wananchi wake walio vijijini kuhusu umuhimu wa pembejeo na kuhusu umuhimu wa Kilimo Kwanza ili mashamba haya yaweze kuboreshwa na pia waweze kupata ziada ambayo wataweza kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitokako mimi, kilimo cha pamoja ni kilimo kilichotawala sana. Utakuta migomba inalimwa pamoja na kahawa. Sasa wakati ambapo mkulima anaachia shamba lile linakuwa kichaka cha migomba basi hata ile kahawa haipati mwanga wa kutosha ili iweze kushamiri. Nashukuru kwamba Serikali imeona umuhimu wa kutoa mbegu mpya ya kahawa na *TACRI* inajitahidi. Lakini wakati zao hilo linaoteshwa kule kule katikati ya migomba haichukui muda baada ya miaka mitatu miche ile inazoofu na hatuoni matokeo yake. Ninaomba sasa hapa Maafisa Ugani waweze

kuona namna ambavyo watasaidia na kuonesha katika yale mashamba darasa kwamba migomba ile kusogelea kahawa ni kitu ambacho si endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hiyo, ninaomba sasa nizungumzie kilimo cha umwagiliaji. Mwaka huu tumepata mvua za kutosha na wakati ule wa mvua, mifereji na mito yote ilikuwa inatiririka maji lakini baada ya muda sasa ni kiangazi, yote itakauka. Ninaomba wakati najibiwa mchango wangu, nielezwe tu ni mabwawa mangapi yamejengwa ya kukinga maji yale ambayo yalikuwa yanatiririka kwa wingi sana badala ya kwenda baharini na baadaye tukaanza kulalamika, ni ukame. Jambo hili ninaomba liwe endelevu angalau kwa Mikoa ile ambayo inapata mvua kwa msimu, tuweze kuwa na mpangilio kwa kupanga kwamba tutajenga mabwawa mangapi kwa mwaka ili wakati wa mvua hizo zitakapokauka tuwe sasa na maji ambayo yako kwa ajili ya kumwagilia mashamba yetu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba basi wakati ambapo tunazungumzia wajasiliamali au elimu kwa wajasiliamali kama alivyoiweka Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ule ukurasa wa 27 na 28 na hapa naomba kunukuu, inasema:-

“*Elimu ya ujasiriamali itatolewa kikamilifu ili kuongeza ushiriki wa wajasiriamali wadogo katika kukuza uchumi*.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba wanawake wangu wa Kilimanjaro, ni kati ya hao wajasiliamali wadogo, kwa hiyo, ninaomba endapo kama Serikali itaona ni vyema, iwe pia na mpango wa kuwasiliana na sekta binafsi kutoa elimu hiyo ya wajasiliamali kwa akina mama hawa ambao wanakiu sana ya elimu. Wabunge wa Viti Maalum katika Mikoa yote, wamekuwa nyakati zote wanakwenda kugonga hodi kuomba elimu kwenye Benki zetu, kwenye viwanda lakini huwa mafanikio ni madogo kwani jambo hili linaonekana kwamba labda ni hisia au ni pendekezo tu la kiongozi huyu wa akina mama. Ninaomba kama itawezekana basi watu hawa ambao wanafanya shughuli kwa kutumia mazao hayo kwa mfano kule Kilimanjaro tuna ndizi kwa wingi, kuna watu wenye viwanda vya *Banana Wine* ambao hawako pale Kilimanjaro wako Arusha, watu kama hawa washirikishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

Kuna Vijiji ambavyo vimeomba kukusanya ushuru lakini Vijiji hivyo vimekuwa vikikusanya ushuru zaidi ya makisio. Hapo awali watu wengine walikuwa wanakusanya ambao ni wakala ambao walikuwa wanakusanya chini ya kiwango ambacho kimekisiwa. Lakini cha kushangaza sasa kwa sababu Halmashauri hazipati nafasi ya kuzipata zile pesa, basi wanataka vile Vijiji ambavyo vinakusanya juu ya kiwango viache kukusanya wakusanye wakala kwa sababu wao wanao uwezo wa kuwaamrisha vyovyote ili pesa ziingie mfukoni mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia hii lakini kuna mengi zaidi. Lakini nataka Serikali kwa kupitia TAMISEMI iende ikaangalie Halmashauri ya Kilwa. Halmashauri ya Kilwa ni mbovu mno ikaangaliwe. Kuna mapato mengi, lakini mapato

haya hayafiki Serikalini, yanaingia mifukoni mwa watu. Hilo ndilo ombi langu kwenye Halmashauri ya Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Waziri amesikia na Mbunge mwenzio wa Kilwa namwona na yeye yumo naye kakusikia vile vile.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia machache yale ambayo ninayo. Lakini nianze kwa kusema tu kwamba naunga mkono hoja kwa ujumla. Lakini hapo hapo naomba niipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pamoja na Hotuba ya Wizara ya TAMISEMI na wote ambao wamehusika katika kuandaa hotuba hiyo kwa kweli ilikuwa ni hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kidogo katika kuchangia kuhusu mambo ya mashamba. Naomba nianzie na Ilungu. Katika Jimbo langu la Mbeya vijijini kuna sehemu ambayo *TANAPA* ilichukua na ilipochukua maeneo yale wale watu walikuwa hawajapata mafanikio ya kulipwa fedha zao leo hii. Ni miaka miwili imepita na kumekuwa na malalamiko makubwa sana hasa kwa sababu kwanza hawana maeneo ya kulima na pili maeneo ya kuchungia ng’ombe hawana na wamejaribu kufuatilia, lakini mafanikio hayo hakuna.

Kwa hiyo, ninaiomba Serikali iwafikirie kuwalipa hao watu haraka sana kwa sababu hawana maeneo ya kulima na kama wangelipwa bila shaka wangeweza kununua au wangeenda mahali kokote kule wakahamia. Lakini kibaya zaidi ni kwamba kuna maeneo ambayo yametengwa na kuwa hifadhi ya kawaida. Lakini eneo hili lilikuwa ni eneo ambalo wananchi wale wenyeji walikuwa wanachungia mifugo yao pale na kila wakati wamekuwa wakikamatwa hasa wanapokwenda kuchunga mifugo yao na baada ya kukamatwa wamelipishwa hela zaidi. Kwa mfano, anaweza akalipishwa laki moja, lakini akaandikiwa hela kidogo labda Sh. 30,000/= au Sh. 40,000/=. Ninaiomba Serikali ijaribu kufuatilia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuongea na Waziri akasema kwamba anafuatilia. Lakini naomba na nitoe tamko leo kwamba naomba Serikali kwa bidii zote iweze kufuatilia suala hili kwa sababu wananchi wamejaribu kufuatilia kwa *DC* na mahali kwingine lakini juhudi zao zimeshindikana. Naomba hilo suala lifuatiliwe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, naomba mashamba yale ya *Tanganyika Packers* najua pale kile kiwanda cha nyama kimejengwa miaka ya 1970 na mpaka leo kiwanda kipo, lakini hakifanyi kazi. Walijenga na sasa hivi imebakia kuwa magofu. Lakini kuna maeneo ambayo wananchi wanalima pale na wanalima kwa kutozwa hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naiomba Serikali kama inawezekana kwa sababu kiwanda bado na kama kiwanda baadaye watakifufua basi hawa wananchi

wanyang'anywe haya mashamba. Lakini kwa wakati huu nilikuwa naiomba Serikali kama inawezekana wapewe maeneo ya kulima bila kutozwa hela. Waorodheshwe majina yao walime pale mpaka hapo Serikali itakaposema kwamba sasa kiwanda kinafufuliwa ndipo wanyang'anywe hayo maeneo. Lakini sasa hivi kumekuwa na kero kubwa wanakwenda kule wananyanyaswa. Nilikuwa naiomba Serikali kwa hilo pia ilifikirie. Hilo ni eneo la Mbalizi *Tanganyika Parckers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ambalo limenisumbua sana na wananchi wamekuwa wakinipigia simu kila wakati lilikuwa ni eneo la Chuo cha Ufundi cha Mbeya *(MIST)*. Eneo hili lilikuwa limechukuliwa miaka mingi ya nyuma na kwa kweli wameendelea nalo, lakini juzi juzi hasa imejitokeza kwamba wanataka kuchukua eneo lingine katika eneo la Iyunga. Lakini kile Chuo cha *MIST* kiko katikati ya Mbeya Mjini na Mbeya Vijijini. Sasa inaelekea kwamba ni kama *MIST* inataka kuchukua eneo kubwa zaidi kuliko lile ambalo lilikuwa limeshachukua.

Sasa wananchi wamekuwa na malalamiko makubwa sana kwamba hata yale maeneo ambayo walikuwa wameyakodisha wanalima, sasa wanataka kuchukua maeneo mengine waweze kutukodishia tena mashamba yetu. Kwa hiyo, ninaomba pia Serikali ingelifuatilia suala hili ione kwamba ukweli uko wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ilikuwa imeahidi kwamba itatekeleza ahadi yake ya kuendeleza mradi wa maji pale Iwindi, Igale na maeneo ya Songwe. Lakini naona hatua za mkandarasi zinachukua muda mrefu kiasi ambacho ahadi ilikuwa kabla ya uchaguzi wangeaza kufungiwa maji, lakini mpaka leo hii wala hakuna dalili kwamba kutakuwa na maji yanakwenda pale. Hapa Mheshimiwa Waziri wa Maji aliniahidi sana akasema Wizara yake itakuwa ni ya kwanza kupewa hela na *World Bank* kwa ajili ya kuendeleza mradi huo wa maji. Lakini mpaka sasa hivi sioni kama kuna matunda yoyote. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali ijaribu kuangalia suala hili.

Lakini lingine ambalo nilitaka kuongelea ni kuhusu fidia ya kahawa. Kulikuwa na fidia ambayo walilipwa mwaka jana, kahawa ambayo ilikuwa ni ya mwaka 1995 pamoja na pamba. Naishukuru Serikali kwa kuchukua hatua kwa kuifidia wale watu. Lakini kulikuwa na mapungufu mengi sana. Nilikuwa naiomba Serikali kama inawezekana pia kwa haraka haraka ijaribu kufuatilia suala hili na kuona kwamba: Je, kuna uwezekano wa kufanya uhakiki ili wale ambao kwa kweli walipaswa walipwe na wao walipwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu barabara ya Ilembo. Barabara hii ya Ilembo wakati Rais amekuja kutembelea kule aliahidi kwamba barabara hii ikafanya kazi kwa wakati wa kiangazi na wakati wa mvua. Kidogo mwaka huu umetusumbua, lakini pamoja na hayo nimejitahidi kufuatilia *TANROAD* Dar es Salaam na kwa kweli wamejitahidi kutoa hela kwa ajili ya kutengeneza maeneo ambayo ni korofi.

Lakini ninaomba, barabara hii ni barabara ni muhimu sana kwa uchumi wa kule mahali. Kule wanalima sana mahindi, kuna *dry farming* na ni mahali ambako ni kuzuri sana kwa kilimo, lakini barabara isipopitika na nimekwenda mahali kuna watu wana mazao yao wanashindwa kupeleka mazao kwa sababu barabara hakuna.

Ninaiomba Serikali pia ijaribu kuangalia na hasa barabara zile za kwenda Vijijini. Kwa hiyo, ninaomba kwamba hili nalo liangaliwe na Mheshimiwa Rais aliahidi kwamba lazima itapitika wakati wote. Lakini imenisumbua sana kuhakikisha kufuatilia hapa na pale. Lakini Mbeya Vijijini ni wakulima wazuri wa mahindi lakini mwaka huu tunaishukuru Serikali ilitusaidia lakini bahati mbaya kama nilivyosema maeneo mengi ya Mbeya Vijijini hasa kule nyanda za juu hasa kule Tarafa ya Isangati maeneo yale wanalima mahindi mwezi huu wa Sita na wa Saba. Kwa maana hiyo, wangepaswa waanze kupewa mbolea mapema.

Sasa ile mbolea ya msimu wa kawaida inachelewa na inakuta mahindi yameshakuwa tayari. Nilikuwa naomba kama inawezekana Serikali ijaribu kutafiti na kuona ni namna gani mbolea inaweza kupelekwa mahali kule kwa wakati muafaka. Ninaomba hilo liweze kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni la mwisho, ninaomba kama tulivyosema au kama ilivyo kauli mbiu ya Serikali kwamba Kilimo Kwanza, naiomba Serikali kwamba hili suala la kilimo cha umwagiliaji kingekuwa ni muhimu sana. Labda Serikali ingejaribu kubainisha maeneo yote yale ambayo yanafaa kabisa kwa kilimo cha umwagiliaji. Hasa kama pengine mradi huo hauwezi kutekelezwa sasa hivi, lakini ibainishe tujue kwamba ni wapi na wapi na ndipo baadaye kazi ianze kufanyika. Ninaomba maeneo hayo yabainishwe na itasaidia sana kujua kwamba ni wapi Serikali itaweza kutekeleza miradi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na ni kweli watu wanaweza kusema na kulaumu lakini kwa ujumla watu wanafahamu ni nini ambacho kimefanyika. Serikali imefanya mambo mengi sana na mimi kwangu nashukuru kwa sababu kuna maeneo mengi ambayo kwa kweli Serikali imenisaidia.

Kila nilipokwenda kufuatilia nimeona Serikali yangu ni sikivu kabisa, wamejitahidi kwa kila hatua kuhakikisha kwamba wananisaidia na maeneo yale niliyoomba wameweza kunipatia hela na kufanya kazi ile. Lakini mwisho naishukuru Serikali kwa Wizara ya Nishati kwa mpango wake wa kupeleka umeme kule Ilembo. Naamini kwamba kabla ya uchaguzi bila shaka umeme utakuwa unafika kule. Hapo sina budi kumshukuru Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Serikali kwa ujumla hasa kwa juhudi zake na kazi nzuri ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja yote kwa ujumla. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku. Kipekee, namshukuru Mwenyezi Mungu, ametupa tena uhai tunaweza kujadili mambo ya maendeleo katika nchi yetu. Nitakuwa sijajibu haja ya nafasi yangu kama sitawashukuru wanawake wa Kilimanjaro walionifikisha hapa Bungeni kwa kunichagua niwatetee.

Nawashukuru sana na ninawaambia kwamba bado nipo pamoja nao na nitaendelea kutetea yote yale yanayotuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nizungumzie maeneo mawili tu. Lile la Kilimo Kwanza na lile la Ujasiriamali. Katika Kilimo Kwanza tumeelezwa kwamba kuna nguzo kumi za Kilimo Kwanza. Nguzo hizo zikiwa ni Dira ya Taifa ya Kilimo, kugharamia Kilimo Kwanza, Muudo mpya wa Taasisi kwa ajili ya usimamizi wa Kilimo Kwanza, mabadiliko ya mfumo wa kimkakati wa Kilimo Kwanza, ardhi kwa ajili ya kilimo kwanza, vivutio kwa ajili ya Kilimo Kwanza, viwanda kwa ajili ya Kilimo Kwanza, Sayansi, Teknolojia na rasilimali watu kwa ajili ya Kilimo Kwanza, miundombinu kwa ajili ya Kilimo Kwanza na ile ya kumi ambayo nitaizungumzia ni uhamasishaji wa Watanzania kwa ajili ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhamasishaji wa Watanzania katika Kilimo Kwanza ni jambo ambalo mimi linanisumbua na hasa ninapoangalia Mkoa wangu wa Kilimanjaro kwa ujumla. Wengi wa wakulima wa Mkoa wa Kilimanjaro ni wakulima wadogo wadogo ambao kwa kweli wanavishamba vidogo au wana maeneo ambayo tunaita vihamba. Ukimkuta mwenye kihamba kikubwa sana labda ni heka tano, lakini vingi ni ekari moja na nusu, ekari mbili mpaka ekari tatu. Hapo wanajipatia chakula cha kutosha na pia unakuta kwamba wakati mwingine wana eneo la ekari moja mbali na pale nyumbani kwa ajili ya kulima mahindi.

Hao wanaolima mahindi, Serikali imewaona na imetoa ruzuku na vocha kwa ajili ya kuendeleza kilimo hiki ambacho ni kilimo cha msimu. Sina tatizo na hilo na naomba nichukue fursa hii niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeona umuhimu wa kutoa vocha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kuna tatizo la vocha hizi kupata mbolea kwa wakati ule inapotakiwa. Kamati zile za kugawa vocha au kugawa pembejeo ziko vizuri, lakini pembejeo hizi haziko karibu na wananchi ambapo wakishapata mara moja anakwenda kupata vocha hiyo na kupatiwa mbolea. Hapo anatakiwa afunge safiri afuate mbolea hiyo mbali na pale alipo. Je, Serikali imejipanga vipi kuona kwamba wananchi hapa wanapata pembejeo hizo karibu zaidi na majumbani mwao? Najua kuna watu ambao ni ma-*agent* wamejipanga, lakini nataka ifahamike kwamba ma-*agent* hawa hawako karibu na maeneo yale, nilikuwa napendekeza endapo inawezekana yajengwe maghala karibu na mashamba au karibu na maeneo ambayo wananchi hawa wanaweza wakapata pembejeo hizo ili wasiingie gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nirudi sasa kwa uelewa wa wananchi wetu na hamasa ya kufanya kilimo kiwe kizuri zaidi. Ni muda sasa tumekuwa tukizungumzia kuboresha mashamba na tumezungumzia sana Maafisa Ugani.

Lakini mimi pekee nimejiuliza, endapo watu hawa wanapenda hasa na wanajisikia kulima kilimo cha kisasa na wenyewe wakahamasika, hivi kweli wangechukua vocha wakauza ni wazi kwamba hawajapata elimu ya kutosha. Ninaiomba Serikali iweze kuweka msisitizo katika kuelimisha wananchi wake walio vijijini kuhusu

umuhimu wa pembejeo na kuhusu umuhimu wa Kilimo Kwanza ili mashamba haya yaweze kuboreshwa na pia waweze kupata ziada ambayo wataweza kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitokako mimi kilimo cha pamoja ni kilimo kilichotawala sana. Utakuta migomba inalimwa pamoja na kahawa. Sasa wakati ambapo mkulima anaachia shamba lile linakuwa kichaka cha migomba, basi hata ile kahawa haipati mwanga wa kutosha ili iweze kushamiri.

Nashukuru kwamba Serikali imeona umuhimu wa kutoa mbegu mpya ya kahawa na *TACRI* inajitahidi. Lakini wakati zao hilo linaoteshwa kule kule katikati ya migomba haichukui muda baada ya miaka mitatu miche ile inadhoofu na hatuoni matokeo yake. Ninaomba sasa hapa Maafisa Ugani waweze kuona namna ambavyo watasaidia na kuonyesha katika yale mashamba darasa kwamba migomba ile kusogelea kahawa ni kitu ambacho sio endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia hayo, ninaomba sasa nizungumzie kilimo cha umwagiliaji. Mwaka huu tumepata mvua za kutosha na wakati ule wa mvua mifereji yote na mito yote ilikuwa inatiririka maji, lakini baada ya muda sasa ni kiangazi yote itakauka. Ninaomba wakati najibiwa mchango wangu nielezwe tu ni mabwawa mangapi yamejengwa ya kukinga maji, yale ambayo yalikuwa yanatiririka kwa wingi sana badala ya kwenda baharini na baadaye tukaanza kulalamika ni ukame. Jambo hili ninaomba lile endelevu angalau kwa Mikoa ile ambayo inapata mvua kwa msimu tuweze kuwa na mpangilio kwa kupanga kwamba tutajenga mabwawa mangapi kwa mwaka ili wakati mvua hizo zitakaponyauka tuwe sasa na maji ambayo yako kwa ajli kumwagilia mashamba yetu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninaomba basi wakati ambapo tunazungumzia wajasiriamali au elimu kwa wajasiriamali kama alivyoiweka Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ule ukurasa wa 27 na 28 na hapa naomba kunukuu: “Elimu ya ujasiriamali itatolewa kikamilifu ili kuongeza ushiriki wa wajasiriamali wadogo katika kukuza uchumi.”

Naomba ieleweke kwamba wanawake wangu wa Kilimanjaro ni kati ya hao wajasiriamali wadogo. Kwa hiyo, ninaomba endapo Serikali itaona ni vyema iwe pia na mpango wa kuwasiliana na sekta binafsi kutoa elimu hiyo ya wajasiriamali akina mama hawa ambao wana kiu sana ya elimu.

Wabunge wa Viti Maalum katika Mikoa yote wamekuwa nyakati zote wanakwenda kugonga hodi kuomba elimu kwenye Benki zetu, kwenye viwanda, lakini huwa mafanikio ni madogo kwani jambo hili linaonekana kwamba labda ni hisia au ni pendekezo tu la kiongozi huyu wa akina mama. Ninaomba kama itawezekana, basi watu hawa ambao wanafanya shughuli kwa kutumia mazao hayo kwa mfano kule Kilimanjaro tuna ndizi kwa wingi, kuna watu wenye viwanda vya *Banana Wine* ambao hawako pale Kilimanjaro lakini wako Kilimanjaro. Watu kama hao washirikishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Pili, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Manaibu wake wote kwa kazi nzuri na *presentation* nzuri ya bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niruhusu kutumia nafasi hii kumpongeza sana na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri anayofanya. Lakini kwangu mimi namshukuru sana kwamba amewezesha kugawa Jimbo langu la Singida Kusini na sasa kuna majimbo mawili Singida Magharibi na Singida Mashariki. Maombi yalikuwa mengi zaidi ya 47, lakini sisi watu wa Singida Kusini tukawa miongoni mwa majimbo saba tu ambayo yamegawanywa. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mchango wake na niishukuru sana Tume ya Uchaguzi kwa kufanya kazi hiyo vizuri kwa kugawa Jimbo langu. Naishukuru Serikali, TAMISEMI kwa kugawa Vijiji na Kata, nashukuru sana mmetusaidia kurahisisha kuwaendea wananchi sasa baada ya kugawa majimbo. Baada ya kugawa Kata na kugawa Vijiji, matarajio yangu na ombi langu la siku nyingi la kuigawa Wilaya za Mkoa wa Singida na hasa Wilaya ya Singida kwa maana ya kupata Wilaya mpya ya Ikungi nategemea nayo itakuwa njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM ni sikivu, mlisikia vilivyopita kwa hakika na hii Wilaya ya Singida nayo itagawanywa kama ambavyo yamefanyika haya. Namshukuru Waziri Mkuu kwa kutembelea Mkoa wa Singida na Wilaya ya Singida Jimboni kwangu, namshukuru zaidi kwa kuniunga mkono kusaidia maendeleo katika Jimbo langu hasa Kijiji cha Msingua na Wilaya ya Sepuka ameweka chachu nzuri. Ninamshukuru sana na wananchi wamenituma nimshukuru sana kwa msaada huu ambao ameutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo, Serikali ya CCM mimi ninaishukuru sana. Mimi sidhani kama kuna mtu wa Singida atasema au atabeza mafanikio ambayo yamepatikana kwa Serikali ya CCM, sidhani! Tulikuwa na matatizo ya barabara, sasa hivi na baada pengine ya miaka miwili hivi mtu wa Singida kokote atakapokwenda ataingia kwa barabara ya lami Dodoma lami, aende Tabora lami, aende Mwanza lami, aende Mbeya lami, aende Arusha lami, yaani kokote ambako utatoka kwenda nje ya Mkoa wangu, utakwenda kwa barabara ya lami. Hawaoi kupata mambo kama haya. CCM hoyeeee! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo sisi watu wa Mkoa wa Singida tumepata hospitali ya Rufaa. Siyo kidogo hicho. Ninachoomba hapa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye mwenyewe ameona kazi ni kubwa, atuongezee. Shilingi bilioni mbili kila mwaka hazitoshi, kwa hiyo, namwomba ziendelee zaidi ili kuimaliza hospitali hiyo haraka. Shule za Sekondari zimejengwa nyingi sana. Katika Kata yangu, Kata zote 316 zina sekondari zaidi ya mbili na kuendelea. Hayo sio mafanikio makubwa? Simu za

mikononi mpaka Vijijini vitongojini kule! Sasa huyu anayebeza kuwa CCM haijafanya kitu, sijui bwana. Labda hajaoa anataka CCM wamwozeshe na tuko tayari kumwozesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie kilio changu cha muda mrefu. Kilio cha wanyama waharibifu, tembo na ndege waharibifu, ni cha muda mrefu sana. Hairuhusiwi kulia humu ndani, lakini ningeweza kulia, ningelia. Muda mrefu sana nimeeleza, kila mahali, hakuna ngazi ambayo sijafika, Mheshimiwa Rais alipokuja katika Jimbo langu mwaka jana au mwaka juzi nilimfikishia habari kuwa mzee hapa tunaumia sana kwa tembo waharibifu, usalama wa watu ni tatizo. Mazao yao ni tatizo na nimeshauri mara nyingi kuwa basi jamani angalau askari wa wanyamapori waongezwe pale kwenye Halmashauri, lakini mpaka leo hii ni wawili na Wilaya ya Singida karibu Tarafa zote zinahitaji askari wa wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linanisononesha. Limekuwa ni kero kubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu chonde chonde mimi nashindwa kujibu maswali kwa sababu sifa ya Serikali ya CCM kama nilivyosema inasikia. Sasa vipi katika hili Serikali ya CCM haijasikia? Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hili kwa kweli mazao ya watu yameharibika.

Juzi wamewahitaji askari wa wananyamapori wale wiki mbili, wiki tatu hawajapatikana kwa sababu hawatoshi. Nimemwona Waziri wa Utumishi, nimezungumza na Waziri wa Maliasili, sasa nimwambie nani zaidi ya kuwaambia viongozi hawa? Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli naomba anisaidie sana juu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege waharibifu ni hivyo hivyo Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ninamsumbua, lakini naendelea kumwomba kwamba aendelee kutusaidia. Kuhusu elimu kama nilivyosema tumefanikiwa sana. Tuna matatizo matatu. Kwanza, kuna upungufu wa walimu na upungufu mkubwa wa maabara, hatuna maabara na vilevile nyumba za walimu.

Wizara ya Elimu katika bajeti hii ni shilingi bilioni 2.045. Matumaini yangu ni kwamba Singida tutaonekana katika bajeti hii ili tupate maabara ya kutosha na ili tupate nyumba za walimu za kutosha, wengine walishapiga hatua. Sasa shule tumeshajenga tusaidiwe kupata maabara na tusaidiwe kupata nyumba za walimu ili licha ya upungufu wa walimu ili na sisi tuweze kupiga hatua juu ya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia kuanzisha *Form Five and Six* kwa kila Tarafa, sasa *Form Five* na *Six* kwa kila Tarafa kama tukianzisha kama hakuna maabara hii Elimu itakuwaje? Tunalalamika siku zote hapa kwamba wanafunzi wanaojali mambo ya sayansi ni haba au hawajitokezi hata kama wakijitokeza kama maabara hakuna haiwezekani, hawawezi wakasoma. Kwa hiyo, naomba sana katika fedha hizi ambazo zimetengwa Wizara ya Elimu Singida watuone ili tupate maabara, lakini na kuondoa tatizo la siku zote la upungufu wa nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine ambayo inatuuma na Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua tunaambiwa kuwa Singida sisi ndio Mkoa wa mwisho, yaani Mkoa masikini wa mwisho wa 21. Hili linatuuma, linatusikitisha kwa sababu sio kweli wewe ukija Singida na hata Waziri Mkuu amekuja juzi ameona kwamba maelezo yanayoelezwa kwamba ni Mkoa wa mwisho na hali halisi ilivyo kule ni tofauti kabisa. Siyo kweli huyo aliyeweka vigezo hivi aliweka lini? Nani huyu? Je, sababu zile za kuweka wakati ule enzi ya ukoloni mpaka sasa bado zipo? Hivi sababu hizi hazijapitwa? Kwa sababu tumeendelea, kuna barabara, mambo ya elimu, mambo ya kilimo, kuna alizeti, kuna vitunguu, kuna asali, kuna pamba, kuna kuku, sasa vyote hivi jamani. Nyumba nzuri mimi nimetembea sana, Tanzania hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa asilimia 80 za nyumba ni nyumba za bati, sasa mimi nashangaa sana kuambiwa kuwa Singida ni Mkoa wa mwisho. Nani huyo aliweka hii kitu? Hivi haiwezi kuwa *reviewed?* Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba sana juu ya hilo, tulikwambia kule na mimi ninakwambia hapa kwa kweli watume vijana wako walifanyie jambo hili uchunguzi mzuri kwa sababu linaturudisha nyuma. Lina–*discourage* watu wa Singida wasiendelee kupiga hatua kwa sababu hatua walizopiga bado wanaambiwa kuwa ni Mkoa wa mwisho, sasa kama ni hivyo wanavunjika moyo. Nakuomba sana, vijana wako na ofisi yangu ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya waweze kuzingatia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijijini tumeongeza Vijiji kama nilivyosema, lakini Watendaji hawapo. Najua nia ya Serikali ni kuwa na Watendaji wa Vijiji ambao ni *Form Four*, lakini kwa sasa ukimpata *Form Four* siku ya kwanza, siku ya pili, likitolewa tangazo la maendeleo ya jamii anakwenda kwenye maendeleo ya jamii. Ushauri wangu ni kwamba hawa walioko sasa waangalie wale ambao ni *trainable material* wapelekwe Hombolo waelimishwe, wapewe nafasi hizi, wasiendelee kukaimu. Naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na leo hii kuweza kusimama na kuweza kuchangia hotuba hii. Pia, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ninampongeza Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wanaotupa sisi katika kipindi hiki na kwa muda wote huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya bajeti amegusia sekta nyingi tu kama elimu, afya, kilimo na mawasiliano. Lakini hata hivyo, alisahau kuzungumzia juu ya sekta ya Sheria. Kwa hiyo, mimi naanza na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama zetu zina upungufu wa Mahakimu na Majaji. Pia, Mahakama zetu hasa Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya na majengo yake ni mabovu hayaridhishi kwa hivyo ni upungufu. Vilevile katika Mahakama hakuna vitendea kazi vya kutosha, hilo nalo ni tatizo. Kwanza, mimi ninazungumzia kuhusu Majaji na Mahakimu, ni lazima maslahi yao yaboreshwe ili waweze kufanya kazi zao vizuri waepukane na maneno yanayozungumzwa Mitaani kuwa wao hali zao ni ngumu. Hili ni tatizo, naomba waangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika vyombo vya habari tulisikia Kenya kuwa wao tayari wamekwishaboresha Katiba yao mpya na katika marekebisho ya Katiba yao mpya jambo walilolipa kipaumbele ni Mahakama ya Kadhi.

Mahakama ya Kadhi ni kitu muhimu sana kwa Waislamu. Kenya ina idadi ya watu isiyopungua milioni 35, Tanzania ina watu wasiopungua milioni 40, lakini ukiangalia Kenya waumini wa Kiislamu ni wachache zaidi kuliko waumini wa dini nyingine, na ukiangalia Tanzania inasema kuwa Waislamu ni wengi zaidi kuliko waumini wa dini wa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana sekta hii nilichangia na mara hii nachangia tena suala hili, kila siku linazungumziwa liko katika mchakato, lakini bado halijatatuliwa. Jambo hili limo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 132. Ninanukuu kifungu cha 108 (b), je, Waislamu wa Tanzania utawaambia nini kuhusu suala hili? Ahadi bado haijatekelezwa, Waislamu mnawadanganya, kesho kutwa Waislamu mtawaambiaje katika majukwaa? Hili jambo litekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafi wa Jiji wa Dar es Salaam linalalamikiwa kuwa ni chafu sana na uchafu huu hutokana na takataka zinazozalishwa kila siku. Miongoni mwa sababu zinazopelekea hivyo ni magari yanayosomba taka kupeleka kwenye madampo ya taka kukumbana na msongamano wa magari wakati wa mchana, kwa hiyo, hawawezi kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayojishughulisha na mamlaka hii, tunataka ifanye marekebisho. Badala ya takataka zile kusombwa mchana, wawe wanasomba nyakati za usiku ili wasikumbane na matatizo ya msongamano wa magari kama wanaopata mchana wakati wakifanya kazi, kutokana na uchafu kuongezeka hasa kipindi cha mvua maji yanayotiririka katika mabomba ya taka huchukua maji yale yakaziba mitaro na makaro hivyo, uchafu kuzidi, inzi kuenea na baadaye kupelekea kupata maradhi ya kuharisha na kutapika pamoja na malaria na kipindupindu. Kwa hiyo, suala hili liangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja katika Mamlaka ya Bandari zetu. Bandarini kuna usumbufu ambao tunaupata sisi akina mama, siyo maadili mifuko yetu sisi kama akina mama kupekuliwa na wanaume hasa mikoba yetu ya mikononi kwasababu kuna siri nyingi ndani ya mikoba yetu. Askari wa kike wapo, kwa nini wasipekue mizigo yetu sisi wanawake? Kwa hiyo, hili halitufurahishi, tunaona kama ni unyanyasaji, mtu *handbag* yake kupekuliwa na mwanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naongelea maafa ya vifo vinavyotokea baharini. Kwanza vyombo vyetu kabla havijaondoka Bandarini vinafaa vikaguliwe. Kwasababu vyombo ni vichakavu na hupakiwa mizigo pamoja na abiria kupita kiasi cha uzito wa chombo kile. Chombo kile kinaposafiri muda mfupi tu kinapigwa na dhoruba, kinapinduka. Kikizama chombo kile idadi ya watu waliopakiwa mle hawatajulikana. Hasa vyombo vinavyotoka Tanga kwenda Pemba na vinavyotoka Pemba kwenda Tanga

au kutoka Tanga kwenda Unguja, kwa hiyo suala hili naona *SUMATRA* wanalifumbia macho, ifanyike juhudi na upembuzi wa kina juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mauaji ya watoto. Mwenzangu mmoja mchana hapa alizungumzia kwamba watoto wanauawa na kabla hawajauawa, wanaingiliwa kinjisia, watoto wa miaka miwili mpaka mitatu, watoto wa kike, halafu wananyongwa eti kwa imani za kishirikina ili kupata mali. Sasa ninauliza, kati ya maaalbino waliouawa, ni nani alitajirika? Au hawa walioua hawa watoto, ni nani alipata cheo kwa kuua Albino au mtoto asiyekuwa hatia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linatia uchungu sana. Siku moja hapa Waziri Mkuu alilia kwa suala hili la mauaji ya Albino na watu wasiokuwa na hatia. Hivyo, hawa wauaji ni sawa sawa na wanyama. Wanyama wakali wakiingia katika Kijiji wakivamia wanauliwa na hawa wakiingia kwenye majumba kuiba mtoto akikamatwa auawe, yaani ahukumiwe kunyongwa kwa sababu huyu anahatarisha maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina zaidi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, sasa namwita Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba ajiandae.

**MHE. JUMA A. NGASONGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni hotuba ambayo mimi imenitia moyo sana hasa katika ile sehemu ya kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu, sehemu ile sasa wale wanaobisha ni kwamba wanabisha tu, lakini mafanikio yameonyeshwa pale vizuri na nina hakika tutaendelea kuonyesha mafanikio mazuri zaidi, tutakapopata fursa zaidi kutoka kwa Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwombe rasmi hapa Waziri Mkuu jambo ambalo wapigakura wangu wa Ulanga Magharibi wamenituma. Wakati tunafanya maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Vijiji na vitongoji tulipata matatizo katika Kata ya Usangule ambayo mpaka leo hatujachagua viongozi kwasababu kulikuwa wa utata wa mipaka ile. Wananchi wakaibishia na Serikali, baadaye wakafikia kwamba badala ya kuwa na Vijiji vinne katika Kata ile kuwe na vijiji vitatu, yaani Vijiji vya Kalingakelo, Usangule A na Usangule B na vitongoji vyao ni vile vya Chikole, Mipululu na Likeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo hili lifanyike basi na nina hakika mmekwishalikamilisha, sasa tufanye uchaguzi na wale washiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, yaani Madiwani na Serikali Kuu kwasababu kuachia wasiendelee kuchagua kwanza, kuchaguana wenyewe kupata Serikali ya Vitongoji na Serikali za Vijiji ni dosari kubwa katika kutekeleza mambo yao. Kwa hiyo, naomba ombi hili nilifikishe kwenu Serikalini, pale ofisi ya Waziri Mkuu ili lichukuliwe hatua za haraka.

Kwa hiyo, naomba sana Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama tunavyosema wewe ni mtekelezaji mzuri sana wa Ilani ya Uchaguzi na ni kweli

inathibitisha kwamba wewe ni mtoto wa mkulima kwa sababu ulivyopita kwenye maeneo yetu ulikiri kwamba alah! kumbe na Tabora, Manispaa wanalima mahindi! Sasa bahati nzuri umekwenda lakini sisi tunaoishi katika mazingira yale tumeyaona. Kwa hiyo, tunaomba Waziri Mkuu aliangalie hilo ili hawa nao waweze kuingiza kwenye mtazamo wa pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba sisi tuna Soko Kuu la Tabora, kwa miaka ya nyuma soko hili lilikuwa limeungua likaachiwa Manispaa kutenga fedha, likawa linafanyiwa ukarabati mdogo mdogo ambao haukidhi matakwa ya soko la kisasa. Kwa hiyo, naomba Mama Mheshimiwa Celina Kombani utusaidie soko kuu hili liingie kwenye mradi maalum wa utekelezaji wa masoko yote nchini kama ilivyoelezwa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu. Tunaomba sana kwa sababu fedha zinazotengwa na Manispaa hazitoshi lakini ikiingizwa kama mradi maalum mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* (Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezunguka maeneo mengine nimeona kuna kumbi ambazo wenzetu wameomba kama mradi. Sasa sisi kwa kuwa sasa hivi kipaumbele chetu ni soko, tunaomba soko lile ambalo lina uzoefu na ni la miaka mingi na kwa kuwa Tabora ina historia ya mambo mengi. Sasa kwa awamu hii ya nne Mama yangu, Dada yangu na kipenzi changu naomba soko hili liingizwe kama mradi maalum kwa Mkoa wa Tabora angalau hili nalo tulione. Mheshimiwa Waziri Mkuu nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niingie pia kwenye suala zima la elimu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuja kwenye ziara yake alitembelea shule ya *Tabora Girls*, walimweleza upungufu mkubwa wa walimu na yeye mwenyewe alijionea. Zile shule ni shule maalum yaani *Tabora Boys, Tabora Girls* na Milambo, shule hizi zina historia kubwa na kama historia ni kubwa basi tuienzi kama alivyoweza kuienzi Hayati Baba yetu wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere. Alizienzi hizo shule, wale watoto wanatoka Mikoa mbalimbali hawawezi kusoma hata *tuition* wanapokosa walimu hususan kwenye masomo ya hisabati, historia, sayansi, jiografia na kadhalika ni tatizo, hizi shule tatu pamoja na kwamba kuna shule nyingine za sekondari hazina walimu, zina upungufu mkubwa. Naomba Serikali iangalie kwa kina suala zima la walimu kupelekwa katika shule hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine la barabara, naipongeza sana Serikali, ni Serikali sikivu, miaka yote ndiyo maana leo nimekuja nimetulia sijapeta mikono lakini miaka yote huwa napeta mikono, nimefurahishwa na kazi nzuri na nimefurahishwa na Bajeti hii kwa kiasi kilichotengwa nimeridhika na sasa hivi Tabora unakwenda unagusa tu barabara zinatengenezwa na wakandarasi wako kwenye *site*.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri unayoifanya. Lakini ombi langu kwenye miundombinu kuna barabara za ndani ambazo ni za Mkoa, kuna barabara ambayo inaunganisha kutoka Tabora Mjini Manispaa kwenda Bukene kupitia Mambali, pale kuna kipande kikubwa sana ambacho kinaitwa barabara ya Mwanza, pana vumbi watu wamekula vumbi mpaka wamechoka na hatujui hatima yake itakuwaje. Kwa hiyo, naomba Wizara kipande hicho kilichobaki kupitia *TANROAD* hebu

wakimalizie kwa kilomita hizo mpaka kiwanda cha nyuzi na hatimaye kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni suala la mgogoro tuliokuwa nalo hivi sasa, kiwanda cha nyuzi kulikuwa na mgogoro mkubwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara anaelewa alishafika katika eneo hilo. Kuna watu ambao mpaka leo wamedhulumiwa haki zao hawajapata wafanyakazi waliokuwepo pale. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele Ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanne Mchemba na sasa namuita Mheshimiwa Juma Njwayo atafuatiwa na Mheshimiwa Hasnain Dewji na Mheshimiwa Bujiku Sakila, ajiandae.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu kwenye Bajeti ya Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru Waziri Mkuu, kaka yangu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mheshimiwa Celina Kombani, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na watendaji mbalimbali waliopo katika Ofisi zao…

**MWENYEKITI:** Ni Mwanri!

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mwanri na watendaji wote waliopo katika Ofisi zao kwa mambo mbalimbali ya maendeleo wanayotusaidia hapa nchini. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru wananchi na wapiga kura wa Tandahimba kwa heshima waliyonipa mwaka 2005 ya kunipa kura nyingi za kutosha zilizonifanya kuwa Mbunge wa Jimbo la Tandahimba. Naamini kuwa kwa ushirikiano walionipa na kwa mambo mengi tuliyoyafanya mwaka 2010 watanipa tena heshima hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kumpongeza mdogo wangu Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa kumuunga mkono Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kule Kigoma, huu ndiyo upinzani, upinzani tusifiane pia kwa yale mambo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi iliahidi ahadi nyingi na kwa kiasi kikubwa imetekeleza. Mimi nataka kutoa mfano tu wa Jimboni kwangu Tandahimba asiye na macho basi avae miwani kama nilivyovaa mimi ili nione vizuri. Lakini ndugu zangu mwaka 2005 Tandahimba ilikuwa haina Hospitali ya Wilaya sasa tuna Hospitali ya Wilaya nzuri yenye kila aina ya vifaa, tuna *ultra sound machine* na x-*ray machine*, wananchi wa Tandahimba walikuwa wanakwenda Ndanda zaidi ya kilomita 60 lakini leo mambo yale hayapo tena. *(Makofi)*

Ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, mwaka 2004 alikuja kama Mwenyekiti wa CHADEMA aliona pale hapakuwa na kitu lakini juzi alikuwa pale ameona mambo yanavyokwenda vizuri. Mwaka 2006 Tandahimba tulikuwa hatuna shule za sekondari za kutosha tulikuwa na sekondari tisa tu lakini leo tuna shule za sekondari 26 na mimi kama Mbunge wao nimechangia katika shule hiyo ama mabati au saruji au matofali ya kuchoma kuwaunga mkono kwa jitihada hizo wanazofanya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu mwaka 2005 ilikuwa haiwezekani kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi kuwa na wanafunzi wengi walioko Chuo Kikuu lakini leo Chuo Kikuu cha Dodoma peke yake kina wanafunzi 550 wanaotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi, haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tandahimba sasa tuna Benki mbili, Benki moja ya wananchi tumeshirikiana nao na tuna Benki ya *NMB* lakini mwaka 2005 tulikuwa hatuna. Barabara zinazopitika na ushahidi tosha ni Wabunge wa Kamati ya Hesabu ya Serikali za Mitaa mwezi Aprili walitoa *report* yao hapa waliipongeza sana Wilaya ya Tandahimba wakiongozwa na Mheshimiwa Dr. Slaa  mwenyewe na Makamu Mwenyekiti ndugu yangu Mbunge wa Singida akasema watendaji waende Tandahimba wakajifunze tunavyofanya mambo  mazuri. Kwa hiyo, nashangaa watu hapa wanavyobeza kwamba CCM haijafanya vitu vizuri, jamani CCM imetutoa kubaya inatupeleka kuzuri. CCM Oyeeee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shaban Robert aliwahi kusema kwamba wakati una mabawa kama ndege na kwamba nilikuwa natoa tu *introduction* ya mambo yanavyokwenda ni afadhali niende moja kwa moja katika kushauriana na Serikali. Kuna watu hapa wanaamini kwamba Serikali inaweza kufanya kila kitu kwa miaka miwili, tuwape nafasi si wanaendelea kusonga kazi?  Si wanaendelea kutufanyia mambo mazuri?

Tuwape nafasi na ushauri wa wapi wanakwenda pole pole ili wakazanie maeneo hayo na kwa sababu hiyo mimi naomba kuishauri Serikali na hii inakwenda moja kwa moja kwa Waziri Mkuu maana ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali. Serikali yetu ina tatizo ninaloliona, inatusaidia kurudi nyuma kidogo na lenyewe ni urasimu wa watendaji wetu. Urasimu huu umetuzalishia mambo madogo madogo mengi ambayo yangetusaidia kusonga mbele sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aya ya ishirini amesema Tanzania ni ya 131 kati ya nchi 183 kwa wepesi wa kufanya biashara. Mimi nadhani wa 131 hii inatokana tu na urasimu urasimu usio wa lazima. Nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ujitahidi watendaji hawa uwabanebane wabadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Haroub Said Masoud,  jana alisema hapa kwamba Daraja la Kigamboni kama si mambo ya urasimu urasimu haya pengine lingekuwa limeshakwisha, sasa wabane tupunguze urasimu huu maana hauna sababu. Wakati *ATMUS* wanataka

kuanza kuzalisha umeme kule Mtwara kipo kitu kinaitwa *National Negotiation Team* ilichukua mwaka mmoja na nusu bila kufikia maamuzi ya nini kifanyike. Hivi walikuwa wanafanya kitu gani kwa mwaka mmoja na nusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri kuna haja ya kutazama mbele. Maamuzi tuliyoyafikia tuyafanikishe haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili ni kwamba umeme kama unavyojulikana ni nguzo muhimu sana, nchi kama Malaysia imetumia Mifuko ya Jamii kuwekeza katika umeme na hivyo imeweza kuzalisha kiasi kikubwa cha umeme mpaka na kuwa na ziada ya karibu megawati 4,600. Kwa kuwa mifuko yetu ya jamii Tanzania imeanza kufanya vizuri kama tunavyoona Chuo Kikuu cha Dodoma na mimi juzi nilikuwa Hombolo nimeona *GEPF* unavyofanya vizuri kwenye Chuo cha *Local Government*. Mimi naomba tuwatengenezee mazingira mazuri ili hii mifuko ambayo tayari imeanza kuonyesha nia ya kuwekeza kwenye suala la umeme ili tuweze kupata maendeleo yaliyo bora na kutukuka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada zilizofanywa na Serikali za kuleta umeme Mkoa wa Mtwara umeanza kupunguza kwa kiasi fulani matatizo ya maji kwenye Wilaya ya Newala na Tandahimba, kama wengi mnavyojua Wilaya ya Tandahimba na Newala ina matatizo makubwa ya maji. Mimi natoa rai kwa sababu suala la umeme muda mfupi ujao katika muda wa miezi miwili au mitatu tutakuwa tumeachana nao.

Naomba basi kwa sababu Serikali ilikuwa na miaka mitano, imemaliza minne na sasa Bajeti yake ya mwaka wa tano ni hii basi nguvu ifanyike kuhakikisha ukarabati wa mabomba ule unaohitaji karibu shilingi bilioni nne na milioni mia tano unafanyika kwa haraka ili tuwapunguzie wananchi wale wa Tandahimba na Newala adha ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa minajili hiyo hiyo ya kwamba Bajeti hii ndiyo ya mwisho ya Awamu ya Nne, kwa kipindi cha kwanza naomba barabara ile ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi tuimalize. Nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ulikuwa kule umetuahidi na hata hapa Naibu Waziri wa Miundombinu alisema kwamba kwenye Bajeti hii tutatenga fedha za kutosha kwa ajili ya usanifu, sasa yasije yakawa maneno tu, wananchi wametusikia kule ili tuhakikishe kweli yale tuliyowaahidi Watanzania yanatimia kama tulivyowaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Serikali itafute namna ya kupunguza tatizo la wataalamu wanaokataa kwenda kwenye ile Mikoa iliyo pembezoni yaani *marginalised regions*, hili ni tatizo kubwa, tutazalisha walimu wa kutosha, tutazalisha madaktari na manesi lakini tusipotengeneza mpango wa kuhakikisha kwamba wanakwenda, watakuwa wanazaliwa wanapotelea Dar es Salaam pale, hawaeindi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii leo ili kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu ambayo ni hoja iliyo mbele yetu, namshukuru sana Waziri Mkuu, watendaji wake wote na Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo vilevile nawashukuru wananchi wangu wa Kilwa Kusini kwa kunichagua ili niwe mtetezi wao na mwakilishi wao, leo nasema nimeshatimiza miaka mitano, nimepambana na mambo mengi, tumefanya mengi na bado tunataka kufanya mengi huko mbeleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo niipongeze sana Serikali za awamu zote, tatizo la Kusini limekwisha, barabara, Daraja la Mkapa, wale ambao wanasema Serikali haijafanya kitu ni wapumbavu, hao wamezaliwa hivi karibuni. Kwa nini nasema hivyo? Kama mtu kazaliwa mwaka 1990 atasema hivyo, zamani unakwenda Kilwa inakuchukua siku tatu kufika Kilwa kilomita 380. Daraja lilikuwa halipo tulikuwa tunavuka kwenye mitumbwi, lakini leo tuna daraja, tunavuka kwa dakika moja kilomita moja lile daraja lina urefu wa kilomita moja, tunavuka kwa gari kwa dakika moja na ni *duel*, gari mbili zinapisha pale. Mwenye macho haambiwi tazama, barabara kutoka Mtwara mpaka Mwanza mwakani itakuwa tayari na hivi ninavyoongea barabara kutoka Somanga – Fungu mpaka Nyamwage iko mbioni na kilomita thelathini zimeshakwisha. Bado hatujafanya kitu hapo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme nilikuwa napigia kelele umeme hapa Bungeni lakini leo umeme wa Somanga – Fungu uko tayari, tatizo limebaki la mita na hilo naona mpaka wiki ijayo…

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Kuhusu Utaratibu!

**KUHUSU UTARATIBU**

**MWENYEKITI:** Kanuni!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Kanuni ya 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Bunge tuna lugha maalum tunayotumia, Mheshimiwa Mbunge lugha aliyotumia imetuudhi baadhi yetu, tunaomba afute usemi, hakuna mpumbuvu hapa kila mtu amekuja kwa kazi ya wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nimekusikia, huyu ni mchangiaji wa pili kutoka Lindi ambaye amekuja na Kiswahili cha ajabu baada ya yule wa mwanzo kuwa na Kiswahili cha aina hiyo hiyo. Nadhani ingekuwa vizuri ukamsaidia na msamiati wa kutumia badala ya hilo neno alilolitumia kwa maana hiyo, itamsaidia. Naam Mheshimiwa! Ni msamiati tu endelea. *(Makofi)*

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hilo kwa sababu inatia uchungu kwamba Serikali yetu ina bidii ya kufanya vitu mbalimbali, lakini tunakuja kuambiwa hatujafanya kitu, hatuwezi kusema upumbavu, sijamtaja mtu ambaye ni nani mpumbavu asiyeelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa umeme tunaelekea kuzuri kwa kuwa tuna gesi ya Songosongo, umeme sasa umekuwa historia Kilwa, hatuna matatizo, umeme wa kutosha tuna megawati saba, hakuna sehemu ya kupeleka. Wilaya za Rufiji na Kilwa zinafaidika hatuna matatizo ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kilimo Kwanza, Kilwa tuna maeneo makubwa sana ya kilimo, tunaomba wawekezaji waje kuwekeza Kilwa kwenye kilimo. Maeneo yapo ya kutosha tunawakaribisha, tunawaheshimu wawekezaji waje kuwekeza kwenye kilimo. Tuna kilimo cha umwagiliaji, tuna uwekezaji mwingine wa *gypsum* pale Kilwa, tunawakaribisha wawekezaji waje waweke viwanda kwa kuwa tuna umeme wa kutosha.

Kuhusu uvuvi, naishukuru Serikali kwa kupunguza ushuru na kuondoa *VAT* katika vifaa vya uvuvi, leo unilinde nimepoteza dakika zangu tatu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kuna muda wako mfupi sana.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa upande wa uvuvi kwa sababu tumepunguza ushuru kwenye vifaa vya uvuvi na naiomba Serikali itangaze kwa sababu tumeweka hii siri, kwenye kilimo tumeitangaza kwa sababu matrekta yamepunguzwa ushuru, lakini kwa kule wananchi wa Kilwa wengi wao ni wavuvi, tungeitangaza kwa sababu boti, *engines*, nyavu, nyuzi na maboya yote yamepunguzwa ushuru, isipokuwa nilikuwa nataka ufafanuzi tu Waziri husika atueleze nyavu *size* gani inakubalika kwenye maeneo gani, *size* gani inakubalika kwenye maziwa yetu, kama Ziwa Victoria na *Lake Tanganyika* ili wavuvi wetu wasije kupata ile *harrassment* wanayopata sasa hivi, bugudha ile ya kuchomewa moto na kupelekewa kwenye vyombo vya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka niseme kidogo upande wa elimu. Elimu tuna shule za sekondari nyingi tu 22 pale katika kata yangu, lakini tuna tatizo moja la mlo kwenye shule zetu hizi. Nilikuwa naiomba sana Serikali kwa kuwa wananchi wetu hali zao ni duni sana, mkulima anapata pesa wakati anavuna, kuna wakati mkulima hana hela, kijana anatembea maili tano kwenda shuleni akirudi ana njaa, hatuwezi kupata elimu bora kama hatukuwapa chakula katika shule zetu za sekondari. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili katika shule zetu za sekondari kwa sababu Serikali inafanya mambo mazuri, naona Serikali itatilia mkazo upatikanaji wa chakula katika shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nilikuwa nataka niiombe Serikali kwa kuwa tuna gesi ya Songosongo nimeiongelea sana hapa kuhusu gesi ya Songosongo pale tuna mwekezaji ambaye wawekezaji wote wanaambiwa wasaidie jamii iliyo kando kando na hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichagie katika Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa kabla sijasahau naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda labda nianze moja kwa moja na kutoa taarifa ya mafanikio katika Jimbo langu. Fanikio la kwanza, mwaka 2005 maji ya Ziwa Victoria yalikuwa bado hayajaingia Jimboni kwangu, hivi sasa maji hayo yapo kwenye Tarafa ya Mwambashimba na usambazaji umeshaanza. Ombi tu hapa ni moja tu kwa Serikali, Wilaya ya Kwimba imeomba shilingi milioni 55 kutoka Serikali ili kusaidia katika maji hayo. Serikali imeshakubali, tunaomba fedha hii itolewe haraka ili Halmashauri ya Kwimba wasambaze maji hayo haraka katika vijiji vinavyotakiwa kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano iliyopita mradi wa maji Ilula ulikuwa haufanyi kazi, mradi huo sasa hivi unafanya kazi. Tulikuwa na matatizo na mradi wa maji ya Kilewi, mradi huu unafanya kazi sasa hivi. Hatukuwa na mpango wowote wa kupatia maji katika kijiji cha Humarwa, hivi sasa kuna *JICA* ambao wanafanya kazi kukamilisha kutoa maji katika kijiji cha Humarwa, hayo yote ni mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende upande wa umeme. Kwa bahati mbaya sana mradi haujaanza lakini angalau sasa hivi tunauongelea, miaka mitano iliyopita hatukuwa na mpango ambao ulikuwa wazi wa kutoa umeme kwa kijiji cha Humarwa, Shirima, Mwamashimba na Ilula. Hivi sasa mradi huo upo katika utekelezaji, kwa hiyo, haya ni mafanikio. Lakini vile vile ni vizuri tukasema miaka mitano iliyopita hatukuwa na shule hata moja iliyokuwa na *solar*, hivi sasa tuna shule karibu tano ambazo zina *solar*. Lakini tuna zahanati ambazo zina *solar* na vituo vya afya ambavyo vina *solar* kitu ambacho miaka mitano iliyopita hatukuwa navyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda upande wa barabara hatukuwa na barabara kutoka Hungumaro kwenda Ngudu ingawa sasa hivi tuna barabara hiyo, hatukuwa na barabara katika kijiji cha Igunganoro, Igunganoro wakati wa masika ilikuwa ni kisiwa hivi sasa kuna barabra ambayo inatoka Mijongo kwenda Igunganoro, hata wakati wa masika unaweza kwenda kwa gari yako bila wasiwasi, unaweza kutoka Igunganoro kwenda Nyahonge bila shida. Haya yote ni mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, barabara ya Lunele kwenda Gaturi ilikuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na kutoka Kungumaro kwenda Ngudu pamoja na kwamba hapakuwa na barabara, lakini barabara hizi zilikuwa zinahudumiwa na Halmashauri. Hivi leo barabara hizi zote ziko Mkoani, kwa hiyo, haya ni mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha miaka hii mitano tumefanyikiwa kukarabati hizi zahanati saba katika Jimbo la Kwimba, tumefanyikiwa kupata gari la wagonjwa ambalo liko Mwamashimba na kabla ya hapo, mtu kama ana mgonjwa wake Mwamashimba, ili aweze kumpeleka Ngudu alikuwa lazima atumie kati ya laki moja na laki tatu, hivi sasa mtu akiwa na mgonjwa anatakiwa kwenda Ngudu,

anaenda na gari la wagonjwa kwa gharama ambayo ni sifuri, yote hayo ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais katika Serikali ya Awamu ya Nne, imefanya kazi nzuri. Haya niliyoyataja ni mifano tu, bado kuna mambo mengi lakini kwa sababu ya muda nimeona nitaje haya machache kuonesha kwamba kuna mambo ambayo yamefanyika katika Jimbo la Kwimba. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake ni watu waadilifu sana, watu wasikivu sana na kila mmoja anaweza kuwa mashahidi, mimi sijasikia hata siku moja Tume inayokwenda kwa Waziri Mkuu wala kwa Waziri Mheshimiwa Celina Kombani, wala kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hawa wanafanya kazi nzuri sana na kwa kweli nawapongeza sana. Lakini kwa sababu ya muda labda niende moja kwa moja kwenye maombi. Ombi la kwanza nimeshalisema kwa Serikali tumeshaomba shilingi milioni 51 naomba zitolewe haraka ili maji yaendelee kusambazwa katika kata ya Mwambashimba, tumeshaomba maji haya ya Ziwa Victoria yaende mpaka Ngudu. Serikali imeshapokea ombi hilo, naomba sana ombi hilo na lenyewe litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna vijana wengi ambao wanamaliza *form four,* baada ya hapo siyo wote ambao wanapata nafasi ya kwenda kidato cha tano, tumeiomba kuwe na Chuo cha Ufundi, tumeahidiwa, tunaomba sana kile Chuo cha Ufundi kijengwe haraka katika Wialya ya Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba barabara ya kutoka Kungumaro kwenda Ngudu iwekewe lami, kwa sababu barabara hii isiishie Ngudu tu iende hadi Magu, itasaidia sana katika usafiri kati ya watu wa Shinyanga, Musoma na watu wa Ngudu wenyewe watakuwa wameshatoka kwenye kisiwa cha usafiri. *(Makofi)*

Naomba sana kituo cha afya cha Mwamashimba kiwezeshwe kutoa huduma zaidi. Tatizo la maeneo hayo kuwa ni watu wengi sana, lakini vilevile kuna shida ya malaria sana. Kwa hiyo, tunachohitaji sasa ni huduma ya mgomjwa kupatiwa damu au maji. Kwa hiyo, tunaomba sana kituo cha afya cha Mwamashimba kiwezeshwe kutoa huduma zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende moja kwa moja kwenye Kanuni. Pamoja na kwamba Wizara hii, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara hiyo husika zinafanya kazi vizuri sana, lakini bado kuna watumishi ambao wanahitaji kusimamiwa kwa karibu zaidi. Mimi nilikuwa najaribu kufikiria hivi kuna tatizo gani? Ni vyema hizi Kanuni za Utumishi zikaangaliwe vizuri zaidi ili wanaohudumiwa na watumishi hawa na wenyewe wawe na nafasi ya kutoa katika tathmini ya watumishi hao ili huyu mtu asitathminiwe na viongozi wake wa juu pekee yake ambao hawapokei huduma yake moja kwa moja, itakuwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea kwenye uchaguzi. Mimi niko Mbugenge wa Jimbo la Kwimba hali sio mbaya, nafahamu kuna watu ambao wametangaza nia, ninawakaribisha sana, lakini wananchi wa Kwimba wanajua kati ya mwakilishi na mfadhili. Kwa hiyo, wanajua lini wamchague mfadhili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bujiku itakuwa kengele yako ya pili hii.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kushiriki katika mjadala huu. Naomba kwanza nianze kutoa *clarification,* wakati Mheshimiwa Juma Njwayo akichangia alisema mwaka 2004 Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa alikuwa Mwenyekiti wa CHADEMA, hapana, Mwenyekiti wa CHADEMA alikuwa Mheshimiwa Freeman Mboye na yeye alikuwa Katibu Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitaenda moja kwa moja kwenye suala la umeme wa Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Kigoma, katika ukurasa wa 51(e) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi naomba kunukuu, inasema kwamba “Kutakuwa na kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Ruvuma na Gridi ya Taifa.” Mpaka awamu hii ya nne inamaliza muda wake ahadi hiyo haijatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikika ni kwamba kuna umeme pale Mkoani Kigoma, pale mjini ni mashine ambazo zinatumia dizeli ambazo ni za *packing’s* ambazo zimekuja kuongeza nguvu mashine ambazo tayari zilikuwa zimeshachakaa na kwa upande wa Kibondo na Kasulu ndio kwanza wamejenga kama *basement* sehemu ya kuweka tu hizo mashine zitakapoweza kuja na hazijajulikana zitakuja lini na hiyo inaonekana ni kwa sababu tu tunaelekea kipindi cha uchaguzi. Kwa hiyo, suala langu nataka kujua, kwa mfano mwaka 2006/2007 tuliambiwa kwamba akiwa Waziri kipindi hicho…

**MWENYEKITI:** Mashine una maana *generator* au vipi?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Gridi wa Taifa ninachosemea mimi.

**MWENYEKITI:** Hizo mashine unazoongelea ni *generators* au mashine gani?

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *generators,* ninachoulizia mimi ni ahadi ya Gridi ya Taifa. Mwaka 2006 ilitolewa ahadi hapa ndani ya Bunge katika kipindi cha Bajeti akiwepo Mheshimiwa Ibrahim Msabaha nafikiri ndio

alikuwa Waziri kipindi hicho, alisema zimetengwa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya umeme wa Gridi ya Taifa ambao utapitia Kaliuwa -Tabora - Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007, Waziri kipindi hicho alikuwa Mheshimiwa Nazir Karamagi akaja na mpango mpya anasema kwamba umeme wa Gridi ya Taifa utatokea Geita uje ufike Kibondo - Kasulu halafu Kigoma Mjini. Mwaka 2008, Mheshimiwa William Ngeleja anatuambia kwamba tutapata umeme kwa kupitia mradi wa *MCC,* mimi nashangaa Serikali gani ambayo haina mipango ambayo ni endelevu na wakati wametuambia kabisa tangu mwaka 2006 kwamba upembuzi yakinifu tayari umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua lini umeme wa Gridi ya Taifa utafika kwa Mkoa wa Kigoma kwa sababu kwa kutumia dizeli, yaani bado hali itakuwa ni ile ile kwa sababu Bajeti saa nyingine inakuwa ni ndogo, watakuwa wanakata umeme wakituambia kwamba hakuna mafuta ya kuendeshea hizo mashine na mashine zilizopo ni kwa Kigoma Mjini tu, Kasulu na Kibondo bado hawajapata na hamna nguzo wala hamna waya. Nilikuwa naomba wakati wa kuhitimisha Bajti hii, nipate jibu kuhusiana na hii hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye suala lingine, nitapenda kuongelea *issue* ya uvuvi. Kigoma tunalo Ziwa Tanganyika, bahati mbaya sana lile ziwa ni *under utilised,* wavuvi wana hali ngumu sana, hatuna meli za uvuvi wala vifaa ambavyo ni madhubuti kwa ajili ya uvuvi na ukizingatia kuna haya matatizo ya hizi nyavu, watu wamekuwa wakinyang’anywa nyavu zao ambapo tunaiomba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba basi kuna viwanda maalum ambavyo zinahitajika kuliko hivi sasa ambapo watu wana nyavu zao ambazo wamezoea kuzitumia siku zote wananyang’anywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ambalo ni kero kwa wavuvi wa Mkoa wa Kigoma wananyang’anywa mali zao, mashine za boti pamoja na vifaa vingine vya uvuvi. Wananyang’anywa na wenzetu kutoka *DRC Congo*, maharamia, lakini bahati mbaya sana nakumbuka mwaka 2007 jambo hili liliongelewa katika Bajeti ya Wizara ya Usalama wa Raia nafikiri, kipindi hicho Naibu Waziri Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed ndio alijibu hili suala wakati akihitimisha Bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia kwamba wavuvi mpaka leo hicho kitu bado kinaendelea na kwa taarifa wanatakiwa kuchangia mafuta ya petroli kwa ajili ya polisi ambao wanafanya doria. Mheshimiwa Waziri kipindi hicho aliniambia kwamba sio wajibu wao, lakini kama wanachangia sio vibaya kwa sababu polisi wana Bajeti ndogo, hawawezi kutosheleza. Sasa nilikuwa naomba Serikali iangalie baadhi ya majukumu kwa sababu wale unakuta kwanza vifaa wanavyotumia ni duni, halafu wanatakiwa wakamuliwe kutoa mafuta kwa ajili ya doria na hawana *alternative* inabidi wafanye hivyo kwa sababu mali zao zinakuwa zikiibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nilikuwa naomba niende kwenye Bajeti ya mwaka huu. Tunaona Bajeti ya mwaka huu ni shilingi trilioni 11 na ushee, lakini kinachonisikitisha mimi ni kwamba Bajeti ya kuendesha Serikali kwa Matumizi ya

Kawaida itakuwa shilingi trilioni 7.7 na ushee, kibaya zaidi ni kwamba makusanyo ya ndani ni trilioni 6 tu na kidogo. Sasa hapa, inaonekana kwamba inabidi nchi ikope, Serikali ikope kwa ajili ya kuendesha matumizi ya kawaida ya Serikali ya kila siku kwa takribani trilioni 1.7. Sasa napenda kujiuliza inakuaje nchi inashindwa kujiendesha yenyewe mpaka inatokea Bajeti tu ya kuendesha Serikali inabidi ikopwe kwenye mabenki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi hii naona ni aibu kubwa na inabidi tujitahidi kufuata maoni hata yanayotoka Kambi ya Upinzani kwa sababu tumechoshwa na vyanzo vilevile vya mapato kila siku tukiambiwa ni bia na sigara ndio vinatakiwa kuchangia Bajeti yetu. Ina maana watu watakapoamua kuokoka wasivute sigara wala kunywa pombe ina maana tutakuwa kwenye hali ngumu sana. Pamoja na hivyo, bado matumizi ya Serikali ni makubwa pamoja na kwamba Bajeti kila mwaka inakuwa ni ndogo, ununuzi wa magari ya kifahari unaendelea, ununuzi wa samani kila mwaka unaendelea kwa sababu samani zinazonunuliwa sio bora kwa sababu nyingi tunaambiwa zinatoka China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia pia ripoti ya *CAG*, lipo tatizo la *ghost workers*, kwa upande wa Wizara ya Elimu imefanyka kwamba kuna *ghost workers* 1413 na tayari shilingi milioni 43 na ushee zimeshalipwa kwa hao *ghost workers* yaani walimu ambao hawapo, vivyo hivyo kwa Wizara ya Afya ambapo tayari imeshalipwa shilingi bilioni 4 kwa wafanyakazi hewa. *(Makofi)*

Naomba Serikali iangalie hilo, nikisema niende Wizara moja moja, muda hautoshi, lakini naweza kwenda kwenye mfano mwingine katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, inaonekana watumishi walilipwa shilingi milioni 282 kwa ajili ya kulipia hoteli wakati tayari wameshapewa posho zao za kujikimu, masurufu ambayo hayajarejeshwa shilingi milioni 492 na ushee, ukienda matumizi ambayo hayakuwa na viambatanisho shilingi milioni 705, sasa utaangalia Bajeti yetu ni kidogo, haiwezi kutosheleza lakini bado mianya ya wizi na ubadhilifu ni mikubwa, ukienda kwenye Halmashauri unakuta hivyo hivyo, ukiangalia safari za viongozi zina misululu mikubwa ya watu ambapo saa nyingine haina tija, mimi nafikiri tuangalie tunahitaji nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye suala la Kilimo Kwanza. Kilimo Kwanza kwa mimi ninavyoona ni kauli mbiu kama zilivyokuwa kauli nyingine. Kulikuwa na kilimo ni uti wa mgongo, siasa ni kilimo na kadhalika. Mimi nafikiri kwamba tunatakiwa kuwa na mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba hicho Kilimo Kwanza kinakuwa siyo cha kumnufaisha Mtanzania ukizingatia kwamba asilimia 80 ya wananchi wamejiajiri kwenye kilimo. Lakini ukiangalia malengo ya MKUKUTA *cluster one* mwaka 2000 mpaka 2008 ilitakiwa ifikie asilimia 10. Tatizo ni kwamba tuna mipango mizuri ambayo hatuwezi kuitekeleza, tumejikuta hatukufikia asilimia 10, tukafika asilimia 4.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia inasema kwamba tutafikia asilimia 20. Lakini mpaka miaka hii inaisha tumefika asimilia 3.9 tu. Sasa unaangalia kwa kilimo hiki kuendelea kudodora maana yake ni kwamba ndiyo

maana umaskini umeendelea kuongezeka na ukiangalia *house hold survey report* unagundua kwamba Watanzania wanazidi kuwa maskini na tumeona kwamba Watanzania mwaka 2001 walikuwa milioni 11.2 kwa umaskini. Lakini kwa sasa hivi umaskini umeongezeka wamefika milioni 12.9. Hii ni hali ya hatari na hii inatokana na kwamba wananchi wengi wanatumia kilimo na kilimo kimekuwa hakiendelei mbali na sababu zingine za kuwafanya Watanzania waweze kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi ya kilimo yanatakiwa pamoja na hivyo uboreshaji wa sekta hii pia unatakiwa pamoja na hivyo wakulima wadogo wadogo na wale wa kati wapatiwe mikopo ili waweze kuhakikisha kwamba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika hoja hii iliyo mbele yetu. Napenda nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote kwa jinsi walivyoandaa Bajeti yao na jinsi walivyoiwasilisha kwa umahiri kabisa. Lakini zaidi kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa utendaji wao wa kuendesha nchi kwa wakati wote. Ni kazi kubwa kweli na inatakiwa umahiri mkubwa kuendesha na ku-*supervise* Halmashauri zote za nchi hii. Wazisimamie, wameziongoza na tumekuwa na mafanikio. *(Makofi)*

Lakini pia ningependa kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyoendesha kipindi chake cha Maswali kwa Waziri Mkuu. Mwanzoni tulikuwa na wasiwasi wengine kwamba hii itakuwa ni ngumu. Lakini kwa umahiri wake na uwezo wake mkubwa ameweza kila mara hata siku ya leo kuweza kujibu maswali yote vizuri na kuhakikisha kwamba anaonyesha uwezo mkubwa katika kuongoza na katika kujibu maswali yale ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Kyerwa, ambalo ni Jimbo langu. Nawapongeza kwa shughuli zote ambazo wamefanya tukishirikiana pamoja katika kujiletea maendeleo. Wameshirikiana na mimi na viongozi wao wengine bila kuchoka katika kuendesha mambo ya kujijengea zahanati, masuala ya kujenga mashule ya msingi na sekondari na niseme kwamba kila mara ambapo walitakiwa kutenda yale ambayo wanatakiwa kuyatenda hasa katika masuala ya michango, wameweza kuchangia vizuri na hata kujitolea katika kazi fulani fulani. *(Makofi)*

Nitoe mfano kama katika nyanja ya elimu, maelekezo ya Serikali yalikuwa ni kwamba ijengwe shule ya sekondari katika kila Kata. Lakini ni jambo la kutia faraja kweli kwamba katika Kata nyingi za Jimbo la Kyerwa walijenga shule zaidi ya moja katika kila Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Kata ya Mabila wamejenga shule tatu za sekondari, Kata ya Mkwenda ambayo ni Kata ya mfano kabisa kila kijiji wamejenga shule ya sekondari na hadithi inaendelea hivyo hivyo. Kuna Kata ya Kimuri, kuna Kata ya Lwabwere wote wamejenga shule za sekondari zaidi ya moja. Nawapongeza sana na nawatia moyo kwamba tukiendelea hivyo katika ushirikiano wetu tutaweza kujiletea maendeleo makubwa katika Jimbo la Uchaguzi la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ya kutoka Ngakorongo kupitia Bugomora kwenda mpaka Mrongo na kuendelea mpaka nchi ya Uganda. Barabara hii ilikuwa chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, lakini tunashukuru Serikali kwamba imekubali kuichukua hiyo barabara ili iwe barabara ambayo inahudumiwa na Serikali Kuu. Sasa hivi hiyo barabara ina matatizo makubwa. Lakini nimefanya mikutano mingi na Meneja wa *TANROADS* na tumekubaliana kwamba sasa hii barabara imeshatengewa fedha na ameniahidi kwa niaba ya wananchi wangu kwamba hii barabara itaanza kutengenezwa mwezi wa Julai, 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalotaka kusisitiza ni kwamba Serikali iwe makini, ijitahidi ahadi hii itekelezwe na barabara hii na mkandarasi awe katika barabara mwezi huu wa Julai, 2010.

Lakini ningependa kuweka chagizo lingine ni kwamba barabara kama hizi zinapoondolewa katika Mamlaka ya Halmashauri kama hii barabara ni ya kilomita 105. Sasa ile nguvu ambayo Halmashauri ilikuwa inaitumia katika kutengeneza barabara hizi sasa nguvu hiyo ielekezwe katika kufungua barabara zaidi katika vijiji vyetu, barabara ziwe fupi za kusaidia wananchi kuweza kupeleleka mazao yao, kuweza kwenda kwenye shughuli zao. Hizi *savings* sizije zikawa ni za kuwaongezea makandarasi bei na pesa zaidi katika shughuli za kutengeneza barabara. Hizi tunasema hazifai mpaka ziweze kuwanufaisha wananchi wa Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kyerwa tumeomba sana tangu muda kitambo kwamba jimbo hili ni kubwa, litengwe kuwa Wilaya ya Kyerwa. Maombi haya yalishafika Serikalini kwa muda mrefu na tumeshadhihirisha kwamba vigezo vya kutengwa Wilaya ya Karagwe ikawa na Wilaya mbili, Wilaya ya Karagwe na Kyerwa kwamba vigezo vipo. Ukubwa wa Wilaya yenyewe na pia hususan ukubwa wa Jimbo la Kyerwa pia sisi tunapakana na nchi mbili kaskazini na nchi ya Uganda na magharibi nchi ya Rwanda na kwa muda mrefu tumekuwa tunawapokea wakimbizi na mambo haya inataka utawala uwe karibu zaidi na wananchi. Utawala uwe karibu na mipaka hii, uhamiaji, polisi viwe karibu na sehemu hizi ambazo zinakuwa zina matatizo ya mipakani. Kaskazini Uganda, Magharibi Rwanda. *(Makofi)*

Lakini pia Jimbo la Kyerwa lina uchumi wa kujitosheleza kuweza kujiendesha kama Wilaya. Tuna kahawa ya kutosha, tuna maharage yetu yanaliwa na kulisha sehemu nyingi za Tanzania hata mpaka Sudan. Tunapeleka maharage sehemu za Kahama na Mwanza. Uchumi wetu unatutosha kuweza kuwa Wilaya ya kujisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la umeme. Hii ni ahadi ya Serikali kwamba tutapata umeme vijijini na wakati Mheshimiwa Rais alipotembelea Jimbo langu Wilaya ya Karagwe alisimama pale mpakani na Uganda na akatoa ahadi hii kwamba umeme utapatikana katika vijiji vya Wilaya ya Karagwe. Sasa ni kweli nimeshaona pilika pilika za Kampuni ya *TANESCO* na Wizara ya Nishati na Madini wakipitapita na kuangalia mradi unavyokwenda. Lakini kinacho-*matter* sasa hivi hapa ni *speed* ya utekelezaji wa mradi huu wa kusambaza umeme katika vijiji vya Wilaya ya Karagwe hususan katika Jimbo la Uchaguzi la Kyerwa. Nasema kwamba wenzetu wa Uganda maana yake tuna *trading centre* ambayo ipo pale karibu na mpaka wa Uganda na nchi yetu, panaitwa Mrongo. Wenzetu wa Uganda walikuwa hawana umeme, lakini sasa hivi wameshachangamka haraka haraka na sasa hivi upande wa Uganda sehemu ya Mrongo umeme unawake tayari, ni sehemu ya Tanzania tu ambayo bado iko gizani. *(Makofi)*

Naomba sana na naomba kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Karagwe hususan Jimbo la Kyerwa ili Serikali yetu pia ichangamke, Wiraza ya Nishati na Madini ichangamke, *TANESCO* wachangamke, ili huu umeme wetu na sisi ufungwe na ili iweze kuwasha pale Mrongo lakini na kusambaa katika vijiji na Kata ya Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu niweze kuchangia na pia niseme kwa dhati kabisa kwamba naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze pia kwa kupongeza Ofisi ya Waziri Mkuu na kumpongeza Waziri Mkuu yeye mwenyewe pamoja na Mawaziri wake, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Celina Kombani na pia kijana wetu mahiri Mheshimiwa Aggrey Mwanri pamoja na Makatibu Wakuu na wote kwa kazi nzuri ambayo mpaka sasa hivi wamejitahidi kufanya mpaka kuleta maendeleo makubwa katika mji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba na mimi nianze kuchangia. Eneo zaidi nitakalopenda kuchangia ni kuhusu mpangilio na usafi wa miji mikubwa pamoja na miji midogo. Kama tunavyofahamu miji mikubwa ni kioo na kipimo cha maendeleo na ustaarabu duniani kote. Lakini cha kusikitisha kioo cha miji ya Tanzania hakionekani, ni muhimu nchi yetu tukahakikisha tunakuwa makini katika eneo hili na hasa katika miji yetu kama Jiji la Dar es Salaam, Mwanza, Mji wa Arusha, Dodoma na mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji hii mikubwa inapata wageni wengi sana wakiwepo wawekezaji, watalii na watu wengine na kadhalika. Kwa maana hiyo basi, ni lazima tuweke nguvu ya kutosha katika kuhakikisha miji yetu ni safi na inakuwa na mipangilio iliyo mizuri. Uchafu umekidhi sana hasa katika Jiji la Dar es Salaam, hiyo lazima tukubali. Jiji la Dar es Salaam pamoja na kuwa kuna makandarasi wamefanya kazi vizuri, lakini watu wamepewa *tender* kusafisha Jiji lile mpaka leo halisafishiki. Ni mitaa michache mikubwa inayojulikana misafi lakini ukienda pembezoni Manzese na sehemu nyingine hali si nzuri. *(Makofi)*

Aidha, maji yanatiririka na hasa wakati wa mvua. Inatia huruma ni uchafu, maji yanatiririka ovyo, mifereji haitoshi. Mifereji tuliyokuwa nayo na yenyewe pia imezibwa na michanga, imezibwa na maplastiki, *oxidation ponds* hazitoshi katika mji ule. Basi mradi wakati wa mvua watu wanashindwa kusafiri katika mji ule, wanaosafiri kwa miguu ndiyo wanaathirika zaidi kupata magonjwa na wanaosafiri kwa magari, wanapata shida magari mengine yanazimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa nilitaka kusema kitu kimoja kwa wale ambao wanaelewa vizuri Dar es Salaam na nina hakika wengi wenu mnajua. Katikati pale ya *TMJ Hospital* na *Shoppers Plaza Shopping Centre* kuna sehemu ambayo ni mkondo wa maji wa kwenda baharini. Karibu yake katika siku za nyuma yaani miaka ya nyuma kulikuwa pia ni sehemu ambayo wakitumia matuta ya kutengenezea chumvi. Sasa mikondo hiyo kwa bahati mbaya sijui ni nani aliyetoa ruhusa, watu wamejenga magorofa mengi ya kibiashara yanayofanana. Matokeo yake pamefurika kabisa, bonde la mpunga limefurika kabisa, watu wanapotoka mjini kwenda Kawe hawawezi, wanapata shida kupita pale, maji yanajaa. Gari nyingine hazioni kile kidaraja pale katikati zinatumbukia. Sasa sijui ni nani waliwapa ruhusa watu hawa kuwapa maeneo kama hayo kujenga bila hata kuwaambiwa watengeneze barabara nyingine za kupeleka maji baharini. Hata ukienda mbele eneo wanaita Kwa Warioba vile vile kuna mwekezaji mmoja mwenye nyumba yake ameweka ukuta basi maji yameingilia hayawezi kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi hili jambo naliona linaleta huzuni sana maana yake mlipuko wa maradhi unazidi kuja. Kwani hata wakati mwingine mimi mwenyewe kwa safari hii mvua hizi nimeona vinyesi vikielea, inasikitisha sana. Lakini kingine ambacho kilikuwa kinasikitisha sana ni kuhusu vituo vya petroli. Vituo vya petroli vimekuwa vingi sana katika jiji la Dar es Salaam. Lakini kikubwa kinachosikitisha vituo hivyo vya petroli kweli vinajengwa, vinawekwa katikati ya makazi ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara hayo wote tunayajua, ikilipuka *petrol station* moja sijui nyumba ngapi na maisha mangapi ya watu watakwenda. Sasa hilo jambo ni la kufikiria kabisa katika Ofisi ya Waziri Mkuu wewe ndiyo mwenye sauti kubwa na watakusikia. *(Makofi)*

Lakini jambo la pili, kuna ustaarabu kweli mabango yamewekwa ya utangazaji. Lakini mabango hayo wakati mwingine mengine ni makubwa mno na yanawekwa mbele ya nyumba za watu, juu magorofani kukinga hali ya hewa, kabisa haingii na hayapendezi wakati mwingine. Lakini pia mabango mengine ni mafupi yako barabarani ambayo yanazuia kabisa dereva asiweze kuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine kinachonikera sana biashara zimezuka, zimetapakaa katika makazi ya watu. Kwa mfano barabara ya Haile Selasie, utaona baa zimeongoza upande mmoja, baa upande wa pili. Sasa huwezi kuelewa waliopanga miji wamepangaje au wamefanya kinyemela tu kuwapa watu nafasi ya kuweka biashara zao. Hili jambo linatia uchungu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miji midogo pia imeachiwa, imezuka na inapanuka bila mpangilio wowote. Matokeo yake siku moja watakuja kuamua kuweka barabara au miundombinu mingine nyumba zitabomolewa, watu watanung'unika, halafu Serikali itasema haina pesa za kutosha kuwafidia. Sasa kwa nini tusianze mapema kuangalia eneo hili tukakataa?

Ushauri wangu ninaotaka kutoa kwa sasa kwa upande wa mazingira, kinachosemekana hapa kuwa fedha hazitoshi, lakini mimi ninachosema siyo fedha hazitoshi katika mambo ya mazingira, ila ni kuwa usimamizi na ukaguzi ndiyo hautoshi yaani haupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shauri langu katika tawala ni kuwa tuwe basi na chombo, kiwekwe chombo madhubuti cha kuangalia usimamizi na ukaguzi ambao ni *supervision inspectorate.* Chombo hiki kiwe na Wajumbe kutoka watu wanaojitegemea binafsi kutoka *NEMC*, kutoka *TCI* na pia kutoka Mabaraza ya Viwanda ambayo ni *CTI.* Tafadhali tukipata hiki chombo tuna hakika kitafanya kazi na kitasimamia ukaguzi na pia kitatoa taarifa wakati wote katika Serikali yetu Kuu na kitatoa taarifa katika Halmashauri za Jiji. Upande wa pili kuhusu sehemu za burudani na mapumziko na *open spaces. Open spaces* nyingi hata hapa Dodoma zimevamiwa kujengwa majumba. Sasa nilikuwa nataka kutoa ushauri kuwa kuwekwe mkutano kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili wahusishe mabenki waangalie maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengi ya kusema lakini nashukuru, ahsante na naunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa hotuba nzuri walizotoa, hotuba ambazo zinaonesha mwelekeo wa nini kilichofanyika kwa miaka ya nyuma na vilevile inatuelekeza ni nini kitakachofanyika katika mwaka huu wa 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba kwa miaka hii mitano ambayo Chama chetu cha Mapinduzi kimepewa madaraka ya kuongoza nchi yetu, kwa kiasi kikubwa sana imeweza kuleta maendeleo ambayo hata wananchi kule nyuma walikuwa wanashangaa kama maendeleo haya ya miaka mitano kama yangekuwa yanatokea tangu mwaka 1961, mpaka sasa nchi yetu ya Tanzania ingekuwa imenawiri sana na wala isingekuwa katika hali hii ya sasa, tungekuwa mbali. Hii inadhihirishwa na uongozi imara wa viongozi waliokuwepo wa kusimamia vizuri Serikali yao na kuhakikisha kuwa kila kinachopangwa kwenda katika ngazi mbalimbali kinafika na kinatekelezwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kwa ufupi tu kwamba Chama cha Mapinduzi, na hasa katika Jimbo la Kibiti na Wilaya nzima ya Rufiji kimefanya kazi kubwa sana. Kimefanya kazi kubwa katika huduma za jamii, kimefanya kazi kubwa sana katika sekta

mbalimbali, kwa mfano kwenye Jimbo letu la Kibiti, nianzie katika mradi mmoja mkubwa wa maji ambao haupo katika Wilaya au vijiji vingine vyote, kijiji kile cha mji wa Kibiti pekeyake kimepewa zaidi ya bilioni 4 na milioni 600 kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji ambao tunatarajia utafunguliwa mwezi wa nane mwaka huu. Mradi huu ni mradi ambao kwa kweli umewapa faraja kubwa wananchi wa Kibiti ambao walikuwa wanahangaika kwa muda mrefu bila kuwa na maji na umewapa imani kubwa sana kwamba Serikali yao inapoamua jambo lake basi inalitekeleza. *(Makofi)*

Lakini mji wa Kibiti kwa kiasi kikubwa tumeweza kuimarisha hospitali yetu, kituo chetu cha afya kilichokuwa pale Kibiti, kimeimarishwa sana na sasa hivi kile kituo cha afya kimekuwa na kazi kubwa ya kuweza kutoa huduma kwa Jimbo zima hasa la Kibiti. Kulikuwa hakuna huduma za *operations*, lakini sasa hivi zinafanyika na akina mama wale wanaojifungua badala ya kwenda Utete ambako ni zaidi ya kilomita 85 kutoka Kibiti, sasa wanafanyiwa shughuli zote palepale Kibiti, bila ya kwenda huko Utete ambako ni mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huduma nyingi za jamii ambazo zimefanyika, kuna maradi wa umeme, tunatarajia umeme huu utawaka sio zaidi ya wiki mbili kutokea sasa kwa sababu majaribio tayari yameshafanyika na kazi yote imekamilika. Kuna miradi ya elimu, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, imeboreshwa sana katika Jimbo letu la Kibiti na Wilaya ya Rufiji. Kwa ujumla kazi kubwa imefanyika kwenye wilaya hii ya Rufiji. Nimshukuru sana Mama Salma Kikwete, kwa kutoa mchango mkubwa wa elimu katika Jimbo la Kibiti, kupitia taasisi yake ya *WAMA* na *KAYAMA*, imejenga shule kubwa sana pale Nyamisati na imeanza kufanya kazi mwaka huu na imewachukua wanafunzi 90. Tunatarajia mwakani watakuwa wanafunzi wengi zaidi watakaojiunga na shule hii; shule hii ni ya Kitaifa inachukua wanafunzi kutoka katika kila wilaya ya nchi yetu. Nampongeza sana Mama Salma Kikwete kwa jitihada zake za kuimarisha shule pale Nyamisati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali kupitia mradi wa *MASEMP* katika Jimbo la Kibiti, tuna eneo la *delta* ambalo lina urefu wa zaidi ya kilomita 70 kutoka kijiji cha kwanza kule Pombwe mpaka kijiji cha mwisho Simbaulanga, urefu wake ni kilomita 70. Lakini kupitia mradi wa *MASEMP* kwa kiasi kikubwa kila kijiji sasa hivi kina maboti ambayo yanatumika kwa ajili ya usafiri na kwa ajili ya uvuvi.

Serikali ya Awamu ya Nne imetoa zaidi ya shilingi milioni 700, wamepewa wananchi bure, sio kwa mkopo wala kitu kingine chochote, wananchi wamewezeshwa na sasa hivi kupitia vikundi mbalimbali walivyoviunda wana mashua zao na wengine wana boti kwa ajili ya kuhakikisha kuwa ustawi wao unapatikana na maendeleo. Kwa sasa hivi kwa kweli yanazidi kuwa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu. Jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la watumisi wa Idara yetu ya Afya; kama wiki mbili zilizopita nilikwenda Wizarani, nilipokwenda Wizara ya Afya nilikwenda kuangalia mgawanyo wa watumishi ambao tunatarajia kuwaajiri katika wilaya yetu ya Rufiji kwa mwaka 2010/2011, jambo la kushangaza kabisa, nafika pale

yule Daktari anatuambia kwamba kwa mwaka huu wilaya ya Rufiji kuna mgawanyo wa kupewa *Nursing attendant* sita tu. Nilishangaa, wilaya kubwa kama ya Rufiji yenye zahanati na vituo vya afya zaidi ya 59, leo mgawanyo kwa mwaka mzima tunapewa watumishi sita wa Idara ya Afya! Suala hili linakwenda namna gani? Sasa namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa Waziri wa Afya, hebu waangalie upya huu mgawanyo; tuna zahanati tumezijenga hazina watumishi mpaka sasa, sasa unapotoa watumishi sita tu, watafanya kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nilitaka nizungumzie suala zima la *arrears* kwa watendaji wa vijiji. Suala hili tumelizungumza kwa muda mrefu, kuna watendaji wa vijiji na watendaji wa Kata ambao wameajiriwa kwa muda mrefu sana, walipoajiriwa hawakupata mishahara yao, wamekuja kuipata muda umepita zaidi ya miezi 10, 12, lakini ajira zao zilikuwa nyuma huko. Wanadai *arrears* toka mwaka 2007 lakini mpaka leo hawajapata! Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba Ofisi yako iweze kuhakikisha kwamba watendaji hawa nao wanapata *arrears* zao ili waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ombi tu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna barabara nyingi tumezijenga kwa mradi wa *TASAF*. Barabara hizi tokea zilipotengenezwa mpaka sasa nyingi hazipati huduma nzuri, baada ya kutengenezwa zimeachwa tu. Ombi langu ni kuwa barabara zote za *TASAF* hapa nchini, wenzetu wa Miundombinu hebu wazipandishe barabara hizi ziwe ni barabara za wilaya badala ya kuwa ni barabara za vijiji ili ziweze kuhudumiwa. Serikali imepoteza fedha nyingi sana kuzitengeneza. Ombi langu ni hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, barabara hizi ziweze kuchukuliwa na wenzetu wa Miundombinu ziwe barabara za Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni maombi ya mgawanyo wa wilaya. Tulizungumza kwa muda mrefu kwamba Wilaya ya Rufiji ina eneo la *delta*, Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe unalifahamu. Eneo lile kama unataka kulitembelea kupitia kijiji hadi kijiji, inachukua zaidi ya siku kumi hujamaliza, *delta* peke yake ambako kuna Kata nne na Jimbo la Kibiti kuna Kata 15. Tulitoa maombi yetu rasmi yapo mezani kwenu, hebu tuangalieni, tupendeleeni, lile Jimbo ni gumu, hata mimi Mbunge kutembelea Jimbo lile napata shida sana. Sasa nilikuwa naomba tu hayo maombi hebu yafikiriwe, waangalie mazingira ya *delta* ni magumu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama ilivyo ada na mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wataalamu wake, wasaidizi wake wote, kwa kuweza kuandaa hotuba ambayo imefika kwetu katika Bunge hili kwa ukamilifu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Ngorongoro kwa kunichagua katika kipindi cha miaka mitano na sasa tunaelekea kumaliza mkataba waliotupa wananchi lakini *Inshallah*, tunategemea kurejea na hasa niwashukuru wananchi wa Tarafa ya Sale, Tarafa ya Loliondo na Tarafa ya Ngorongoro kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana kwa pamoja kushughulikia suala la

amani, kwa sababu bila amani maendeleo yote haya yasingewezekana. Kulikuwa na migogoro kati ya Wamasai na Wabatemi au kwa jina lingine Wasonjo, lakini tumefanya kazi hiyo na wilaya sasa ina amani, iko shwari kabisa. Pia tulikuwa na matatiazo ya migogoro ya vijiji, wizi wa mifugo wa hapa na pale baina ya makabila hayo, lakini tumeshughulika na sasa hali ni shwari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wilaya ya Ngorongoro katika kipindi ambacho mimi nimekuwa madarakani, tumepata matatizo makubwa ya aina mbili; tulikuwa na tatizo kubwa la maafa yaliyosabishwa na mlipuko wa mlima Oldonyo Lengai, ambayo kwa sehemu kubwa kwa kweli ulituletea mataizo makubwa kwa upande wa watu, kwa upande wa mazingira, kwa upande wa wanyamapori, umelazimisha shule kadhaa kufungwa, umetuletea matatizo makubwa. Lakini nashukuru kwamba kwa kweli tumepata usaidizi kwanza kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kusaidia chakula, nashukuru sana Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi na Bodi ya Ngorongoro walioidhinisha pesa kusaidia chakula kwa ajili ya mlipuko huo. *(Makofi)*

Lakini vile vile tulipata usaidizi kutoka kwenye Serikali Kuu, kuanzia kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, Mashirika ya Dini na Mashirika ya Kimataifa, baada ya sisi kuwa tumekwenda kuomba misaada hiyo na kwa kweli wametupa msaada na hali hiyo ilimalizika shwari na salama kabisa. Nawashukuru wote waliotusaidia katika kipindi hicho kigumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa ambalo tumelipata ni tatizo la ukame. Kama mnavyofahamu mwaka jana kulikuwa na ukame mkubwa sana uliouwa mifugo kwa wingi, mifugo ambayo hawa wafugaji wa Ngorongoro wanaitegemea kwa 100%, kwa kweli wamepuputika kwa sehemu kubwa sana. Lakini *Inshallah* Mwenyezi Mungu vilevile ametusaidia na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, amesema tutaangalia uwezekano wa namna ya kuwasaidia hao watu walioathirika na ukame huo katika Wilaya ya Ngorongoro na katika Wilaya ya Longido na hata kule Simanjiro na maeneo ambayo kwa kweli mifugo ya wafugaji imekufa kwa wingi sana kutokana na ukame huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ni jambo ambalo ni la msingi pia kwa maisha ya binadamu. Msingi wa elimu unaanzia chekechea, shule ya msingi, sekondari, unakwenda na vyuo vya kati na vyuo vya elimu ya juu. Bila kuweka msingi kwa maana ya chekechea na shule za msingi, huku juu elimu inaweza isiwe *stable* sana. Lakini naiomba sana Serikali itusaidie kule Lainokanoka, kuna sekondari ambayo huu ni mwaka nadhani wa saba tunahangaika na ile sekondari, lakini haijakamilika. *(Makofi)*

Nashukuru kwamba imeanza, wameanza kujenga imefikia msingi na wengine wanapandisha matofali, lakini bado shule hiyo huu ni mwaka wa sita au wa saba tunakwenda haijakamilika na sijui hasa tatizo ni nini? Kwa sababu tatizo la kwanza lilikuwa ni tathmini ya mazingira *(environmental impact assessment)*, hilo limeshafanyika, imefanyika na shule imeanza kujengwa. *(Makofi)*

Sasa naomba Serikali iweze kutia mkono wake ili iweze kwenda kwa kasi zaidi, kwa sababu katika Jimbo langu la Uchaguzi au katika wilaya ya Ngorongoro hatuna

shule nyingi sana za sekondari na kama tunazo sio zaidi ya nane wakati wenzetu wanazungumzia shule zaidi ya 10, 15, 20. Elimu ni jambo ambalo ni la msingi sana na hata sisi ni lazima tuhangaike na elimu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni la mawasiliano. Hili suala tumehangaika nalo na hasa simu za mkononi kwa muda mrefu; namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kuna wakati alikwenda na kampuni za simu mpaka kijiji changu cha Ngalesero kule Ziwa Natron, akapeleka kampuni zote lakini mpaka sasa hivi bado hatujafanikiwa kupata mawasilaino ya simu katika eneo lile na bahati mbaya, eneo lile kwa kweli huwa linapata ajali ya ndege kuanguka pale, huwa zinaangukia hata kwenye Ziwa Natron pale. Hakuna namna ya kupeleka taarifa kwa haraka ili kuomba msaada. *(Makofi)*

Nawashukuru wananchi wa maeneo yale, mara zote wao wamekuwa ndio wanakimbia kwenda kutoa msaada huko na naomba sasa Serikali ya Mkoa na Serikali Kuu, itusaidie kwa kweli maeneo yale. Najua kwamba Serikali haifanyi biashara lakini inaweza kutoa ushawishi na msukumo ili tuweze kupata mawasiliano katika eneo la vijiji vya Ziwa Natron na hasa kule Ngalesero, Monik, Kinyin, Laparkashi, sehemu za Malampo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majina ni magumu kidogo lakini ni mazuri tu. Jambo lingine ni kwamba naishukuru sana Serikali kwa hatua ambayo imeichukua hivi karibuni kujaribu kwenda kupima vijiji katika Tarafa ya Loliondo ili kuweza kuondosha migogoro iliyotokea, migogoro ya ardhi kati ya wawekezaji na wananchi. Naomba tu jambo hili liwashirikishe wananchi kikamilifu ili kama wana maoni tofauti wasikilizwe lakini pia na wananchi tutawaomba wasikilize upande wa Serikali ili kuweza kufikia muafaka na hatimaye kuondoa migogoro iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru kwa nafasi uliyonipa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri kabisa pamoja na Waziri wa TAMISEMI na Naibu Waziri wake. Lakini mimi nampongeza Waziri Mkuu katika aina tofauti kabisa, kwa mara ya kwanza kabisa hotuba ya Waziri Mkuu anasimama anamuachia Waziri wake kwanza atoe utekelezaji, halafu yeye ndio aje amalizie. Hii ni kuthamini kwamba ninao wenzangu ambao ninafanya nao kazi, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wajibika kupongeza watendaji wanaoandamana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu kule waliko Morogoro kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Wa kwanza ni Mkuu wa Mkoa, tuna Mkuu mpya kabisa wa Mkoa, ndugu yangu Machibya; yeye ni mwanajeshi hasa na anaonesha kweli utendaji wake wa kijeshi na si kwa mabavu, kwa akili na utamaduni mpya kabisa ambao ametuletea na tungependa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa muda huu ambao yule bwana yupo, kidogo msimsogeze,

kwa sababu yeye na *RAS* wake ni kama pete na chanda na wanafanya kazi vizuri sana. Kwa hiyo, sisi tumefurahi kusema kweli, kwa muda mfupi tu aliokuwepo pale, anaujua mkoa wote na miradi yote. Ukizungumza na yeye atakuambia ni mradi gani una matatizo. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Vile vile tunashukuru kwamba ameshirikiana sana na *DC* wake kwa sababu katika migogoro ya wakulima na wafugaji kwa hakika watu hawa wawili wasingeshirikiana nadhani tungekuwa katika hali ile ya Kilosa. Lakini ushirikiano wao umeweza kabisa kuwapatanisha wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja ya Jimbo. Morogoro Vijijini kwa bahati mbaya sana tunahemea, tumepanga Makao Makuu Morogoro Mjini. Tunatoka kilomita 194, kutoka Kidunda au kutoka *Kisaki Station,* mikutano yote tunafanyia Mjini Morogoro. Kwa hiyo, ni lazima tusafiri huko, tulale huko, tufanye mikutano halafu asubuhi yake ndio turudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha hiyo tumeifanyia maamuzi na maamuzi ni kwamba tunataka kuhamisha Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwenda Kijiji cha Mvuha na tunafanya hivi makusudi kwa sababu hiki ni kijiji ambacho kipo katikati ya wilaya, kwa hiyo kila pembe ya wilaya ni rahisi kuja pale kufanya mikutano, kufanya shughuli za Kiserikali na kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba rasmi kwa makusudi kabisa kwenye Bajeti, tumeomba ombi maalum la shilingi bilioni moja katika Ofisi ya Waziri Mkuu ili atuwezeshe kuhama na kwetu kuhama pale ni muhimu sana kwa sababu ama sivyo tutaendelea kuwa wapangaji, tutaendelea kuwa na maendeleo duni, ni maendeleo tunayoendeleza Mji wa Morogoro na sio Halmashauri ya Morogoro Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiit, ikumbukwe Morogoro kuna Manispaa na hapo hapo sisi tumepanga kama Halmashauri, kwa hiyo tunataka kuhama ili tuendeleze Halmashauri yetu; hatutaki kumuhamisha *DC,* hapa naomba nieleweke kabisa kwamba sisi hatuna haja ya kumuhamisha *DC. DC* wetu akae Morogoro Mjini, sisi Halmashauri tu tunataka kuihamishia Morogoro Vijijini, kwa sababu tunadhani kwamba kwa *DC* kukaa Morogoro Mjini, bado anaweza kuhudumia Manispaa na Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itusikilize na ninaamini itatusikiliza, kwa sababu wakati Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Matombo, alimuuliza Mkurugenzi wa Halmashauri; ninyi bado mko Morogoro tu? Na yeye akasema tunapanga kuhama. Akasema, mna mipango gani ya kuhama? Mmeweka kwenye Bajeti? Akasema hapana. Akasema ni lazima mwaka huu muweke kwenye Bajeti ili mhame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna huo mkono na kwa bahati nzuri Mkuu wa Mkoa na yeye amelidakia hili vizuri sana na kabisa yuko katika msisitizo kwamba Morogoro Vijijini ni lazima ihamie Mvuha. Kwa hiyo, tunaomba sana Ofisi ya Waziri

Mkuu, itusaidie katika hili. Tunaomba tusaidiwe tuhame kutoka Morogoro Mjini kwenda Morogoro Vijijini na hili linawezekana tu kwa Serikali kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, naona muda unakimbia sana, lingine kubwa ni ombi. Tuna vijiji ambavyo vinaweza kuwa miji midogo, kijiji kimojawapo ni Mtamba ambacho kipo kwenye Tarafa ya Matombo, kijiji kingine ni Dutumi ambacho ni vijiji viwili vimetengwa kwa sababu ya ukubwa, lakini kutengwa kwao ni kwa mpaka wa Mto tu. Dutumi ni mahali ambapo palikuwa na kiwanda cha kusindikia pamba *(ginnery)*, kwa hiyo, ni kijiji kikubwa sana na hivyo tunawaomba iwe ni mji dogo. Hali kadhalika tungeomba *Kisaki Station* nayo vilevile iwe ni mji mdogo. Ni mahali pakubwa sana na nadhani inawezekana kabisa. Wataalamu wanaweza kwenda kule na kuangalia uwezekano wa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni shukrani kwa Serikali, kutuwezesha sisi katika Jimbo la wilaya yote ya Morogoro Vijijini, kuwa na mtandao wa simu za viganjani. Tunashukuru sana kwa sababu tunaweza kuwasiliana katika wilaya yote kwa simu ya kiganjani, hivyo tunashukuru sana. Lingine tena ni shukrani kwamba Serikali imeweza kabisa kutuwezesha watu wa Morogoro Vijijini na hasa Jimbo la Morogoro Kusini ambalo mazingira yake ni mabaya sana ya milima na mabonde makubwa, lakini imeweza kutupatia barabara ya kupitika muda wote wa masika ama kiangazi, kutoka Morogoro mpaka *Kisaki Station*, tunashukuru sana.

Halikadhalika ziko barabara ambazo zinapitika wakati wote kutoka Msalabani kwenda Tawa, kwenda Kiboga, kutoka Tawa kwenda Kibungo Juu, huko kote kunaendeka bila matatizo. Kutoka Dutumi kwenda Kolelo kwenda Kasanga kwenda Singisa, huko kote kunaendeka kwa uwezo na mipango mizuri kabisa ya Serikali. Tunawashukuru sana kwa hili na hiyo inawezekana tu kwa sababu Serikali ya CCM inajali, inasikia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenegoha.

Waheshimiwa Wabunge, bado tuna idadi kubwa sio sana ya wachangiaji na kesho baada ya maswali tunakusudia kuendelea kutoa fursa za watu kuendelea kuchangia, lakini wakati huo huo tutakuwa tunazingatia ukweli kwamba Wizara hii ya Waziri Mkuu, wachangiaji wengi mmekuwa mkichangia mkizigusa sekta nyingi sana ambazo zinahusu Wizara tofauti tofauti. Sasa nadhani ingekuwa ni vyema mimi nisitoe hapa uamuzi ili nimuachie Mheshimiwa Spika au Mwenyekiti atakayekaa asubuhi, ili aje atoe muongozo mzuri zaidi wa namna gani ya kuweza kuwaruhusu mpaka Mawaziri wengine kuweza kusaidia majibu haya katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu, kwa sababu sekta zao zimeguswa. *(Makofi)*

Baada ya hapo, napenda sasa niliahirishe Bunge mpaka kesho saa tatu barabara za asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 18 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*